# UHAKIKI WA UBUNILIZI WA CHANGAMOTO ZA NDOA KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI KIUHUSIKA NA KIUSIMULIZI

**NA**

**MBERESIA BENARD TSIMANGO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**© 2021**

## IKIRARI

Tasnifu hii inatokana na utafiti wangu wa asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya shahada katika chuo kikuu kingine. Hakuna sehemu ya tasnifu hii inayoweza kutolewa bila idhini yangu na au Chuo Kikuu cha Maseno.

**Mberesia Benard Tsimango**
PG/ MA/ 00024/ 2012

Sahihi………………………… Tarehe…………………………..

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa kibali chetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maseno.

**Prof. Florence Indede**
Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Maseno

Sahihi………………………… Tarehe…………………………..

**Dkt. Nanyama Deborah Amukowa**
Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Maseno
S. L. P 333, Maseno

Sahihi………………………… Tarehe…………………………..

**SHUKRANI**

Ningependa kwanza kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, maarifa na uvumilivu wakati wote nilipokuwa nikisomea shahada hii ya uzamili. Ninatoa shukrani kwa wazazi wangu kwa kunipa moyo, kunishauri na kunihimiza kila wakati kuendelea kusoma zaidi. Shukrani pia ni kwa mke wangu Ruth Kamali, wanangu: Ivan Kiriza, Michelle Mengesa, Lean Yavwezi, Prince Tsimango na Acer Vidonyi. Uchangamfu na furaha yao ilituliza akili na kunipa motisha wakati wa kusomea shahada hii.

Ningependa kushukuru idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Maseno kwa kunipatia fursa ya kuendeleza masomo yangu. Ninawashukuru wasimamizi wangu Prof. Florence Indede na Dkt. Nanyama Deborah Amukowa kwa kujitolea na kunielekeza vyema wakati wa kipindi cha kusomea shahada hii ya uzamili.Shukrani pia ziwaendee Dkt. Asiko, Prof. Mohochi na Dkt. Lumwamu miongoni mwa wahadhiri wengine katika idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno. Wahadhiri hawa walinifaa sana kwa kunifundisha na kunishauri ipasavyo  wakati wa utafiti wangu.

Sina budi kuwashukuru wanafunzi wenzangu niliosoma nao wakiwa ni pamoja na Sospeter Arodi, Omondi Mango, Ochieng Faluja, Mourine Musindalo na Rebah Namarome. Hawa walinifaa sana wakati wa mijadala na pia kwa kunihimiza nisikate tamaa.

Ndugu zangu walinifaa kwa hali na mali wakati wa kipindi chote cha kusomea shahada hii; Edward Lisaliza, Judy Kamira, Edith Kasoha, Metrine Njemo, Sammy Chanzu na Irene Mideva wanastahili shukrani za dhati. Nawashukuru marafiki zangu na wale wote ambao walinifaa kwa njia mbalimbali wakati wa kusomea shahada hii ya uzamili.

# TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu Rahel Tsimango na Joseph Tsimango kwa kujikaza kisabuni kunilea licha yachangamoto nyingi walizokumbana nazo na kunihimiza kuendeleza masomo yangu.

## IKISIRI

Ndoa ni asasi muhimu inayoiendeleza jamii na kudumisha uthabiti wake kupitia majukumu yake muhimu ya kuhakikisha wanajamii wapya wanazaliwa na kulelewa. Tafiti za kifasihi na za kisosholojia kuhusu ndoa zinaonyesha kuwa inaendelea kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Tafiti za awali kuhusu ndoa katika fasihi ya Kiswahili zimebainisha changamoto zinazoiyumbisha na kufanya ishindwe kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hata hivyo, tafiti hizi zimeegemea uchunguzi wa usawiri wa maudhui ya ndoa katika kazi mahususi za kifasihi.Kuna haja ya kuchunguza namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia vipengele vya kibunilizi kwa kurejelea kazi mbalimbali za kifasihi. Kwa msingi huu, utafiti huu unahakiki namna uhusika na usimulizi umetumika kujenga changamoto za ndoa katika riwaya tofauti za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi tofauti. Lengo la utafiti huu ni kuhakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Madhumuni ya utafiti huu ni; kueleza jinsi changamoto za ndoa zimesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili; kutathmini namna athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili na hatimaye kufafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimewasilishwa kupitia mbinu za usimulizi. Utafiti huu unaongozwa na mseto wa nadharia ya umuundo- uamilifu kwa mujibu wa Merton (1957) na nadharia ya naratolojia kwa mujibu wa Genette (1980) na Kenan (1983). Muundo wa utafiti huu ni wa kiuchanganuzi. Eneo la utafiti huu ni la maktaba, muktadha wa fasihi na mahususi riwaya ya Kiswahili. Kundi lengwa ni riwaya za Kiswahili ambazo zimesawiri changamoto za ndoa. Usampulishaji dhamirifu uliwezesha kubainishwa kwa sampuli ya riwaya tano zifuatazo; *Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008). Data ilikusanywa kutoka kwa riwaya teule kwa kutumia mbinu ya unukuzi kwa kutumia orodha ya uchunzaji. Data ilichanganuliwa kimaudhui na kuwasilishwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba changamoto za ndoa kama vile umaskini zimesawiriwa kupitia uhusika wao kimatendo, kiusemi, kimazingira na wa muonekano wa nje. Aidha yanaonyesha kuwa athari za changamoto za ndoa kama vile ukosefu au upungufu wa mahitaji ya kimsingi zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao kimatendo, kiusemi, kimazingira na kwa muonekano wa nje. Hatimaye, matokeo haya yanaonyesha kuwa njia za kukabilia na changamoto za ndoa kama vile ushauri nasaha zimewasilishwa kupitia mbinu zifuatazo za usimulizi; usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa ndani, mtazamo wa nje, msimulizi tawasifu, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Matokeo yanaonyesha tofauti na kulingana katika matumizi ya uhusika na usimulizi katika kujenga changamoto za ndoa kwenye riwaya teule. Utafiti huu unatarajiwa kuonyesha namna uumbaji wa wahusika na mbinu za usimulizi zinasawiri maudhui; unachangia utafiti zaidi kuhusu ndoa katika fasihi ya Kiswahili kwa kuhakiki ubunilizi wa changamoto zake na kupanua uelewa kuhusu changamoto hizi.

# ABSTRACT

Marriage is an important institution that develops and maintains stability of the society through its important roles of ensuring that new members of the society are born and brought up. Literary and sociological researches on marriage show increase in its instability and failure to perform its roles effectively. Previous researches on marriage in Kiswahili literature have identified challenges that make it unstable and fail to perform its roles effectively. However, these researches have focused on studying the portrayal of the theme of marriage in specific literary works. Therefore there is need to study how marital challenges have been constructed through fictional elements in different literary works. On this basis, this research critiques how characterization and narration has been used to construct marital challenges in different Kiswahili novels written by different authors. The aim of this research is to critique characterization and narration in fictionality of marital challenges in selected Kiswahili novels. The objectives of this research are; to explain how marital challenges are portrayed through characterization in selected Kiswahili novels; to examine how effects of marital challenges are depicted through characterization in selected Kiswahili novels and finally to describe how ways of solving marital challenges in selected Kiswahili novels are presented through narrative strategies. This research was guided by two theories; structural- functionalism theory by Merton (1957) and narratology theory by Genette (1980) and Kenan (1983). This research employed analytical design. The study area of this research is library, literary context and Kiswahili novel and its target population is all Kiswahili novels that have portrayed marital challenges. Purposive samping of these novels resulted in a sample of the following five novels; *Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) and *Unaitwa Nani?* (2008). Data wa collected by citation technique using an observation schedule. The findings of this research show that marital challenges for example poverty have been constructed through characterization by action, speech, environment and outside appearance of characters. They also show that effects of marital challenges for example lack of or inadequate basic needs are depicted through characterization by either action, speech, environment or outside appearance of characters. Finally, they show that ways of addressing marital challenges such as guidance and counselling have been presented through the following narrative strategies; first person narration, third person narration, internal focalization, external focalization, heterodiegetic narrator, homodiegetic narrator and non- intrusive narrator.The findings show differences and similarities in use characterization and narration to construct marital challenges in the selected novels. This research is expected to demonstrate how characterization and narrative strategies portray themes. It enriches research on marriage in Kswahili literature by critiquing fictionality of its challenges and finally it will broaden understanding of these challenges.

# YALIYOMO

IKIRARI ........................................................................................................ ii
SHUKRANI ........................................................................................................ iii
TABARUKU ........................................................................................................ iv
IKISIRI ........................................................................................................ v
ABSTRACT ........................................................................................................ vi
YALIYOMO ........................................................................................................ vii
FASILI YA ISTILAHI ........................................................................................................ x
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........................................................................ 1**
1.1 Utangulizi ........................................................................................................ 1
1.2 Usuli wa Utafiti ........................................................................................................ 1
1.3 Swala la Utafiti ........................................................................................................ 8
1.4 Maswali ya Utafiti ........................................................................................................ 9
1.5 Madhumuni ya Utafiti ........................................................................................................ 9
1.6 Upeo wa Utafiti ........................................................................................................ 9
1.7 Misingi ya Uteuzi ........................................................................................................ 10
1.8 Kiunzi cha Nadharia ........................................................................................................ 11
1.8.1 Nadharia ya Umuundo-uamilifu ........................................................................ 12
1.8.2 Nadharia ya Naratolojia ........................................................................ 15
1.9 Hitimisho ........................................................................................................ 24
**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI ........................................................ 26**
2. 1 Utangulizi ........................................................................................................ 26
2.2 Usawiri wa Changamoto za Ndoa ........................................................................ 26
2.3 Udhihirishaji wa Athari za Changamoto za Ndoa ........................................ 31
2.4 Uwasilishaji wa Njia za Kukabiliana na Changamoto za Ndoa ........................ 34
2.5 Hitimisho ........................................................................................................ 36
**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................................ 38**
3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 38
3.2 Muundo wa Utafiti ........................................................................................................ 38
3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................................ 38
3.4 Kundi Lengwa ........................................................................................................ 39

3.5 Sampuli na Usampulishaji ........ 39
3.6 Ukusanyaji Data na Vifaa vya Kukusanya Data ........ 41
3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........ 41
3.8 Maadili Katika Utafiti ........ 42
**SURA YA NNE**: **UCHANGANUZI, UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO . 43**
4.1 Utangulizi ........ 43
4.2 Changamoto za Ndoa na Jinsi ambavyo Zimejengwa Kupitia Uhusika ........ 44
4.2.1 Ulevi na Usawiri wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi, Kimatendo, Kimazingira na kwa Muonekano wa Nje ........ 45
4.2.2 Talaka na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 49
4.2.3 Uasherati na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 52
4.2.4 Umaskini na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo, Kiusemi, Kimazingira na Muonekano wa Nje ........ 55
4.2.5 Kutowajibika na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 60
4.2.6 Ukosefu wa Watoto na Usawiri wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 65
4.2.7 Magonjwa na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo, Kiusemi, Muonekano wa nje na Kimazingira ........ 68
4.2.8 Kifo na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 74
4.2.9 Kushikilia kwa Utamaduni Hasi na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 77
4.2.10 Ugomvi na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 82
4.3 Udhihirishaji wa Athari za Changamoto za Ndoa Kupitia Usawiri wa Wahusika ........ 90
4.3.1 Kutatizika Kimasomo na Udhihirishaje Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 91
4.3.2 Ukosefu au Upungufu wa Mahitaji ya Kimsingi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi, Kimazingira na Kimatendo ........ 97
4.3.3 Ajira ya Watoto na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 103
4.3.4 Chuki ya Watoto kwa Wazazi, Huzuni, Ukiwa na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 105
4.3.5 Watoto Kuachiwa Jukumu la Ulezi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 109
4.3.6 Ndoa za Mapema na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 110

4.3.7 Matatizo ya Kiafya na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi na Kimatendo 112
4.3.8 Ukeketaji wa Wasichana na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi ........ 114
4.3.9 Kubaguliwa Kijinsia kwa Watoto na Wazazi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo ........ 115
4.3.10 Kunajisiwa na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika Kiusemi ........ 117
4.4 Njia za Kukabiliana na Changamoto za Ndoa na Jinsi ambavyo Zinawasilishwa na Mbinu za Usimulizi ........ 118
4.4.1 Mazungumzo na Jinsi ambavyo Yanawasilishwa na Mbinu Zausimulizi ........ 120
4.4.2 Ushauri Nasaha na Jinsi ambavyo Unawasilishwa na Mbinu za Usimulizi ........ 123
4.4.3 Msamaha na Jinsi ambavyo Umewasilishwa na Mbinu za Usimulizi ........ 129
4.4.4 Uvumilivu na Jinsi ambavyo Unawasilishwa na Mbinu za Usimulizi ........ 133
4.4.5 Kuanzishwa kwa Mradi wa Kuleta Pato na Jinsi ambavyo Kumewasilishwa na Mbinu za Usimulizi ........ 136
4.5 Hitimisho ........ 138
**SURA YA TANO: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEZO ........ 140**
5.1 Utangulizi ........ 140
5.2 Muhtasari ........ 140
5.3 Hitimisho ........ 147
5.4 Mapendekezo ya Kijumla Kutokana na Matokeo ya Utafiti ........ 150
5.5 Mapendekezo Kuhusu Utafiti wa Baadaye ........ 150
**MAREJELEO ........ 152**
**VIAMBATANISHO ........ 156**

## FASILI YA ISTILAHI

**Uhusika-** mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katikakazi yake.

**Usimulizi-** uelezaji wa matukio katika hadithi.

**Ubunilizi-** istilahi ambayo asili yake ni Kilatini na inamaanisha kujenga/kuumba/kuunda.

**Mbinu za kiusimulizi-** mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kusimulia hadithi yake.

**Usawiri-** neno hili hutumiwa kwa maana mbalimbali. Kwanza, kueleza utoaji wa picha fulani. Pili, hutumiwa kuelezea uumbaji wa wahusika. Katika utafiti huu imetumiwa kuelezea uumbaji wa wahusika na pia wa changamoto za ndoa.

**Usawiri wa wahusika-** hii ni dhana inayotumiwa kuelezea jinsi wahusika wa kifasihi walivyochorwa au kuwasilishwa na msanii au mtunzi wa kazi fulani.

**Uhusika wa kimatendo**- mbinu ya kuwajenga wahusika kupitia matendo yao.

**Uhusika wa kiusemi-** mbinu ya kuwasawiri wahusika kwa kutumia matamshi au mawazo yao.

**Uhusika wa kimazingira-** mbinu ya kuwasawiri wahusika kwa kutumia mazingira yao kwa mfano makaazi yao au hali ya watu wanaowazunguka.

**Uhusika wa muonekano wa nje-** mbinu y a kuwasawiri wahusika kwa kutumia maumbile yao au mavazi yao.

**Usimulizi wa nafsi ya kwanza**- Usimulizi unaofanywa na mmoja wawahusika katika kazi ya kifasihi anayeeleza matukio anayoshiriki au anayoshuhudia.

**Usimulizi wa nafsi ya tatu-** usimulizi unaofanywa na msimulizi anayeeleza matukio wanayoshiriki wahusika wengine.

**Mtazamo**- hii ni dhana inayoelezea aliko msimulizi anapoyaangalia matukio katika hadithi.

**Mtazamo wa ndani-** huu ni mtazamo unaojitokeza katika hadithi inayosimuliwa na msimulizi ambaye anapatikana ndani ya ulimwengu wa hadithi anayosimulia au mshiriki katika hadithi au matendo anayosimulia.

**Mtazamo wa nje-** huu ni mtazamo unaojitokeza pale ambapo msimulizi yuko nje ya ulimwengu wa hadithi anayosimulia au si mshiriki katika matukio ya hadithi anayosimulia.

**Msimulizi wasifu-** msimulizi ambaye anasimulia matukio ya hadithi ambayo hashiriki.

**Msimulizi tawasifu-** ni msimulizi ambaye ni mhusika katika hadithi na husimulia matukio ya hadithi ambayo yeye anashiriki na kuathiriwa nayo.

**Msimulizi wasifu horomo-** ni msimulizi ambaye hutoa habari tu na kuwaacha wahusika wazungumze wao wenyewe kwa wenyewe bila kuwaingilia kati au kutoa ushauri na maamuzi fulani ya kimsingi.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1Utangulizi

Katika sura hii maelezo yametolewa kuhusu usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya uteuzi na misingi ya kinadharia. Maelezo kuhusu vipengele hivi yalitoa mwelekeo kuhusu utafiti uliofanywa. Yalibainisha mada ya utafiti, pengo la kiutafiti, umuhimu wa utafiti huu na nadharia zilizotumiwa. Maswali yaliyoongoza ukusanyaji data na madhumuni ya utafiti yameorodheshwa.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Asasi ya ndoa imejadiliwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo wa Sosholojia na fasihi ya Kiswahili. Wataalamu wa Sosholojia ambao wameijadili ndoa ni Vidya na Sachdeva (2007), Durkheim (1962), Parsons (1951), Selfe (1993), Giddens (2006), Schaefer (2008), Macious (2002), Charles (2008), Masua (2016) na Odhiambo (2013). Ndoa ni asasi ambayo huleta mume na mke pamoja ili kuanzisha familia (Vidya na Sachdeva, 2007). Asasi hii inatarajiwa kutoa mazingira bora ya kuza na kulea kizazi kipya ambacho kinategemewa kuiendeleza jamii. Ndoa ni mojawapo ya asasi zinazounda mfumo wa jamii na hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Asasi hii hudumisha jamii kupitia majukumu yake ya kuhakikisha wanajamii wapya wanazaliwa, wanakidhiwa kwa mahitaji yao na kufunzwa kanuni na amali za jamii zao (Durkheim,1962).

Talcot (1951) anaeleza kuhusu haja ya wanandoa kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili majukumu ya ndoa kwa jamii yaweze kutimizwa. Kulingana na mtaalamu huyu mume anatarajiwa kuwa kiongozi wa familia na akimu mahitaji yake. Mke naye anatarajiwa kuwa mnyenyekevu, mpole na mtunzi wa familia na nyumba yake. Hata hivyo mabadiliko yameisha yamesababisha mabadiliko katika majukumu ambayo wake na waume wametengewa kijinsia. Wanawake sasa wanajihusisha na shughuli za kutafuta pato na kuchangia mahitaji ya familia badala ya kumtegemea mume kulingana na mtaalamu huyu.

Ndoa imesawiriwa kama asasi inayokumbwa na matatizo mengi licha ya kwamba imetengewa majukumu muhimu ya kijamii ya kuzaa na kulea kizazi kipya. Masua (2016) anasema kuwa kuna ongezeko la ukosefu wa uthabiti katika ndoa kote duniani. Hii ni kwa sababu ya

kuongezeka kwa talaka na utengano. Odhiambo (2013) katika utafiti wake kuhusu mizozo ya kindoa na vyanzo vyake nchini Kenya anagundua kuwa kuna ongezeko la mizozo katika ndoa nchini. Ongezeko la ukosefu wa uthabiti katika asasi hii unatatiza utekelezaji wa majukumu yake ya kijamii. Gicuku (2012) anaisawiri ndoa kama asasi ambayo imeshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na changamoto mbalimbali zinaizokumba. Hii inaathiri maisha ya watoto na uthabiti wa jamii kwa ujumla. Asasi hii imechorwa kuwa inayokumbwa na changamoto nyingi zinazoifanya ikose uthabiti na kushindwa kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya kijamii ya kuzaa na kulea kizazi kipya.

Charles (2008) anasema asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi kwa mfano ulevi, uasherati, wivu, matatizo ya kifedha, mapigano na mgongano wa maslahi ya wanandoa. Macious (2002), Giddens (2006), Sachdeva na Vidya (2007) na Schaefer (2008) wanatoa maelezo zaidi kuhusu changamoto za ndoa. Wanasema kuwa ndoa inakumbwa na changamoto kama vile umaskini, kutotoshelezwa kwa tendo la ndoa, mauaji, ukosefu wa mawasiliano, uhasama, ugumba, utasa, ugomvi na ukosefu wa mapenzi. Hizi changamoto zinafanya asasi hii kukosa uthabiti ambao ni muhimu katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Selfe (1993) kwa kurejelea taaluma ya Sosholojiaanatoa maelezo kuhusu atharihasi za talaka kwa jamii. Talaka huvuruga familia na kutatiza maisha ya wazazi na watoto wao. Wanaweza kukosa usalama, utambulisho, makao mazuri na huduma nyingine muhimu kama elimu bora kwa watoto. Kuvunjika kwa ndoa husababisha viwango vya juu vya mawazo, kuongezeka kwa matatizo ya kiafya, ulevi na kujiua. Talaka hutatiza watoto na kuwafanya kuwa na matatizo ya kiakili na kitabia. Pia husababisha kuongezeka kwa familia za mzazi mmoja na kufanya ulezi wa watoto kukumbwa na shida nyingi. Talaka imewafanya watu kuwa na mwelekeo hasi kuhusu ndoa na kuwafanya kuamua kuishi bila kuoa au kuolewa ama kuishi katika ndoa mjarabu. Ndoa mjarabu ni ndoa ambazo hazijaidhinishwa kulingana na sheria, dini au utamaduni wa jamii.

Charles (2008) anajadili athari za talaka kwa jamii kwa ujumla. Anasema kuwa talaka husababisha umaskini ambao hulazimu jamii nzima kuingia gharama za kuushughulikia. Hii athari hutokea katika ndoa ambazo zilikuwa na pato la chini. Jamii huingia gharama kama za kupunguzia waliotalakiana kodi za nyumba kwa kulipa sehemu ya kodi hiyo, kulipa mawakili

wanaohusika na kesi za talaka na ukusanyaji wa pesa za kugharamia mahitaji ya wake na watoto baada ya talaka.

Gichinga (2005) anasema kuwa changamoto za ndoa zinachukua nafasi ya pili miongoni mwa matatizo yanayowafanya watu kuendea ushauri nasaha nchini Kenya. Anasema kuwa ndoa nchini zinakabiliwa na changamoto kama vile kuthuriwa kimwili na kiakili, magonjwa, uasherati, unywaji pombe na matumizi ya vileo kupindukia, matatizo ya kifedha, kukosa kupata watoto, kutatizwa na jamaa za wanandoa na pia kutoridhika na tendo la ndoa. Mtaalamu huyu anajadili athari za changamoto za ndoa kama vile mawanandoa kutoroka kila mara na kurudi, waume kukaa kwa vyumba vya starehe muda mrefu ili kuepuka mizozo nyumbani  na wanandoa kuishi tu pamoja bila kuhusiana kama mke na mume. Athari kwa watoto ni kutelekezwa na wazazi na kuwa na tabia zisizofaa.

Odhiambo (2013) amechunguza mizozo ya ndoa nchini Kenya na vyanzo vyake. Amegundua kuwa kuna ongezeko la mizozo katika ndoa nchini. Mizozo hii inasababishwa na mapato madogo, kutokubaliana kuhusu majukumu kati ya wanandoa, kunywa pombe kupindukia, uchezaji kamari, utesaji wa watoto ambao hawajazaliwa na wanandoa wote na pia wa jamaa za wanandoa na mwingilio kutoka jamaa za wanandoa. Anaeleza kuwa mizozo zaidi ya kindoa husababishwa na mwanandoa mmoja kumpinga mwenzake anapotaka kuwaadhibu watoto, uasherati, mmoja kuchunguza mienendo ya mwenzake kisiri na mume kukosa kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya kuikimu familia naye mke kukosa kutekeleza ipasavyo majukumu ya nyumbani kama vile kazi za nyumba na kulea watoto.

Masua (2016) anasema kwamba kuna ongezeko la ukosefu wa uthabiti katika ndoa kote duniani. Anamefanya utafiti kuhusu ukosefu wa uthabiti wa ndoa miongoni mwa wanawake katika sehemu za mashambani na athari zake. Ametumia kaunti ya Machakosi nchini Kenya kama eneo la utafiti wake. Anajadili sababu ambazo zinafanya ndoa kukosa uthabiti na kuwafanya wake kuwataliki au kutengana na waume wao. Sababu hizi ni unywaji pombe na utumiaji wa vileo vingine kupindukia, kulazimishwa kushiriki mapenzi na kupigwa wanapokataa, kutowajibika kwa waume, uasherati, ghasia, ukosefu wa ajira kwa mume, tofauti za kiumri, ukewenza, kuthuriwa kimwili, utasa, kukosa kupata mtoto wa jinsia inayopendelewa, mume kuoa mke

mwingine, kuingiliwa na jamaa za mume na uchawi au mapepo.Mtaalamu huyu anajadili athari za ukosefu wa uthabiti wa ndoa kwa wake na watoto baada ya ndoa talaka au utengano kwa mfano umaskini na kutatizika kwa masomo ya watoto.

Durkheim (1962), Selfe (1993), Giddens (2006),Schaefer (2008),Macious (2002),Charles (2008),Sachdeva na Vidya (2007), Masua (2016) naOdhiambo (2013) wameshughulikia ndoa kwa kurejelea taaluma ya Sosholojia. Gichinga (2005) ameshughulikia ndoa kwa kurejelea taaluma ya Ushauri Nasaha. Wataalamu hawa sawa na utafiti huu wameshughilia suala la changamoto za ndoa. Hata hivyo utafiti huu ni wa kifasihi na unachunguza ndoa kwa kurejelea kazi za kubuni za fasihi ya Kiswahili. Umechunguza uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili.

Wataalamu wa fasihi ya Kiswahili sawa na wa Sosholojia wametoa taswira hasi ya ndoa katika uandishi na tafiti zao.Wamitila (2002) anasema ndoa ni asasi ya kitamaduni ambayo imejengwa kwa mila na desturi zinazompendelea mume na kumkandamiza mke. Anatoa maelezo kuhusu ndoa kwa kuegemea jinsia ya kike. Mke anabaki kuwa chini ya mamlaka ya mumewe na kulazimika kufuata maamuzi yake yote. Mke anakuwa kama chombo kinachomilikiwa na mumewe, hashauriwi wala kushirikishwa katika maamuzi muhimu ya ndoa. Mtaalamu huyu anaisawiri ndoa kama asasi ambayo inamkandamiza mke na kumkuza mume. Inachukulia kuwa katika ndoa mume anamkandamiza mke ilihali utafiti unaonyesha kuwa waume huteswa na wake wao. Gitau (2005) anasema kuwa wanaume katika ndoa huteswa na wake wao kwa kutukanwa, kupigwa, kudharauliwa, kutengwa na jamaa zao na kushiriki uasherati. Wao huteswa na wake zao kwa kushindwa kuikimu familia au kwa kuwadhulumu.

Katola (2006) amechunguza udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia ya Kiswahili. Anasema kuwa ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazomdhulumu mwanamke. Anaeleza kwamba wanawake walio katika ndoa hukumbwa na changamoto nyingi kama vile kunyimwa haki ya kumiliki mali, kutoa maoni kuhusu maswala muhimu katika ndoa, kuwa chini ya mamlaka na amri za mumewe, kuchukuliwa kuwa ni mali ya mumewe na kutoelezea kutoridhika kwake.

Nyaosi (2008) ametafiti kuhusu taswira ya ndoa katika riwaya mbili za Kiswahili, *Kiu* (1972) na *MsimuwaVipepeo* (2006). Mtafiti huyu anaeleza changamoto zinazowakumba wanawake katika ndoa. Baadhi ya changamoto hizi ni uzinzi wa wanaume, ulevi, kutowajibika kwa wengi wa wanaume na umaskini. Mikakati inayopendekezwa ya kukabiliana na changamoto za wanawake walio katika ndoa ni mawasiliano na ushauri nasasha. Utafiti wa mtaalamu huyu unabainisha changamoto za ndoa, mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi suala linaloshughulikiwa na utafiti huu.

Gicuku (2012) amefanya utafiti kuhusu usawiri wa ndoa katika ushairi wa Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Gicuku amerejelea utanzu wa ushairi kutafiti kuhusu usawiri wa ndoa. Amerejelea diwani zifuatazo: *Kichomi* (1974) ya Euphrase Kezilahabi na *Bara jingine* (2007) ya Kithaka wa Mberia. Utafiti huu unashughulikia usawiri wa maudhui ya ndoa, athari za jamii katika usawiri wa maudhui ya ndoa, changamoto za ndoa na namna ya kukabiliana nazo. Changamoto za ndoa anazobainisha ni ukosefu wa mawasiliano bora, kutoaminiana, umaskini na uasherati. Mikakati ya kukabiliana na changamoto za ndoa inayojitokeza kupitia utafiti huu ni: Msamaha, mawasiliano ya dhati, kuheshimiana, kuwajibika, urafiki wa dhati na kujaliana kimaslahi. Katika utafiti huu anajadili athari kwa watoto wa wanandoa kama vile kutorokea mjini ndoa inapovunjika na kunajisiwa.

Karinge ( 2013) amechunguza usawiri wa maudhui ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Amechunguza changamoto za ndoa na pia mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi. Changamoto zinazojadiliwa ni ukatili na dhuluma, ukosefu wa mawasiliano bora, watoto, kukosa uaminifu katika ndoa, hila na udanganyifu, mila na desturi zilizopitwa na wakati, utandawazi, mahusiano ya kijamii na ukosefu wa hisia. Njia za kukabiliana na changamoto za ndoa anazojadili ni ushauri nasaha,uvumilivu,uelewano na ushirikiano, kuacha mila zilizopitwa na wakati, uwazi wa mawasiliano, matibabu yanayofaa, hisia katika ndoa, msamaha, thamani ya ndoa, uaminifu na uhusiano wa kijamii.

Nyamete (2016) amechunguza vichocheo vya migogoro ya kindoa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Anachunguza mambo ambayo yanasababisha migogoro katika ndoa. Mambo anayojadili kutokana na utafiti wake ni wivu uliokithiri na mashaka,

kutoridhika na tendo la ndoa, matarajio mengi ya wanandoa wanapoolewa, kukosekana kwa uaminifu katika ndoa kwa kushiriki uasherati au kusema uongo, ubinafsi na kiburi, kukosa kupata watoto au kupata wenye ulemavu na mawasiliano finyu. Vichocheo vingine vya migogoro ni kutowajibika, kushikilia mila na desturi zilizopitwa na wakati, mwanandoa mmoja kumdhibiti mwenzake, tofauti za asili ya wanandoa, wanandoa kutokuwa tayari kuungama makosa, kujirekebisha na kusameheana, dharau na tamaa iliyokithiri. Vichocheo Zaidi ni kutovumilia katika maisha ya ndoa, migogoro binafsi, hila na udanganyifu, ukatili na dhuluma na hatimaye ulevi.

Utafiti huu ulilenga kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa kupitia uhusika na usimulizi. Ubunilizi ni neno ambalo tafsiri yake ya Kiingereza ni neno *Fictionality*. Kulingana na Glare (2000) neno *Fictionality* asili yake ni neno la Kilatini *Fingere* lenye maana ya kujenga/kuumba/kuunda. Utafiti huu ulizingatia wahusika kuchunguza namna wanatumika kujenga changamoto za ndoa. Wataalamu mbalimbali wa fasihi wametoa maelezo na hata kufanya utafiti kuhusu kipengele hiki cha kibunilizi.Wamitila (2008b) anasema kuwa wahusika huchangia ujenzi wa maudhui kupitia kwa matendo yao. Wahusika ndio hushiriki katika matukio ya kazi ya kifasihi na kwa kufanya hivi wao hudhihirisha maudhui ya kazi husika. Utafiti huu ulizingatia uhusika kuchunguza namna unachangia ujenzi wa changamoto za ndoa. Wamitila (2003b) anaeleza kuwa uhusika ni mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Kenan (1983) anafafanua mbinu mbalimbali za kuwasawiri wahusika. Mbinu hizi ni: Usawiri bainishi, uhusika wa kimatendo, uhusika wa kiusemi, uhusika wa kimazingira, uhusika wa kianalojia na uhusika wa muonekano wa nje. Utafiti huu ulichunguza namna usawiri wa wahusika kupitia mbinu hizi unajenga changamoto za ndoa na kudhihirisha athari zake.

Ilomo (2015) anajadili mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao akirejelea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Anasema kuwa wahusika ni kipengele muhimu katika kuunda kazi ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani kutoa maudhui yoyote ya kifasihi. Anafafanua njia za kusawiri wahusika kama vile mbinu ya kimatendo,mbinu ya matamshi, mbinu ya uzungumzi nafsiya, mbinu ya kimazingira, mbinu ya mazungumzo baina ya wahusika na mbinu ya uwasilishaji dhahiri. Mbinu ya matendo huhusisha matumizi ya tendo

linalotendwa na mhusika, tendo ambalo mhusika anafaa kulitenda lakini halitendi na tendo ambalo halijatendwa lakini mhusika anadhamiria kulitenda. Mbinu ya matamshi hutumiwa kuwasawiri wahusika kwa kuwaacha wazungumze. Mbinu ya mazingira hutumiwa kwa kuwaweka wahusika katika mazingira ambayo yatasawiri sifa zao. Mazingira haya yanaweza kuwa makaazi yake, jamaa au watu wanaomzunguka. Mbinu ya uzungumzi nafsiya hutumiwa pale ambapo mhusika huchorwa akijizungumzia. Mbinu ya uwasilishaji dhahiri hutumika kwa kutajwa kwa uwazi sifa za mhusika.

Kipengele kingine ambacho kimezingatiwa katika kuchunguza ubunilizi wa changamoto za ndoa ni usimulizi.Wamitila (2003 b) anasema kuwa usimulizi hutumiwa kutoa ufafanuzi kuhusu mandhari, wahusika, matukio na migogoro katika kazi ya kifasihi. Kipengele hiki huchangia uelewekaji mzuri wa kazi ya kifasihi na hadhira na hivyo kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Usimulizi huhusisha matumizi ya vipengele kama vile mtazamo, aina za wasimulizi na nafsi za usimulizi. Utafiti huu umechunguza namna vipengele hivi jinsi vinavyofafanuliwa na Genette (1980) na Wamitila (2003 b) vimetumiwa kuwasilisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Nafsi za usimulizi na mitazamo imewahi kutumika hapo awali katika tafiti za kifasihi.Nakhumicha (2013) amechunguza namna sauti za usimulizi na mitazamo imetumika kusimulia maudhui ya mizozo kati ya marika katika riwaya za Kiswahili. Katika utafiti huu anafafanua namna mizozo mbalimbali kati ya marika imesimuliwa na sauti mbalimbali za usimulizi na aina za mitazamo.

Tafiti za Katola (2006), Nyaosi (2008), Nyamete (2016), Karinge ( 2013) na Gicuku (2012) zinaonyesha kuwa tafiti za awali kuhusu ndoa zimeegemea uchunguzi wa usawiri wa maudhui ya ndoa. Suala la namna changamoto zinazokumba asasi hii zimejengwa kupitia vipengele vya kibunilizi katika kazi za kifasihi ambazo ni tofauti na zimeandikwa na waandishi tofauti halijashughulikiwa. Hivyo basi, kuna haja ya kuchunguza jinsi changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi katika riwaya za Kiswahili ambazo ni tofauti na zimeandikwa na waandishi tofauti. Kwa msingi huu, utafiti huu umehakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Riwaya hizi ni: *Kiu* (1972),*Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008). Wataalamu hawa wote, Katola (2006), Nyaosi (2008), Nyamete (2016), Karinge ( 2013) na

Gicuku (2012) wamechunguza changamoto za ndoa katika kazi mahususi walizorejelea. Utafiti huu umechunguza jinsi changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika katika riwaya teule za Kiswahili. Hizi riwaya ni tofauti na zimeandikwa na waandishi tofauti. Gicuku (2012) amejadili athari za changamoto za ndoa kwa mfano watoto kutoroka nyumbani na kuenda kuishi katika mazingira hatari. Utafiti huu umechunguza jinsi athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao kwa kurejelea riwaya teule za Kiswahili ambazo ni tofauti na zimeendikwa na waandishi tofauti. Nyaosi (2008), Karinge (2013) naGicuku (2012) wamechunguza njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Utafiti huu umechunguza jinsi njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi kwa kurejelea riwaya teule za Kiswahili ambazo ni tofauti na zimeendikwa na waandishi tofauti.

### 1.3 Swala la Utafiti

Ndoa ni asasi muhimu inayoiendeleza jamii na kudumisha uthabiti wake kupitia majukumu yake muhimu ya kuhakikisha wanajamii wapya wanazaliwa na kulelewa. Tafiti za kifasihi na za kisosholojia kuhusu ndoa zinaonyesha kuwa inaendelea kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Tafiti za awali kuhusu ndoa katika fasihi ya Kiswahili zimebainisha changamoto zinazoiyumbisha na kutatiza utendakazi wake. Tafiti hizi zimechunguza changamoto za ndoa kama vile uasherati, ulevi, kutowajibika na umaskini na pia njia za kukabiliana nazokama vile mawasiliano ya dhati, kuheshimiana na kuwajibika. Athari za changamoto za ndoa kama vile kunajisiwa kwa watoto na ukosefu wa makao bora pia zimebainishwa. Hata hivyo, tafiti hizi za awali zimeegemea uchunguzi wa usawiri wa maudhui ya ndoa katika kazi mahususi za kifasihi. Kuna haja ya kuchunguza namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia vipengele vya kibunilizi kwa kurejelea kazi tofauti za kifasihi na ambazo zimeandikwa na waandishi tofauti. Kwa msingi huu, utafiti huu unahakiki namna uhusika na usimulizi umetumika kujenga changamoto za ndoa katika riwaya tofauti za Kiswahili na zilizoandikwa na waandishi tofauti. Unachunguza namna changamoto za ndoa na athari zake zimejengwa kupitia uhusika na pia namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi katika riwaya mbalimbali za Kiswahili zilizoteuliwa.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na maswali yafuatayo:

( i )Ni vipi changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika?

(ii)Je, athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwaje na usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili?

(iii)Je, njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimewasilishwa kupitia mbinu zipi za usimulizi?

### 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Azma ya utafiti huu ni kuhakikiuhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Madhumuni ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:

(i) Kueleza jinsi changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika.

(ii)Kutathmini namna athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili.

(iii)Kufafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimewasilishwa kupitia mbinu za usimulizi.

### 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unahakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Unahakiki jinsi uhusika na usimulizi umetumiwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili kusawiri changamoto za ndoa. Changamoto ambazo zinatatiza majukumu ya ndoakatika riwaya teule za Kiswahili ya kuzaa na kulea watoto ndizo zilizolengwa.Riwaya teule zinazorejelewa ni:*Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008). Riwaya hizi zimeteuliwa kwa sababu zote zimesheni data toshelezi kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Utafiti huu ulizingatia uhusika na usimulizi kuchunguza namna ambavyo vipengele hivi vya kibunilizi vimetumika kusawiri changamoto za ndoa kwa namna ya kipekee na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili. Mbinu za kusawiri wahusika ambazo zilizingatiwa ni uhusika wa kimatendo, uhusika wa kiusemi, uhusika wa muonekano wa nje na uhusika wa

kimazingira. Mbinu za usimulizi ambazo zilizingatiwa ni nafsi za usimulizi, aina za wasimulizi na aina za mitazamo. Ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia ya umuundo- uamilifu na nadharia ya naratolojia. Mihimili ya nadharia ya umuundo-uamilifu ilitumika kushughulikia sehemu ya mada kuhusu changamoto za ndoa nayo mihimili ya nadharia ya naratolojia ilitumika kushughulikia sehemu ya mada kuhusu uhusika na usimulizi.

**1.7 Misingi ya Uteuzi**

Ndoa ni asasi ambayo inatekeleza majukumu muhimu ya kuzaa na kulea kizazi kipya ambacho hutegemewa kuiendeleza jamii. Uhakiki wa maandishi unaonyesha kwamba asasi hii inaendelea kukosa uthabiti kutokana na mizozo mingi inayoikumba na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa kuzingatia dhima ya fasihi ya kushughulikia matatizo ya kijamii utafiti huu unashughulikia changamoto zinazoifanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Utafiti huu unahakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa kupitia uhusika na usimulizi kwa msingi kwamba kuelewa namna masuala ya kijamii yanavyojengwa katika kazi za kifasihi kupitia vipengele vya kibunilizi kunaimarisha ufasiri wake na kudhihirisha usanii katika kuyasawiri. Utafiti huu hivyo basi unachangia juhudi za fasihi ya Kiswahili kushughulikia matatizo yanayokumba jamii kama vile changamoto za ndoa kwa kuhakiki suala hili.

Utafiti huu unaziba pengo la kiutafiti kuhusu ndoa katika fasihi ya Kiswahili. Tafiti za awali kuhusua asasi hii zimetilia mkazo usawiri wa maudhui ya ndoa. Zimeshughulikia changamoto zinazoikumba, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Suala la namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi kwa kurejelea kazi tofauti za kifasihi na zilizoandikwa na waandishi tofauti halijashughulikiwa. Ili kuziba pengo hili la kiutafiti utafiti huu unahakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Unachunguza jinsi uhusika na usimulizi umetumika kujenga changamoto za ndoa kwa kurejelea riwaya za Kiswahili ambazo ni tofauti na zimeandikwa na waandishi tofauti. Unahakiki namna usawiri wa wahusika umetumika kusawiri changamoto za ndoa na kudhihirisha athari zake hasi. Aidha unahakiki matumizi ya mbinu za usimulizi kuwasilisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa.

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali. Unaonyesha namna ambavyo maudhui ya aina moja yanasawiriwa kwa matumizi ya uhusika na usimulizi na waandishi tofauti wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu unatarajiwa kuchangia zaidi utafiti kuhusu ndoa katika fasihi ya Kiswahili kwa kuhakiki ubunilizi wa changamoto zinazoikabili. Unaweza kupanua uelewa wa watakaousoma kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo kupitia mwelekeo wa kuhakiki ubunilizi wake. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kufaidi wasomi wa fasihi kuhusu uhakiki wa ubunilizi wa masuala ya kijamii katika kazi za kifasihi. Hatimaye utafiti huu unaonyesha mwelekeo tofauti wa kuzingatia ubunilizi katika kuhakiki masuala ya kijamii katika fasihi mbali na mwelekeo uliozoeleka wa kuzingatia maudhui.

### 1.8 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili  ambazo ni nadharia ya umuundo- uamilifu na nadharia ya naratolojia. Utafiti huu ulihitaji matumizi ya nadharia mbili kwa sababu ya lengo lake la kuhakiki uhusika na usimulizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Ili kutimiza lengo hili kulihitaji nadharia yenye mihimili kuhusu uhusika na usimulizi na nyingine yenye mihimili kuhusu ndoa na changamoto zake.  Nadharia ya umuundo- uamilifu iliteuliwa kwa sababu ya mhimili wake unaoeleza kuhusu jamii kuundwa kwa michakato na asasi zinazoihudumia kama vile ndoa na haja ya asasi hizi kuwa thabiti ili kuihudumia barabara. Mhimili mwingine wa nadharia hii uliofaa ni unaoeleza kwamba asasi za kijamii zinaweza kuwa na athari hasi au chanya. Nadharia ya naratolojia iliteuliwa kwa sababu ya mihimili yake kuhusu mbinu za kusawiri za wahusika, mbinu za usimulizi na haja ya kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa hadithi. Mhimili wa umuundo- uamilifu unaoleza kwamba asasi za kijamii huwa na athari ulitumika ulitumika pamoja na mhimili wa naratolojia unaoeleza kuhusu mbinu za kusawiri wahusika. Mihimili hii miwili ilitumika kuchunguza jinsi athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na wahusika kuitia usawiri wao. Mhimili wa umuundo- uamilifu unaoeleza kuhusu jamii kuundwa kwa michakato na asasi zinazoihudumia na haja ya asasi hizi kuwa thabiti ili kuihudumia barabara ulitumika pamoja na mhimili wa naratolojia unaoelezambinu za usimulizi na haja ya kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa hadithi. Mihimili hii mitatu ilitumika kuchunguza namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.

### 1.8.1 Nadharia ya Umuundo-uamilifu

Utafiti huu umetumia nadharia ya umuundo- uamilifu kulingana na mtazamo wa Merton (1957). Merton (1957) alipiga msasa uchanganuzi wa kiuamilifu. Kwa maoni yake michakato na asasi za kijamii zinaweza kuwa na manufaa, hasara au zisiwe na athari zozote kwa asasi nyingine au jamii. Alipinga maoni kuwa asasi za kijamii wakati wote hufaidi jamii. Anasisitiza kuwa lazima kipengele au vipengele vinavoathiriwa na kipengele fulani vibainishwe. Vipengele hivi vinaweza kuwa watu binafsi, kikundi au jamii nzima. Kwa mfano umaskini unaweza kuwa na athari mbaya kwa maskini lakini ukawa na faida kwa matajiri. Hii ni kinyume na uchanganuzi wa hapo awali ambao ulizingatia jamii kwa ujumla peke yake katika uchanganuzi. Anasisitiza kuwa asasi za kijamii lazima zichanganuliwe kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, kwa watu binafsi, kwa asasi na michakato ya kijamii na makundi katika jamii. Athari hizi zinaweza kuwa chanya au hasi.

Nadharia ya umuundo-uamilifu iliasisiwa na mwanasosholojia Emile Durkheim katika karne ya kumi na tisa na kuendelezwa na wanasosholojia wengine kama vile Talcott (1951) na Merton (1957). Kulingana na Sharrock, Hughes na Martin (2003) nadharia hii ina asili yake katika taaluma ya Sosholojia. Iliibuka mara ya kwanza karne ya kumi na tisa huko Ulaya. Baadaye ilistawishwa na wanasosholojia mbalimbali katika karne ya ishirini na kuwa nadharia maarufu katika Sosholojia.

Haralambos na wenzake (2004) na Appelrouth na Edles (2007) wanaeleza mawazo ya wanasosholojia Emile Durkheim, Talcot Parsons na Robert Marton ambayo yalisaidia kujenga na kustawisha nadharia hii. Kulingana mwasisi wa nadharia hii jamii ni mfumo ambao umeumbwa kwa vipengele kadha. Vipengele hivi ni asasi na michakato ya kijamii. Baadhi ya asasi za kijamii ni dini, ndoa na serikali. Mifano ya michakato ya kijamii ni mila, thamani, kaida , imani, uhalifu, kujinyonga,umaskini, salamu na ugonjwa. Kila moja ya vipengele vinavyounda mfumo wa kijamii hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha jamii nzima. Kwa mfano imani, thamani na sheria hudhibiti matendo ya wanajamii ikiwa watazizingatia. Ukiukaji wa vipengele hivi husababisha ukosefu wa uthabiti katika jamii na asasi zake.

Talcott (1951) anaeleza msingi wa utaratibu wa kijamii. Utaratibu wa kijamii hutokana na wanajamii kukubali kuzingatia kaida, thamani na dhima walizokubaliana kuzihusu. Vipengele hivi ndivyo hubainisha matendo ya haki na ya kweli miongoni mwa wanajamii. Kila asasi ya kijamii kwa mfano ndoa ina kaida ambazo huiongoza. Kwa mfano kwa mujibu wa Durkheim (1962) kaida ya kijamii ya kutaka wanandoa kujiepusha na uasherati huongoza ndoa. Mume anatarajiwa kuwa kiongozi wa familia na kuikimu kwa mahitaji yake. Mke anatarajiwa kuwa mnyenyekevu, mpole na mtunzi wa familia na nyumba yake. Ukiukaji wa kaida hizi ndio husababisha ukosefu wa uthabiti katika asasi hizi. Mtaalamu huyu anaunga mkono maoni ya Durkheim (1962) kuhusu umuhimu wa asasi za kijamii katika kuidumisha jamii nzima. Anafanya hivi kwa kueleza majukumu ambayo yanatekelezwa na baadhi ya asasi za kijamii. Anatoa maelezo kuhusu jinsi asasi ya uchumi, sheria, elimu na dini huhudumia jamii. Uchumi hutimiza hitaji la chakula nayo asasi ya kisiasa huweka malengo yanayoelekeza shughuli za jamii. Asasi ya sheria hutimiza hitaji la mshikamano ambalo huhusisha kudhibiti mahusiano kati ya asasi za kijamii na hatimaye asasi ya elimu na dini hutimiza hitaji la kudumisha ruwaza ya thamani kwa kufundisha amali za jamii ambazo kila mwanajamii anafaa kuzingatia. Ndoa ina jukumu la kuanzisha na kulea kizazi kipya ambacho kinaiendeleza jamii.

Talcott (1951) anasema kuwa hakuna mfumo wa jamii ambao ni thabiti kikamilifu. Mifumo hii huwa katika hali ya kuelekea kwenye uthabiti. Kulingana naye athari katika baadhi ya vipengele vinavyounda mfumo wa kijamii husababisha mabadiliko katika vipengele vingine ili kudumisha uthabiti. Kuhusu mabadiliko ya kijamii anasema kuwa yanasababishwa na mabadiliko katika thamani za jamii.

Merton (1957) alipiga msasa uchanganuzi wa kiuamilifu. Kwa maoni yake michakato na asasi za kijamii zinaweza kuwa na manufaa, hasara au zisiwe na athari zozote kwa asasi nyingine au jamii. Alipinga maoni kuwa asasi za kijamii wakati wote hufaidi jamii. Anasisitiza kuwa lazima kipengele au vipengele vinavoathiriwa na kipengele fulani vibainishwe. Vipengele hivi vinaweza kuwa watu binafsi, kikundi au jamii nzima. Kwa mfano umaskini unaweza kuwa na athari mbaya kwa maskini lakini ukawa na faida kwa matajiri. Hii ni kinyume na uchanganuzi wa hapo awali ambao ulizingatia jamii kwa ujumla peke yake katika uchanganuzi. Anasisitiza kuwa asasi za kijamii lazima zichanganuliwe kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, kwa watu binafsi,

kwa asasi na michakato ya kijamii na makundi katika jamii. Athari hizi zinaweza kuwa chanya au hasi. Utafiti huu ulitumia mawazo haya kuchunguza namna wahusika katika riwaya teule za Kiswahili wanadhihirisha athari hasi za changamoto za ndoa. Nadharia ya umuundo- uamilifu mbali na kufaa katika kuongoza utafiti huu imewahi kutumika hapo awali kufanya tafiti kuhusu kazi za kifasihi.

Gitau (2011) ametumia nadharia hii kufanya utafiti kuhusu maudhui ya unyanyasaji dhidi ya wanaume kama unavyodhihirika katika kazi teule za fasihi andishi ya Kiswahili. Anasema ametumia nadharia hii kwa sababu inatilia mkazo umuhimu wa kila kipengele cha kijamii katika kuihudumia na kuifanya iwe thabiti. Wanaume ni mojawapo wa vipengele vya kijamii na wanastahili kutafitiwa ili kubainisha changamoto zao na kuzishughulikia. Kwa kutumia nadharia hii amechunguza aina mbalimbali za unyanyasaji unaowakabili wanaume na misingi yake katika jamii, athari za dhuluma dhidi ya wanaume na hatimaye anahakiki kazi za waandishi wa kiume na wa kike na katika kuwalinganisha na kutofautisha yao kuhusu suala la unyanyasaji dhidi ya wanaume. Anarejelea riwaya ya Z. Burhani, *Mali ya Maskini* (1981) na ya Ken Walibora, *Siku Njema* (1996).

Gicuku (2012) ameitumia nadharia hii ya umuundo- uamilifu katika utafiti aliofanya kuhusu usawiri wa ndoa katika mashairi yaliyotungwa na Euphrase Kezilahabi na yale yaliyotungwa na Kithaka wa Mberia. Akitetea ufaafu wa nadharia hii kwa utafiti wake anasema kuwa jamii ni mfumo unaochangiwa na vipengele vyake vyote ili kuleta muumano na utangamano. Ndoa ni mojawapo ya vipengele hivi. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu nadharia hii husisitiza umuhimu wa kila kipengele kinachounda mfumo wa jamii kama vile ndoa kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kudumisha uthabiti wa kijamii. Ameitumia nadharia hii kuchunguza athari za kijamii katika usawiri wa maudhui ya ndoa katika fasihi andishi ya Kiswahili, namna mtunzi Kezilahabi alivyosawiri changamoto za ndoa pamoja na hatua zinazofaa kuchukuliwa kukabiliana nazo na mwisho namna usawiri wa changamoto za ndoa unavyojitokeza katika mashairi ya Kithaka wa Mberia na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kwa mujibu wa mawazo ya Durkheim(1962), Talcott(1951), Merton(1957), Haralambos, Martin na Robin (2004) na Appelrouth na Edles (2007) nadharia hii ina mihimili ambayo ilifaa utafiti huu. Mihimili ya nadharia hii iliyoongoza utafiti huu ni:

(i) Jamii ni mfumo wa asasi na michakato ya kijamii ambayo hutekekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na ni muhimu kwa asasi na michakato hii kuwa thabiti ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

( ii ) Jamii, asasi na michakato ya kijamii inaweza kuwa na athari hasi au chanya kwa jamii, asasi au michakato mingine. Michakato na asasi za kijamii zinafaa kuchanganuliwa kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, watu binafsi, makundi ya kijamii, asasi au michakato mingine ya kijamii

Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza, utafiti huu ulichunguza ndoa ambayo ni mojawapo ya asasi zinazounda mfumo wa jamii. Mhimili huu unatilia mkazo haja ya asasi za kijamii kutekeleza majukumu yake vizuri ili kutimiza mahitaji ya jamii kwa ujumla. Mhimili huu ulitumika kubainisha changamoto ambazo zinaifanya ndoa katika riwaya teule za Kiswahili kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhimili wa pili ulitumika kubainisha athari za changamoto za ndoa kwa wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au watoto wanaolelewa na wanandoa kwa kurejelea riwaya teule za Kiswahili.

### 1.8.2 Nadharia ya Naratolojia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratolojia kwa kuzingatia mtazamo wa Genette (1980) na Kenan(1983). Nadharia hii iliasisiwa na Prop mwaka 1968 na kuimarika zaidi mwaka 1969. Istilahi naratolojia imetoholewa kutoka neno la kiingereza *Narratology*. Neno hili kulingana na Monika(2009) linatokana na neno la Kifaransa *Narratologie* linalomaanisha uchunguzi wa hadithi. Tafsiri hii kutoka Kifaransa hadi Kiingereza ilifanywa na Taradov mwaka 1969. Prop (1968) aliweka msingi katika uchanganuzi wa hadithi kwa kuchunguza hurafa za kirusi. Katika uchunguzi wake alitambua matukio fulani yaliyozihusisha hurafa hizi. Aliorodhesha matukio na viamili katika mfuatano maalumu wa kiusababishi. Alibainisha viamili 31 katika hurafa alizochunguza.

Genette (1980) anatoa ufafanuzi kuhusu kipengele cha usimulizi na mtazamo. Anasema usimulizi ni muhimu katika kusawiri wahusika, kueleza matendo ya wahusika na matukio mbalimbali na kufafanua mandhari ambamo matukio hutendeka. Kipengele hiki huchangia uwasilishaji wa hadithi kwa hadhira. Nadharia hii hutoa maelezo kuhusu aina mbalimbali za usimulizi na dhima ya kila aina. Mtazamo unahusu masuala kama umbali uliopo kati ya msimulizi na matukio, msomaji na matukio, mhusika mmoja na mwingine. Kuna aina mbili za mitazamo. Kuna mtazamo wa ndani na mtazamo wa nje. Mtazamo wa ndani unajitokeza katika hadithi zinazosimuliwa katika nafsi ya kwanza. Msimulizi anaweza kuwa mshiriki katika matukio au awe anayashuhudia. Kwenye mtazamo huu msomaji huwa karibu na huweza kujitambulisha na mtazamo wake kuhusu matukio katika hadithi. Mtazamo wa ndani hufaa kusimulia matukio ya kiajabu. Ni rahisi kwa msomaji kujitambulisha na kumwamini msimulizi wa nafsi ya kwanza. Mtazamo wa nje hujitokeza kwa usimulizi wa nafsi ya tatu. Msimulizi huwa nje ya ulimwengu wa hadithi. Mtazamo huu hutumika pale ambapo mwandishi hutaka kueleza mambo ambayo hayawekani kwa mtazamo wa ndani.

Genette (1980) pia ametoa maelezo kuhusu aina za usimulizi na aina za wasimulizi. Anasema usimulizi sawia hubainishwa na matendo yanayosimuliwa jinsi yanavyotokea, mfano ni usilimulizi wa matukio katika filamu. Matukio husimuliwa wakati yanapotokea na wala si baadaye au kabla. Usimulizi tangulizi ni ule ambao unatangulia matukio au matendo yanayosimuliwa. Hutumia wakati uliopita. Usimulizi wa kirejeshi ni ule ambao hutumia nafsi ya kwanza na hutegemea wakati uliopita. Msimulizi hutumia aina hii ya usimulizi kuelezea maisha yake ya nyuma. Kwenye usimulizi wa kiutomaji mafungu fulani ya hadithi husimuliwa kati ya tendo fulani. Usimulizi wa ki-itimamu ni ule ambapo pana vifungu vya hadithi ambavyo vinatokezea katikati ya tendo fulani. Usimulizi wa aina hii unaweza kupatikana pale ambapo pana matumizi ya barua hasa katika riwaya za aina hiyo. Usimulizi wa nafsi ya kwanza ni ule unaofanywa na mhusika wa nafsi ya kwanza. Mhusika huyu anaweza kuwa mshiriki au asiwe mshiriki katika hadithi anayosimulia. Hutambuliwa kwa matumizi ya "mimi" katika umoja na "sisi" katika wingi. Usimulizi huu hujenga uhusiano wa karibu kati ya hadithi na msomaji. Usimulizi wa nafsi ya pili hupatikana katika hadithi inayosimuliwa katika nafsi ya pili. Hutambuliwa kwa matumizi ya kiwakilishi nafsi "wewe". Usimulizi wa nafsi ya tatu hutambuliwa kwa matumizi ya "yeye". Msimulizi wa nafsi ya tatu hueleza mambo yanayomhusu

mtu mwingine. Mtaalamu huyu anatoa ufafanuzi kuhusu aina mbalimbali za wasimulizi. Anasema msimulizi tawasifu ni mhusika katika hadithi na husimulia matukio ya hadithi ambayo yeye anashiriki na kuathiriwa nayo. Msimulizi wasifu ni msimulizi ambaye husimulia matukio ya hadithi ambayo yeye hashiriki. Msimulizi horomo ni yule ambaye hutoa habari tu na kuwaacha wahusika wazungumze wao wenyewe kwa wenyewe bila kuwaingilia kati au kutoa ushauri na maamuzi fulani ya kimsingi. Utafiti huu ulizingatia aina za usimulizi, aina za mitazamo na aina za wasimulizi kwa mujibu wa maoni ya mtaalamu huyukufafanua namna vipengele hivi vya naratolojia vimetumika kuwasilisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili.

Nadharia hii ya naratolojia hufafanua mbinu za kusawiri wahusika katika kazi za kifasihi. Kenan ( 1983) anafafanua aina mbili kuu za usawiri wahusika katika kazi za kifasihi. Aina ya kwanza ni usawiri bainishi ambapo mwandishi hutoa maelezo kuhusu sifa za mhusika kwa njia ya moja kwa moja akitumia vivumishi vya sifa. Aina ya pili ni usawiri timbe ambapo sifa za wahusika hazielezwi moja kwa moja bali msomaji huachwa kuzitathmini kupitia usemi, matendo, mazingira, muonekano au majina ya wahusika. Chini ya usawiri timbe mtaalamu huyu anaeleza mbinu kadha za kuwasawiri wahusika. Mbinu hizi ni matendo, usemi, muonekano wa nje, mazingira na analojia. Matendo yanaweza kuwa yanayotendwa na mhusika, yale mhusika anakwepa kuyatenda au matendo ambayo mhusika ananuia kuyatenda. Matendo hufafanuliwa ikiwa ni ya kurudia au ya kufanyika mara moja tu. Mbinu ya usemi hurejelea fikira au mazungumzo ya mhusika ambao unaweza kuwa mazungumzo. Kinachozingatiwa chini ya mazungumzo ni namna mhusika anavyoongea na mazungumzo ya mhusika kujihusu au kuwahusu wahusika wengine. Kuhusu namna anavyoongea mhusika kinachozingatiwa ni hisia zinazoibuliwa na kuongea kwake kama vile hasira, huzuni au furaha. Kuongea kwa mhusika kunaweza kudhihirisha unyenyekevu, madharau au unyonge. Namna mhusika anateua maneno na aina za maneno anayotumia huzingatiwa katika usawiri wa aina hii. Kwa mfano mhusika akiwa anatumia maneno ya heshima kila mara anapoongea anaweza kuelezwa kuwa mwenye heshima. Wahusika wanaweza kusawiriwa kupitia maneno wanayosema kujihusu au kuwasawiri wahusika wengine kupitia maneno wanayosema kuwahusu. Mbinu ya muonekano wa nje wa mhusika ambao kuhusisha maumbile ya mhusika au mavazi yake. Usawiri kwa kuzingatia maumbile unaweza kuangazia urefu au ufupi, unene au wembamba, rangi ya ngozi au nywele.

Usawiri kwa kuzingatia mavazi unaweza kuangazia ughali au uduni na ikiwa mavazi yanahusiana na kazi, dini au taaluma fulani. Mbinu ya mazingira huzingatia makaazi ya mhusika na hata jamaa zake au watu anaoishi nao au wanaomzunguka. Kwa mfano mhusika anaweza kuelezwa kuwa anaishi katika nyumba chafu ili kuonyesha kutowajibika kwake.

Mbinu ya analojia imegawanywa kwa vitengo viwili yaani majazi na ulinganuzi wa wahusika. Majazi hujitokeza pale ambapo mwandishi humpatia mhusika jina ambalo linaashiria sifa zake. Mbinu ya mwisho ni ulinganuzi wa wahusika. Wahusika wawili au zaidi wanaweza kuwekwa katika muktadha sawa na kuachwa tofauti kati ya wasifu wao ijibainishe kupitia matendo yao katika muktadha huo. Hata hivyo mtaalamu huyu anasema kuwa mbinu ya analojia si mbinu kuu ya kuwasawiri wahusika bali hutumiwa kushadidia mbinu nne zilizofafanuliwa. Utafiti huu ulizingatia mbinu za kusawiri wahusika kwa matendo, usemi, muonekano wa nje na mazingira kwa mujibu wa maoni ya mtaalamu huyu kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa. Ulihakiki namna changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimejengwa na wahusika kupitia usawiri wao kwa kutumia mbinu hizi.

Mbali na Genette(1980) na Kenan(1983) kuna wataalamu wengine ambao wametoa maelezo kuhusu nadharia ya naratolojia. Wamitila (2003 b) anasema kuwa nadharia hii huchunguza hadithi au usimulizi kwa kurejelea mawazo ya umuundo. Anasema kuwa nadharia hii huchunguza hali, muundo na uamilifu wa simulizi au hadithi na kubaini umilisi alio nao mwandishi wa hadithi. Umilisi wa msanii wa hadithi humtofautisha na wasanii wengine na kuumba umakinifu na mvuto wa sanaa yake. Katika muktadha wa utafiti huu umilisi wa msanii unadhihirishwa na usawiri wa wahusika na matumizi ya mbinu za usimulizi kusawiri changamoto za ndoa. Naratolojia huchunguza mambo kama vile sifa za undani za muundo wa hadithi, usimulizi wake na mtazamo unaotokeza. Kulingana na Wamitila (2003 a) uchunguzi wa kinaratolojia huhusisha vipengele kama vile kinachosimuliwa, matukio yanayosimuliwa na usimuliaji wenyewe pamoja na njia zilizotumiwa na ufanisi wake. Uchunguzi wa usimulizi pia hushughulikia mtiririko wa usimulizi wenyewe. Sauti ya usimulizi na ubunifu wa usimulizi husika pia huchunguzwa. Masuala zaidi yanayochunguzwa ni kufungamana kwa usimulizi na masuala yanayozungumzwa na hatimaye namna mitindo ya usimulizi inaathiri uelewaji wa masuala yanayosimuliwa. Utafiti huu ulichunguza namna suala la njia za kukabiliana na

changamoto za ndoa limefungamana na usimulizi. Umefafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.

Wamitila (2003b) anatoa maelezo zaidi kuhusu dhana ya mtazamo ambayo imeelezwa na Genette (1980). Anasema mtazamo ni dhana inayoelezea aliko msimulizi anapoyaangalia matukio katika hadithi. Msimulizi anaweza kuyatazama matukio akiwa ndani ya ulimwengu wa hadithi au mshiriki katika hadithi anayosimulia. Kwa upande mwingine anaweza kuwa nje ya ulimwengu wa hadithi anayosimulia au akose kuwa mshiriki katika matukio ya hadithi anayosimulia. Ikiwa anasimulia matukio anayoshiriki basi mtazamo unaojitokeza ni mtazamo wa ndani. Ikiwa anasimulia matukio akiwa nje ya hadithi anayosimulia basi mtazamo unaojitokeza utakuwa ni mtazamo wa nje. Anasema mtazamo unahusu nafasi inayochukuliwa ya kuyatazama matukio pamoja na mikabala anayochukua mwandishi ambayo inaweza kuwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, ya tatu au utinde (kutoweza kuyaona au kuyajua yote) au maizi. Kipengele cha mtazamo huchunguza aliko msimulizi anapoyaangalia matukio ya hadithi. Suala hapa huwa ni ikiwa msimulizi anasimulia hadithi akiwa ndani ya hadithi husika kama mshirika au yuko nje ya hadithi hiyo. Msimulizi anaweza kusimulia matukio ya hadithi ambayo anashiriki yeye au akasimulia matukio ambayo wahusika wengine wanashiriki. Mtaalamu huyu anaeleza sawia mbalimbali za mtazamo

Sawia za uchunguzi wa mtazamo ni sawia ya mawanda- wakati, sawia ya kiisimu na lugha, sawia, sawia ya kisaikolojia na sawia ya kitathmini au ki-itikadi. Sawia ya mawanda-wakati hutufahamisha mahali anaposimama na wakati ambapo msimulizi anasimlia matukio. Mawanda humaanisha uhusiano kati ya vitu au visimuliwa na msemaji pamoja na mahali alipo mwenyewe. Vielezi vya mahali kama hapo, hapa na pale huonyesha msimulizi yuko mbali na matukio anayosimulia. Vielezi kama vile hilo na huyu huonyesha msimulizi yuko karibu na matukio. Wakati huonyeshwa kwa kutumia viashiria kama leo, keshoye na juzi.

Chini ya sawia ya kilugha au kiisimu lakakabu au ufupisho wa majina huweza kutumiwa kuonyesha mtazamo. Lakabu huweza kutumiwa kuonyesha ukaribu na uzoefu kati ya wahusika. Kuhusu lugha maneno ya mhusika yanaweza kunukuliwa katika maelezo ya msimulizi na kufanywa kuwa sehemu ya lugha ya msimulizi. Sawia ya kitathmini hutokea pale ambapo

msimulizi hutathmini matukio fulani na labda kuonyesha mwelekeo au mwelemeo wake ki-itikadi. Chini ya sawia hii msimulizi hutoa maoni au msimamo wake kuhusu suala fulani ili kuwashawishi wasomaji wakubaliane na mtazamo wake. Anaweza kumhukumu mhusika, asasi au tukio. Sawia ya kisaikolojia humulika uelewa alio nao mhusika fulani katika kazi fulani ya kifasihi. Msimulizi hufanya hivi kwa kuyasimulia mawazo yanayompitikia akilini. Msimulizi au mwandishi anaweza kutumia mtindo wa usemi usiokuwa wa moja kwa moja kuonyesha mtazamo huu. Utafiti huu ulieleza mtazamo unaojitokeza katika usimulizi wa matukio yanayoashiria njia za kukabiliana na changamoto za ndoa.

Ann na Samuel (2007) wanaeleza vipengele ambavyo hujenga hadithi. Vipengele hivi ni msuko, wahusika, mandhari, mtazamo, mtindo na maudhui. Wahusika ni kipengele muhimu cha hadithi kwa kuwa matukio katika hadithi huhusishwa nao. Wahusika hujenga maudhui aliyokusudia msanii kwa kushiriki katika matukio ya hadithi (Chatman, 1978). Uchanganuzi wa kinaratolojia huchunguza wahusika na mbinu ambazo zimetumika kuwasawiri na pia namna wanachangia katika usimulizi wa hadithi na kushiriki matukio yake. Utafiti huu ulizingatia kipengele cha wahusika na mbinu za kuwasawiri kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa.

Monika (2009) anatoa maelezo kuhusu aina kuu tatu za usimulizi; usimulizi unaotokea baada ya matukio kutendeka, usimulizi wa matukio kabla hayajatendeka na hatimaye usimulizi wa matukio wakati ambapo yanatendeka. Mwandishi huyu anabaini masuala makuu katika usmulizi. Masuala haya ni wakati, wakala au ajenti wa usimulizi, mkabala wa kimtazamo na usemi au diskosi. Kipengele cha wakati katika usimulizi hugawanywa katika wakati hadithi na wakati matini. Wakati hadithi hurejelea wakati ambao matukio ya hadithi huchukua kuanzia mwanzo hadi mwisho, wakati matini ni wakati ambao matini fulani huchukua kusomwa na hutegemea kasi ya msomaji binafsi. Kipengele hiki cha wakati kina vigezo kadha, vigezo hivi ni mpangilio na muda. Chini ya mpangilio matukio ya hadithi huweza kusimuliwa katika mfuatano wa kiwakati, kwa kurejelea matukio ya hapo awali au kwa kusimulia matukio yajayo. Suala la muda hushughulikia kipindi ambacho tukio limechukua. Muda hujitokeza kwa jinsi tano ambazo ni muhtasari, udondosi, onyesho, uendelezaji na mtuo.

Jinsi ya kwanza ni muhtasari ambapo wakati wa matini huwa mfupi kuliko wa hadithi. Katika hali hii muda mrefu wa matukio ya hadithi hufupishwa kwa kutolewa maelezo machache tu. Jinsi ya pili ni udondoshi ambapo maelezo katika matini fulani huachwa. Hapa wakati matini huwa nunge. Jinsi ya tatu ni onyesho ambapo wahusika katika hadithi huigiza. Wao huigiza kupitia kwa mazungumzo na vitendo. Hapa wakati hadithi huwa sawa na wakati matini. Jinsi ya nne ni uendelezaji. Hapa wakati wa matini huwa mrefu kuliko wakati wa matukio. Maelezo marefu huweza kutolewa kuhusu mandhari au fikira za mhusika fulani na yasiweze kusukuma mbele matukio ya hadithi. Mwisho ni kigezo cha mtuo. Kuhusu kigezo hiki wakati wa hadithi huwa ni nunge yaani hakuna kundelea kwa matukio.

Wamitila (2003a) anatoa maelezo kuhusu kipengele cha idadi marudio au umara ambacho huzingatiwa katika uchambuzi wa hadithi. Umara hurejelea idadi ya kutokea kwa matukio na idadi ya kusimuliwa kwake. Dhana hii hutoa maana ya urudiaji wa aina fulani. Uchanganuzi wa kinaratolojia unabaini aina tatu za urudiaji wa tukio. Kuna hali ambapo tukio lililotukia mara moja husimuliwa mara moja tu. Kuna hali ambapo tukio lililotokea mara moja linasimuliwa mara kadha au linarudiwa. Aina ya tatu ni pale ambapo tukio lililotokea mara kadha linasimuliwa mara moja tu.

Msuko ni kipengele kingine ambacho hushughulikiwa chini ya uchanganuzi wa kinaratolojia. Wamitila (2003b) anasema msuko ni mpangilio wa matukio ya hadithi jinsi yanavyofuatana kwa njia ya kiusababishi. Msuko huhusisha matendo ya nguli athari za matendo haya kwa wahusika wengine. Anafafanua aina mbalimbali za misuko ambayo huweza kupatikana katika kazi za kifasihi. Aina hizi ni: Msuko mkuu, msuko msago, msuko linganuzi, msuko kioo, msuko rudufu na msuko kinzani. Dhana ya msuko mkuu hujitokeza katika kazi ya kifasihi ambayo ina hadithi kuu na vihadithi vingine. Msuko mkuu ni msuko wa hadithi kuu. Msuko msago ni ule ambapo matukio hufuatana kwa njia ya moja kwa moja bila kuwepo matumizi ya mbinu rejeshi.

Msuko linganuzi ni msuko ambao matokeo yake yanalengwa kuwa kinyume cha msuko mkuu. Msuko huu huashiriwa na matendo na malengo ya mhusika mkinzani katika kazi ya kifasihi. Msuko kioo ni ule ambapo matukio hayafuatani moja kwa moja. Huhusisha matumizi ya mbinu rejeshi ambapo matukio ya awali hurejelewa. Msuko kinzani ni ule unaodhamiria kuafikia lengo

linalopingana au kinyume na la msuko mkuu. Msuko huu hujitokeza kupitia kwa matendo na malengo ya mhusika anayepingana na nguli. Hatimaye kuna msuko rudufu. Huu ni msuko zaidi ya moja ambao hupatikana katika kazi za kifasihi zilizo na hadithi mbili zinazoweza kutambuliwa wazi.

Kipengele kingine kinachochunguzwa na nadharia ya naratolojia ni msomaji. Wamitila (2003 b) na Monika (2009) wanatoa maelezo kuhusu maana ya na aina za wasomaji. Msomaji ni mtu anayefasiri au kusimbua hadithi iliyoandikwa. Kuna msomaji andikwa, msomaji mlengwa na msomaji mwashiriwa. Msomaji andikwa ni yule anayelengwa kuisoma kazi husika. Msomaji huyu anaweza kutambuliwa kutokana na sifa za kazi husika. Sifa hizi ni pamoja na maudhui, lugha, lugha na uchangamano au usahili wake. Msomaji mlengwa ni yule ambaye mwandishi hudhamiria aisome kazi yake. Msomaji huyu huwa katika mawazo ya mwandishi anapoanza kuitunga na kuiandika kazi yake. Msomaji mwashiriwa ni yule anayeakisiwa na kazi ya kifasihi. Kuna uwezekano akawa msomaji ambaye ana ufahamu fulani wa kazi za kifasihi au kazi inayohusika.

Kinara (2012) amefanya utafiti kuhusu madhara ya ukimwi. Anarejelea riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Nadharia ya naratolojia na ya matendo ya usemi zimetumika katika utafiti huu. Amechunguza jinsi riwaya hizi zimesawiri suala la ukimwi, usemi unaotumiwa kusawiri ukimwi, athari za ukimwi kwa wahusika katika riwaya hizi na nafasi ya masimulizi haya na namna ya kukabiliana na suala zima la ukimwi pamoja na changamoto zake.

Nakhumicha ( 2013) amechunguza namna sauti za usimulizi na mitazamo imetumika kusimulia maudhui ya mizozo kati ya marika katika riwaya za Kiswahili. Katika utafiti huu anafafanua namna mizozo mbalimbali kati ya marika imesimuliwa na sauti mbalimbali za usimulizi na aina za mitazamo. Matumizi ya naratolojia katika tafiti hizi yanaonyesha ufaafu wa nadharia hii katika kuhakiki masuala ya kijamii katika kazi za kifasihi japo wataalamu hawa walishughulikia masuala tofauti na utafiti huu.

Ifuatayo ni mihimili ya nadharia hii iliyofaa utafiti huu kwa kuzingatia mtazamo waGenette (1980) na Kenan (1983)

(i) Uchunguzi wa hadithi unaweza kufanywa kwa kutumia vipengele vya kinaratolojia kama vile matumizi ya lugha, mandhari, mbinu za usimulizi kama vile aina za usimulizi, aina za wasimulizi, aina za mitazamo, wakati, daraja za usimulizi, msuko na aina ya wasomaji na pia wahusika na mbinu za kuwasawiri kama vile usawiri bainishi, uhusika wa kimatendo, uhusika wa kiusemi, uhusika wa kimazingira, uhusika wa muonekano wan a uhusika wa analojia.

(ii) Uchambuzi wa usimulizi katika hadithi unafaa kufanywa kwa kuzingatia namna unahusiana na masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi husika. Masuala haya ni maudhui au yaliyomo.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unabainisha wahusika kama kipengele kinachotumika kuchunguza hadithi. Aidha unafafanua njia za kuwasawiri wahusika. Mhimili huu ulitumika kuchunguza namna changamoto za ndoa na athari zake katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri. Mhimili wa pili wa nadharia hii unaeleza kuhusu haja ya kuhusisha uchambuzi wa usimulizi wa hadithi na masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi husika. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza namna suala la njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili limewasilishwa na mbinu za usimulizi.

Mihimili ya nadharia hizi mbili yaani umuundo- uamilifu na naratolojia iliongoza ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data ili kuafikia madhumuni ya utafiti huu. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuwa jamii ni mfumo wa asasi na michakato ya kijamii ambayo hutekekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na ni muhimu kwa asasi na michakato hii kuwa thabiti ili itekeleze majukumu yake ipasavyo. Mhimili huu ulitumika kubainisha changamoto ambazo zinaifanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unabainisha wahusika kama kipengele cha kuchunguzia hadithi na kutoa maelezo kuhusu mbinu za kusawiri wahusika. Mhimili huu umetumika pamoja na mhimili wa kwanza wa nadharia ya muundo- uamilifu

uliotumika kubainisha changamoto za ndoa kueleza namna changamoto zilizobainishwa zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri.

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kwamba jamii, asasi na michakato ya kijamii inaweza kuwa na athari hasi au chanya kwa jamii, asasi au michakato mingine. Michakato na asasi za kijamii zinafaa kuchanganuliwa kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, watu binafsi, makundi ya kijamii, asasi au michakato mingine ya kijamii. Mhimili huu ulitumika kubainisha athari za changamoto za ndoa kwa wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au wanaolelewa nao. Mhimili huu ulitumika pamoja na mhimili wa kwanza naratolojia unaobainisha wahusika kama kipengele cha kuchunguzia hadithi na kueleza mbinu za kusawiri wahusika. Mhimili huu wa naratolojia umetumika kuchunguza namna athari ambazo zimebainishwa na mhimili wa kwanza uliotajwa wa nadharia ya umuundo- uamilifu zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza umuhimu wa asasi na michakato ya kijamii kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhimili huu ulitumika kubainisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Mhimili wa kwanza wa naratolojia unaelea kuhusu mbinu za usimulizi. Mhimili wa pili wa nadharia ya naratolojia unaeleza kwamba chambuzi wa usimulizi katika hadithi unafaa kufanywa kwa kuzingatia namna unahusiana na masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi husika. Masuala haya ni maudhui au yaliyomo. Mihimili hii mitatu imetumika kuchunguza namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa ambazo zimebainishwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.

**1.9 Hitimisho**

Katika sura hii maelezo yametolewa kuhusu usuli wa utafiti. Ufafanuzi umetolewa kuhusu mada ya utafiti na utafiti wa awali kuihusu. Baada ya usuli swala la utafiti limebainishwa. Maswali ya utafiti ambayo yataelekeza ukusanyaji data yameorodheshwa. Maswali haya yanafuatiwa na lengo na madhumuni mahususi ya utafiti huu. Lengo na madhumuni mahususi yanaweka wazi mambo ambayo utafiti huu ulidhamiria kuafikia. Upeo wa utafiti unabainisha mambo ambayo yalishughulikiwa katika utafiti huu. Mambo haya ni kama vile riwaya zitakazorejelewa na nadharia zitakazotumika. Baada ya upeo kuna maelezo kuhusu misingi ya uteuzi.

Chini ya misingi ya uteuzi maelezo yametolewa kuhusu sababu ya kuchagua mada na manufaa ya matokeo ya utafiti huu. Sehemu ya mwisho inahusu nadharia zilizoongoza utafiti huu. Maelezo

ya kina yametolewa kuhusu nadharia ya umuundo- uamilifu na nadharia ya Naratolojia. Ufaafu wa nadharia hizi kwa utafiti huu umejadiliwa.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii ina uhakiki wa maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Kuna tahakiki kuhusu changamoto za ndoa, athari za changamoto hizi na njia za kukabiliana nazo. Kuna uhakiki kuhusu maandishi yanayoshughulikia vipengele vya usimulizi vilivyozingatiwa katika utafiti huu ambavyo ni wahusika na usimulizi.

## 2.2 Usawiri wa Changamoto za Ndoa

Kwa mujibu wa nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoongoza utafiti huu, ndoa ni asasi ya kijamii ambayo hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha jamii. Vidya na Sachdeva ( 2007) wanaeleza kuwa ndoa ni asasi ambayo huleta mume na mke pamoja ili kuanzisha familia. Asasi hii hutoa mazingira bora ya kuzaa na kulea kizazi kipya ambacho huendeleza jamii. Kupitia ndoa kizazi hiki hupewa mahitaji mbalimbali na kufundishwa amali za jamii. Majukumu haya yanaweza kutekelezwa barabara ikiwa asasi hii itakuwa imara. Hata hivyo tafiti kuhusu ndoa zinaonyesha kwamba inakumbwa na changamoto ambazo zinaifanya isiwe imara na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Charles (2008) anatoa maelezo ya kisosholojia kuhusu changamoto za ndoa. Anasema asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi kwa mfano ulevi, uasherati, wivu, matatizo ya kifedha, mapigano na mgongano wa maslahi ya wanandoa. Macious (2002), Giddens (2006), Sachdeva na Vidya (2007) na Schaefer (2008) wanatoa maelezo zaidi kuhusu chhangamoto za ndoa. Wanasema kuwa ndoa inakumbwa na changamoto kama vile umaskini, kutotoshelezwa kwa tendo la ndoa, mauaji, ukosefu wa mawasiliano, uhasama, ugumba, utasa, ugomvi na ukosefu wa mapenzi. Maelezo haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa yanatoa ufahamu zaidi kuhusu suala la changamoto za ndoa. Hata hivyo maelezo haya yanatofautiana na utafiti uliofanywa kwa kuwa hayarejelei ndoa katika kazi za kubuni. Kazi za kubuni huwasilisha ujumbe kisanaa na kibunilizi na wala si kwa njia ya kiuhalisia. Utafiti huu ulihakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa. Ulidhamiria kuonyesha namna ambayo changamoto za ndoa zimejengwa na waandishi wa riwaya teule kupitia uhusika na usimulizi.

Gichinga (2005) anasema kuwa changamoto za ndoa zinachukua nafasi ya pili miongoni mwa matatizo yanayowafanya watu kuendea ushauri nasaha nchini Kenya. Anaema kuwa ndoa nchini zinakabiliwa na changamoto kama vile kuthuriwa kimwili na kiakili, magonjwa, uasherati, unywaji pombe na matumizi ya vileo kupindukia, matatizo ya kifedha, kukosa kupata watoto, kutatizwa na jamaa za wanandoa na pia kutoridhika na tendo la ndoa. Maelezo haya yanahusu changamoto za ndoa ambalo ni suala linaloshughulikiwa na utafiti huu. Hata hivyo maelezo haya hayahusu namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi kwa kurejelea riwaya ya Kiswahili.

Odhiambo (2013) amechunguza mizozo ya ndoa nchini Kenya na vyanzo vyake. Amegundua kuwa kuna ongezeko la mizozo katika ndoa nchini. Mizozo hii inasababishwa na mapato madogo, kutokubaliana kuhusu majukumu kati ya wanandoa, kunywa pombe kupindukia, uchezaji kamari, utesaji wa watoto ambao hawajazaliwa na wanandoa wote na pia wa jamaa za wanandoa na mwingilio kutoka jamaa za wanandoa. Anasema kuwa wanandoa hudhulumiana kwa njia mbalimbali kama vile kupigwa makofi, kupigwa mateke, kugongwa, mwanandoa kumfungia mwenzake nje ya nyumba yao, kutowasiliana na kususia kutekeleza majukumu kama vile kupika, kuosha nguo na kukataa kushiriki tendo la ndoa. Anaeleza kuwa mizozo zaidi ya kindoa husababishwa na mwanandoa mmoja kumpinga mwenzake anapotaka kuwaadhibu watoto, uasherati, mapato madogo, mmoja kuchunguza mienendo ya mwenzake kisiri na mume kukosa kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya kuikimu familia naye mke kukosa kutekeleza ipasavyo majukumu ya nyumbani kama vile kazi za nyumba na kulea watoto. Mtaalamu huyu anasema wanandoa huendelea kuishi katika ndoa zenye dhuluma kwa sababu ya kuogopa mwenzake kukosa kuwakimu watoto akiondoka nao, kuogopa watoto kuteswa na mwanandoa mpya, kuogopa kuvunjika tena kwa ndoa iwapo ataamua kuolewa tena, kuogopa kukiuka kiapo cha ndoa, mke kumtegemea mume, kumiliki mali kwa pamoja na pingamizi kutoka kwa jamaa za wanandoa. Anasema kuwa waume hutumia utamaduni na dini kuthibitisha haja yao ya kuwataka wake wao kunyenyekea na kuwatii wakati wote. Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na huu kwa kuwa unashughulikia suala la changamoto za ndoa. Unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa si wa kifasihi. Hauchunguzi jinsi changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi katika riwaya riwaya teule za Kiswahili.

Masua (2016) anasema kwamba kuna ongezeko la ukosefu wa uthabiti katika ndoa kote duniani. Anamefanya utafiti kuhusu ukosefu wa uthabiti wa ndoa miongoni mwa wanawake katika sehemu za mashambani na athari zake. Ametumia kaunti ya Machakos nchini Kenya kama eneo la utafiti wake. Anajadili sababu ambazo zinafanya ndoa kukosa uthabiti na kuwafanya wake kuwataliki au kutengana na waume wao. Sababu hizi ni unywaji pombe na utumiaji wa vileo vingine kupindukia, kulazimishwa kushiriki na kupigwa wanapokataa, kutowajibika kwa waume, uasherati, ghasia, ukosefu wa ajira kwa mume, tofauti za kiumri, ukewenza, kuthuriwa kimwili, utasa, kukosa kupata mtoto wa jinsia inayopendelewa, mume kuoa mke mwingine, kuingiliwa na jamaa za mume na uchawi au mapepo.Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na utafiti uliofanywa kwa kuwa umeshughulikia suala la changamoto za ndoa. Unatofautiana huu unatofautiana na wa mtaalamu huyu kwa kuwa umechunguza namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi na waandishi mbalimbali wa riwaya ya Kiswahili.

Ubunilizi ni neno ambalo tafsiri yake ya Kiingereza ni neno *Fictionality*. Kulingana na Glare (2000) neno *Fictionality* asili yake ni neno la Kilatini *Fingere* lenye maana ya kujenga/ kuumba/ kuunda. Utafiti huu hivyo basi unahakiki namna uhusika na usimulizi umetumika na waandishi wa riwaya teule kujenga changamoto za ndoa.

Wamitila (2002) anatoa maelezo kuhusu ndoa kwa kuegemea jinsia ya kike. Anasema ndoa ni asasi ya kitamaduni ambayo imejengwa kwa mila na desturi zinazompendelea mume na kumkandamiza mke. Mke anabaki kuwa chini ya mamlaka ya mumewe na kulazimika kufuata maamuzi yake yote. Mke anakuwa kama chombo kinachomilikiwa na mumewe, hashauriwi wala kushirikishwa katika maamuzi muhimu ya ndoa. Maelezo haya yalifaidi utafiti uliofanywa kwa sababu yanatoa ufafanuzi zaidi  kuhusu changamoto zinazokumba asasi ya ndoa. Yanaonyesha namna mwanamke anakandamizwa katika ndoa, hapewi nafasi sawa na mumewe. Japo maelezo haya yanahusu changamoto za ndoa sawa na utafiti huu, hayachunguzi uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa. Hayaelezi namna changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi.

Katola (2006) amechunguza udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia ya Kiswahili. Anasema kuwa ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazomdhulumu mwanamke. Anaeleza changamoto zinazowakumba wanawake katika ndoa kwa mfano kunyimwa haki ya kumiliki mali, kutoa maoni kuhusu maswala muhimu katika ndoa, kuwa chini ya mamlaka na amri za mumewe, kuchukuliwa kuwa ni mali ya mumewe na kukosa haki ya kuelezea kutoridhika kwake. Utafiti huu mtaalamu huyu unashughulikia changamoto za ndoa sawa na utafiti huu ingawa umeangazia changamoto zinazowakumba wake. Hata hivyo utafiti huu haukuchunguza namna ambavyo changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi. Utafiti huu unaziba pengo hili kwa kuchunguza jinsi ambavyo changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimejengwa kupitia uhusika na usimulizi.

Nyaosi (2008) ametafiti kuhusu taswira ya ndoa katika riwaya mbili za Kiswahili, *Kiu* (1972) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Mtafiti huyu anaeleza changamoto zinazowakumba wanawake katika ndoa. Baadhi ya changamoto hizi ni uzinzi wa wanaume, ulevi, kutowajibika kwa wengi wa wanaume na umaskini. Utafiti huu japo unaegemea changamoto zinazowakumba wake unafanana na wa mtaalamu huyu kwa kuwa unashughulikia suala la changamoto za ndoa. Utafiti wa mtaalamu huyu unatofautiana na huu kwa kuwa haukuchunguza uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa. Utafiti huu kwa kurejelea riwaya teule za Kiswahili unachunguza jinsi ambavyo changamoto za ndoa zimejengwa kupitia uhusika.

Karinge (2013) amechunguza usawiri wa maudhui ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Amechunguza changangamoto za ndoa na njia za kukabiliana nazo. Changamoto zinazojadiliwa ni ukatili na dhuluma, ukosefu wa mawasiliano bora, watoto, kukosa uaminifu katika ndoa, hila na udanganyifu, mila na desturi zilizopitwa na wakati, utandawazi, mahusiano ya kijamii na ukosefu wa hisia.Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na huu kwa kuwa unashughulikia suala la changamoto za ndoa. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na wa mtaalamu huyu kwa kuwa ulichunguza uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa ili kuonyesha jinsi vipengele hivi vya kibunilizi vimetumika kujenga changamoto za ndoa.

Gicuku (2012) amefanya utafiti kuhusu usawiri wa ndoa katika ushairi wa Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. Utafiti huu unashughulikia usawiri wa maudhui ya ndoa, athari za jamii katika usawiri wa maudhui ya ndoa, changamoto za ndoa na namna ya kukabiliana nazo. Changamoto za ndoa anazobainisha ni ukosefu wa mawasiliano bora, kutoaminiana, umaskini na uasherati. Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na huu kwa sababu unashughulikia suala la changamoto za ndoa. Utafiti huu unatofautiana na wa mtaalamu huyu kwa sababu ulichunguza namna ambavyo changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa kupitia uhusika na usimulizi. Ulichunguza namna changamoto za ndoa katika riwaya teule zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri.

Nyamete (2016) amechunguza vichocheo vya migogoro ya kindoa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012). Anachunguza mambo ambayo yanasababisha migogoro katika ndoa. Mambo anayojadili kutokana na utafiti wake ni wivu uliokithiri na mashaka, kutoridhika na tendo la ndoa, matarajio mengi ya wanandoa wanapoolewa, kukosekana kwa uaminifu katika ndoa kwa kushiriki uasherati au kusema uongo, ubinafsi na kiburi, kukosa kupata watoto au kupata wenye ulemavu na mawasiliano finyu. Vichocheo vingine vya migogoro ni kutowajibika, kushikilia mila na desturi zilizopitwa na wakati, mwanandoa mmoja kumdhibiti mwenzake, tofauti za asili ya wanandoa, wanandoa kutokuwa tayari kuungama makosa, kujirekebisha na kusameheana, dharau na tamaa iliyokithiri. Vichocheo Zaidi ni kutovumilia katika maisha ya ndoa, migogoro binafsi, hila na udanganyifu, ukatili na dhuluma na hatimaye ulevi. Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na utafiti huu kwa kuwa ulishughulikia vichocheo au changamoto za ndoa. Utafiti huu ulichunguza uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa ili kuonyesha namna zimesawiriwa kupitia uhusika na usimulizi.

Utafiti huu ulizingatia kipengele cha kinaratolojia cha wahusika kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa. Hii inatokana na umuhimu wa kipengele hiki katika utunzi wa kazi za kifasihi. Kipengele hiki kimetolewa maelezo na wataalamu kuhusu maana yake, usawiri wake na umuhimu wake. Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa wahusika ni sehemu ya fani, na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili kuwasilisha kazi yake kwa hadhira. Mwandishi huwaumba wahusika kwa kuwapa majukumu, sifa, matendo na maneno ambayo yatamwezesha

kuwatumia kujenga maudhui anayodhamiria kuwasilisha. Chatman (1978) anaeleza umuhimu wa kuzingatia wahusika katika uchambuzi wa hadithi. Wahusika hutumiwa na mwandishi wa kazi ya kifasihi kwa kusimulia matukio kwa kuwa matukio hutendwa nao. Wao hushiriki matukio ya hadithi na kwa kufanya hivi hudhihirisha maudhui ya msanii. Utafiti huu ulizingatia umuhimu wa wahusika katika uwasilishaji wa maudhui kwa mujibu wa wataalamu hawa kukitumia kipengele hiki kuchunguza namna kimetumika kubuni changamoto za ndoa.

Kenan (1983) anafafanua aina mbili kuu za usawiri wahusika katika kazi za kifasihi. Aina ya kwanza ni usawiri bainishi ambapo mwandishi hutoa maelezo kuhusu sifa za mhusika kwa njia ya moja kwa moja akitumia vivumishi vya sifa. Aina ya pili ni usawiri timbe ambapo sifa za wahusika hazielezwi moja kwa moja bali msomaji huachwa kuzitathmini kupitia usemi, matendo, mazingira, muonekano au majina ya wahusika. Chini ya usawiri timbe mtaalamu huyu anaeleza mbinu kadha za kuwasawiri wahusika. Mbinu hizi ni matendo, usemi, muonekano wa nje, mazingira na analojia. Anatoa ufafanuzi kuhusu kila mbinu ya kusawiri wahusika. Maelezo kuhusu mbinu hiziyalifaidi utafiti huu kwa kutoa ufafanuzi kuhusu mbinu mbalimbali za kusawiri wahusika japo hayafafanui namna mbinu hizi za usawiri zimechangia ujenzi wa maudhui ya changamoto za ndoa. Utafiti huu ulichunguza namna changamoto za ndoa zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri.

Kuna tafiti ambazo zimechunguza namna kipengele hiki cha wahusika. Murungi (2013) anajadili namna mtindo unaendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala* (1997) ya Kithaka wa Mberia. Amechambua namna wahusika, matumizi ya lugha na mandhari yanachangia kujenga maudhui ya ukombozi wa mwanamke katika jamii. Anajadili namna uumbaji wa wahusika unachangia kujenga maudhui haya. Aidha anaeleza namna matumizi mbalimbali ya lugha yanavyojenga maudhui mbalimbali. Wahusika wamechunguzwa namna wametumiwa kujenga maudhui ya uasherati, urithi wa wanawake, umaskini na kudunishwa kwa wanawake. Utafiti huu haujalenga kuhakiki mahususi suala la changamoto za ndoa. Matokeo ya utafiti huu yalifaa utafiti uliofanywa kwa kuwa yanaonyesha namna wahusika wanachangia usawiri wa maudhui. Utafiti uliofanywa ulichunguza namna wahusika wametumika kusawiri maudhui ya changamoto za ndoa na kudhihirisha athari zake hasi katika riwaya teule za Kiswahili.

Ilomo (2015) anajadili mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao akirejelea riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Anasema kuwa wahusika ni kipengele muhimu katika kuunda kazi ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani kutoa maudhui yoyote ya kifasihi. Anafafanua njia za kusawiri wahusika kama vile mbinu ya kimatendo,mbinu ya matamshi, mbinu ya uzungumzi nafsiya, mbinu ya kimazingira, mbinu ya mazungumzo baina ya wahusika na mbinu ya uwasilishaji dhahiri. Mbinu ya matendo huhusisha matumizi ya tendo linalotendwa na mhusika, tendo ambalo mhusika anafaa kulitenda lakini halitendi na tendo ambalo halijatendwa lakini mhusika anadhamiria kulitenda. Mbinu ya matamshi hutumiwa kuwasawiri wahusika kwa kuwaacha wazungumze. Mbinu ya mazingira hutumiwa kwa kuwaweka wahusika katika mazingira ambayo yatasawiri sifa zao. Mazingira haya yanaweza kuwa makaazi yake, jamaa au watu wanaomzunguka. Mbinu ya uzungumzi nafsiya hutumiwa pale ambapo mhusika huchorwa akijizungumzia. Mbinu ya uwasilishaji dhahiri hutumika kwa kutajwa kwa uwazi sifa za mhusika. Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na huu kwa kuwa umeshughulikia mbinu za usawiri wa wahusika. Hata hivyo unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa hauhakiki namna usawir wahusika kupitia mbinu zilizojadiliwa umetumika kujenga changamoto za ndoa.

**2.3 Udhihirishaji wa Athari za Changamoto za Ndoa**

Selfe (1993) kwa kurejelea taaluma ya Sosholojia anatoa maelezo kuhusu athari hasi za talaka kwa jamii. Talaka huvuruga familia na kutatiza maisha ya wazazi na watoto wao. Wanaweza kukosa usalama, utambulisho, makao mazuri na huduma nyingine muhimu kama elimu bora kwa watoto. Kuvunjika kwa ndoa husababisha viwango vya juu vya mawazo, kuongezeka kwa matatizo ya kiafya, ulevi na kujiua.

Talaka hutatiza watoto na kuwafanya kuwa na matatizo ya kiakili na kitabia. Pia husababisha kuongezeka kwa familia za mzazi mmoja na kufanya ulezi wa watoto kukumbwa na shida nyingi. Talaka imewafanya watu kuwa na mwelekeo hasi kuhusu ndoa na kuwafanya kuamua kuishi bila kuoa au kuolewa ama kuishi katika ndoa mjarabu. Ndoa mjarabu ni ndoa ambazo hazijaidhinishwa kulingana na sheria, dini au utamaduni wa jamii. Charles (2008) anasema kuwa talaka huathiri jamii kwa ujumla. Husababisha umaskini ambao hulazimu jamii nzima kuingia gharama za kuushughulikia. Hii athari hutokea katika ndoa ambazo zilikuwa na pato la chini.

Jamii huingia gharama kama za kupunguzia waliotalakiana kodi za nyumba kwa kulipa sehemu ya kodi hiyo, kulipa mawakili wanaohusika na kesi za talaka na ukusanyaji wa pesa za kugharamia mahitaji ya wake na watoto baada ya talaka. Maelezo haya yalichangia utafiti huu kwa kuwa yanafafanua baadhi ya athari za changamoto za ndoa. Utafiti huu ulichukua mwelekeo wa kuchunguza namna athari za changamoto za ndoa zimesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya zilizoteuliwa.

Maelezo haya ya Charles (2008)  na Selfe ( 1993) yanatokana na taaluma ya Sosholojia  na yanarejelea ndoa katika ulimwengu halisi na wala si katika kazi za kubuni za fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo tafiti hizi zinatoa ufahamu zaidi kuhusu mada ya utafiti huu kwa sababu zinafafanua athari hasi za changamoto za ndoa kwa kurejelea taaluma ya Sosholojia na wala si kazi za fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo maandishi haya yanatoa ufahamu zaidi wa mada ya utafiti huu kwa sababu yanafafanua athari hasi za changamoto za ndoa. Utafiti uliofanywa unatofautiana na huu kwa sababu ulihakiki athari hasi za changamoto za ndoa kwa kurejelea kazi za kubuni za fasihi andishi ya Kiswahili na wala si ulimwengu halisi. Utafiti  huu unatathmini namna athari za changamoto za ndoa zinasawiriwa kibunilizi kupitia usawiri wa wahusika.

Masau (2016) anajadili athari za ukosefu wa uthabiti wa ndoa kwa wake na watoto baada ya ndoa talaka au utengano. Anasema wake na watoto hukabiliwa na umaskini kutokana na ukosefu wa pato la kutosha. Mzigo wa kulea watoto hubebwa na mzazi mmoja ambaye mara nyingi huwa ni mama. Masomo ya watoto hukatika kwa sababu ya mzazi anayebakia na watoto kushindwa kuyagharamia. Aidha watoto hawa hulazimika kuhamia katika makaazi mapya kwa mfano kwa nyanya au babu zao.

Gichinga (2005) anajadili athari za  changamoto za ndoa kwa wazazi na watoto. Anasema kuwa athari wa wazazi ni mawanandoa kutoroka kila mara na kurudi, waume kukaa kwa vyumba vya starehe muda mrefu ili kuepuka mzozo nyumbani  na wanandoa kuishi tu pamoja bila kuhusiana kama mke na mume. Athari kwa watoto ni kutelekezwa na wazazi na kuwa na tabia zisizofaa. Anasema  watoto hawa huanza kuwa kushiriki mambo ya utotoni ambayo walikuwa wameyaacha kama vile kwenda haja ndogo kwa malazi na kunyonya kidole gumba. Watoto ambao ni wakubwa huanza tabia hasi kama vile matumizi ya dawa za kulevya, utundu na

matatizo ya kisaikolojia. Maelezo ya mtaalamu huyu yanahusu suala la athari za changamoto za ndoa kwa watoto sawa na utafiti huu. Utafiti huu unatofautiana na maelezo yanayotolewa na mtaalamu huyu kwa sababu unachunguza namna athari za changamoto za ndoa zimedhihiriswa na wahusika kupitia uhusika wao. Utafiti huu ni wa kifasihi na tofauti na maelezo yanayotolewa na mtaalamu huyu.

Gicuku (2012) anaeleza namna ndoa imeshindwa kutekeleza majukumu yake ya ulezi kwa sababu ya changamoto zinazoikabili. Anaeleza jinsi umaskini huwafanya baadhi ya wanandoa kuwatuma watoto wao kwenye mahoteli kufanya uasherati ili kuwaletea pesa. Vile vile anaeleza namna watoto wa wanandoa hutoroka nyumbani kwa sababu ya changamoto za ndoa za wazazi wao na kwenda kuishi mitaani katika mazingira hatari. Baadhi ya watoto hunajisiwa na jamaa zao wa karibu, hata wazazi wao. Anaeleza namna wazazi wanazama katika shughuli za kutafuta pato na kukosa muda wa kuwaelekeza wanao kimaadili. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha jinsi ndoa huathiri watoto kwa kutatiza malezi yao kupitia kwa changamoto zake suala ambalo limeshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo utafiti huu unatathmini namna athari hizi zimejengwa kupitia usawiri wahusika ambao ni watoto wa wanandoa.

### 2.4 Uwasilishaji wa Njia za Kukabiliana na Changamoto za Ndoa

Tafiti za kifasihi kuhusu ndoa zinadhihirisha kwamba waandishi wa riwaya ya Kiswahili wamewasilisha njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto za ndoa katika kazi zao. Nyaosi (2008) anaeleza mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba wanawake katika ndoa. Alirejelea riwaya ya *Kiu* (1972) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Mikakati inayopendekezwa ni mawasiliano, ushauri nasaha na wanandoa kuheshimiana. Utafiti huu wa Nyaosi unahusiana na utafiti uliofanywa kwa sababu unafafanua njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto za ndoa ili kuifanya iwe imara na kutekeleze majukumu yake barabara. Hata hivyo aliegemea njia za kukabiliana na changamoto zinazowakumba wanawake walio katika ndoa na wala si wanandoa wote. Utafiti huu tofauti na wa Nyaosi (2008) ulichunguza namna njia hizi zimewasilishwa na mbinu za usimulizi yaani nafsi za usimulizi, aina za mitazamo na aina za wasimulizi.

Gicuku (2012) kupitia utafiti aliofanya kuhusu taswira ya ndoa katika mashairi ya kezilahabi na ya Kithaka wa Mberia mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto za ndoa inabainika. Utafiti huu ulirejelea diwani ya *Bara jingine* (2001a) na *Msimu wa Tisa* zilizoandikwa na Kithaka wa Mberia na diwani ya *Kichomi* (1974) iliyoandikwa na Kezilahabi. Mikakati ya kukabiliana na changamoto za ndoa ambayo inajitokeza kupitia diwani hizi ni; kila mwanandoa kuomba msamaha anapokosa, kuwepo kwa mawasiliano ya dhati kati ya wanandoa na kuwa na urafiki wa dhati kati ya wanandoa kabla na baada ya kuoana. Mikakati mingine ni kila mwanandoa ajali maslahi ya mwenzake na kila mwanandoa atosheke na mwanzake na walichonacho, kuheshimiana, kila mwanandoa kujitolea kudumisha ndoa yao na pia kuwajibikia majukumu yake. Mikakati inayopendekezwa ya kukabiliana na changamoto za wanawake walio katika ndoa ni mawasiliano na ushauri nasasha.

Utafiti wa Nyaosi ( 2008) na Gicuku ( 2012) unahusiana na kufaa utafiti huu kwa kuwa unatoa ufahamu zaidi kuhusu njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Watafiti hawa wamejadili njia za kukabiliana na changamoto za ndoa kama vile ushauri nasaha, kuheshimiana, mawasiliano mwafaka na kuomba msamaha. Utafiti huu ulichukua mwelekeo tofauti kwa kuchunguza namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.

Utafiti huu ulizingatia usimulizi kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa kwa sababu ya umuhimu wa kipengele hiki katika utunzi wa kazi za kifasihi. Wataalamu mbalimbali wameeleza maana ya kipengele hiki na umuhimu wake katika utunzi wa hadithi. Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi (Wamitila, 2003 b). Njogu na Chimera (1999) wanasema usimulizi ni sauti ya kuwasilisha hadithi. Ni njia ya kuwasilisha hadithi kwa hadhira au wasomaji katika riwaya au kazi ya kinathari. Akivaga na Odaga (1982) wanasema kuwa usimulizi ni muhimu kwa kuwa humwezesha msimuliaji kufanikiwa kuiwasilisha hadithi yake kwa hadhira. Usimulizi ni kipengele muhimu katika uwasilishaji wa maudhui kwa kuwa hutumiwa kueleza matukio ambayo huibua maudhui ya mtunzi. Maelezo ya wataalamu yanatoa ufafanuzi kuhusu kipengele cha usimulizi ambacho kimezingatiwa katika utafiti huu japo hayaelezi namna mbinu zake zinatumika kuwasilisha maudhui katika kazi za kifasihi. Utafiti huu ulichunguza namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Mbinu za usimulizi ambazo zilizingatiwa ni aina za usimulizi, aina za mitazamo na aina za wasimulizi.

Kuna watafiti ambao wamezingatia kipengele hiki cha usimulizi kuhakiki namna kimetumika kusawiri maudhui katika kazi za kifasihi walizorejelea. Nakhumicha (2013) amechunguza namna sauti za usimulizi na mitazamo imetumika kusimulia maudhui ya mizozo kati ya marika katika riwaya za Kiswahili. Katika utafiti huu anafafanua namna mizozo mbalimbali kati ya marika imesimuliwa na sauti mbalimbali za usimulizi na aina za mitazamo. Utafiti huu japo haushughulikii maudhui ya ndoa ulifaidi utafiti uliofanywa kwa kuwa unaonyesha namna mbinu za usimulizi zinatumika kusawiri maudhui katika kazi za kifasihi. Utafiti huu ulizingatia maelezo kuhusu aina za usimulizi, aina za wasimulizi na mitazamo kuchunguza namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa kupitia mbinu hizi.

Mohochi (2000) amechunguza usimulizi katika riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Mbinu za usimulizi zinazojitokeza katika riwaya hii na kufafanuliwa na mtaalamu huyu ni usimulizi maizi, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu na usimulizi wa nafsi ya pili. Utafiti wa mtaalamu huyu unafanana na huu kwa kuwa pia nao umezingatia kipengele cha usimulizi. Unafaidi huu kwa kutoa ufafanuzi kuhusu aina za usimulizi na matumizi yake katika kazi za kifasihi. Utafiti huu unatofautiana na wa mtaalamu huyu kwa kuwa unazingatia mbinu nyingine za usimulizi ambazo ni aina ya wasimulizi na aina za mitazamo. Utafiti huu unachunguza namna mbinu za usimulizi zimetumika kuwasilisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa, tofauti na utafiti wa mtaalamu huyu.

**2.5 Hitimisho**

Katika sehemu hii uhakiki umefanywa kuhusu usawiri wa changamoto za ndoa, usawiri wa athari zake na pia usawiri wa njia za kukabiliana na changamoto hizi. Uhakiki huu umebainisha kwamba suala la changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo limewahi kushughulikiwa na waandishi wa taaluma ya Sosholojia na fasihi. Imebainika kwamba suala la namna vipengele vya kibunilizi vimetumika katika ujenzi au ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya mbalimbali za Kiswahili halijatafitiwa. Hili ndilo pengo ambalo utafiti huu ulidhamiria kuziba kwa kuhakiki uhusika na usimulizi katika ubunilizi wa changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili. Uhakiki umefanywa kuhusu vipengele vya ubunilizi ambavyo vimezingatiwa katika kuchunguza ubunilizi wa changamoto za ndoa. Vipengele hivi ni uhusika na usimulizi. Maandishi kuhusu maana na umuhimu wa vipengele hivi yamehakikiwa. Uhakiki

umefanywa kuhusu tafiti ambazo zimefanywa kwa kuzingatia vipengele hivi. Tafiti hizi hazionyeshi namna vipengele hivi vimetumika kujenga changamoto za ndoa katika riwaya mbalimbali za Kiswahili. Hata hivyo zinatoa ufahamu kuhusu mbinu za usawiri wa wahusika na pia matumizi ya wahusika kusawiri masuala katika kazi za kifasihi. Isitoshe, zinatoa ufahamu kuhusu namna mbinu za usimulizi yaani aina za usimulizi na aina za mitazamo zimetumika kusawiri masuala ya kijamii kwa mfano tofauti za kirika.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kuhusu mbinu ambazo zilitumika kufanya utafiti. Maelezo yametolewa kuhusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti huu, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data na vifa vya kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data na hatimaye maadili ya utafiti. Mbinu hizi zimeelezwa namna ambavyo zilitumika kufanikisha utafiti huu.

### 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa uchanganuzi. Creswell (1998) anasema kuwa muundo wa uchanganuzi ni muundo ambao unatumia habari ambazo tayari zipo kufanya utafiti. Muundo huu huhusisha uchanganuzi wa habari hizi ili kuibuka na tathmini mwafaka kuzihusu. Muundo wa uchanganuzi hueleza na kufasiri data iliyoko tayari katika vitabu, stakabadhi au picha. Lengo la muundo huu ni kutoa uelewa wa kina wa habari zilizopo.

Muundo huu unafaa kwa sababu utafiti huu unadhamiria kukusanya data ambayo ipo tayari kwenye riwaya teule na kuichanganua ili kuafikia malengo yake. Utafiti huu uliendeshwa kwa kuzingatia muundo huu. Data ilikusanywa kutoka kwa riwaya teule za Kiswahili zilizosampulishwa kidhamirifu kwa kutumia mbinu ya unukuzi. Badaye zilihaririwa na kuchanganuliwa kimaudhui kwa kupangwa katika mada kuu na ndogondogo kwa kutegemea kuoana kwake kimaudhui. Hatimaye iliwasilishwa kimaelezo kama matokeo ya utafiti. Shughuli ya ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data iliongozwa na madhumuni na maswali ya utafiti huu. Pia iliongozwa na mihimili ya nadharia ya umuundo-uamilifu na ya naratolojia iliyoongoza utafiti huu.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huu ni maktabani, muktadha wa fasihi andishi na mahususi riwaya za Kiswahili. Riwaya zilizolengwa maktabani kwa ukusanyaji wa data ni riwaya teule za Kiswahili ambazo ni: *Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000) *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008).

Kilicholengwa kukusanywa kutoka kwa riwaya hizi ni data kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo na vipengele vya kibunilizi yaani wahusika na usimulizi. Fasihi andishi ya Kiswahili imegawanywa katika tanzu tano yaani riwaya, tamthilia, mashairi, hadithi fupi na novela. Riwaya ndio utanzu ambao ni mrefu, mpana na wenye uchangamano kimtindo na kidhamira na hushughulikia masuala kadha katika mtazamo mpana wa kiwakati (Wamitila, 2002). Utafiti huu ulizingatia riwaya kwa sababu ya kushughulikia masuala kwa mapana na kwa uchangamano wa kimtindo. Sifa hizi za riwaya ndizo ambazo zilizingatiwa kuamua kuitumia kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa. Utafiti maktabani ulihusisha kusoma maandishi kuhusu mada ya utafiti, nadharia na mbinu za utafiti.

### 3.4 Kundi Lengwa

Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kwamba kundi lengwa ni kundi la watu, vitu au matukio ambayo yana sifa zinazofanana na zinazofaa utafiti unaolengwa. Anasema kuwa sampuli huteuliwa kutoka kwa kundi hili. Kundi lengwa la utafiti huu ni riwaya za Kiswahili ambazo zimesawiri maudhui ya changamoto za ndoa, athari za changamoto hizi na njia za kukabiliana nazo. Uteuzi wa kundi lengwa ulioongozwa na mada ya utafiti huu, malengo na maswali yake ya utafiti. Utafiti huu haukuweza kubainisha idadi kamili ya kundi lengwa kwa sababu ni wa kithamano na haikuwa rahisi kupata kwa usahihi idadi ya riwaya za Kiswahili ambazo zimesawiri changamoto za ndoa, athari zake  na njia za kukabiliana nazo. Patton (1990) anasema kuwa katika utafiti wa kithamano na unaotumia usampulishaji dhamirifu kama huu suala la idadi ya sampuli, uwakilishi wa sampuli na kiini cha data halitiliwi maanani. Anasisitiza umuhimu wa kupata data mwafaka na ya kutosha kuwezesha kuafikiwa kwa lengo na madhumuni ya utafiti unaofanywa. Ni kutokana na kundi lengwa lenye sifa zilizobainishwa hapo juu ambapo sampuli dhamirifu ya riwaya tano za Kiswahili iliteuliwa. Riwaya hizi ni *Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008).

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ya utafiti huu ni sampuli dhamirifu ya riwaya tano za Kiswahili ambayo imetokana na usampulishaji dhamirifu. Riwaya hizi ni *Kiu* (1972), *Mwisho wa Kosa* (1987), *Maisha Kitendawili* (2000), *Ua la Faraja* (2005) na *Unaitwa Nani?* (2008). Wataalamu mbalimbali

wametoa maelezo kuhusu usampulishaji dhamirifu ambayo yalizingatiwa katika uteuzi wa sampuli ya utafiti huu. Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa usampulishaji dhamirifu humruhusu mtafiti kuchagua sampuli ambayo ina habari anazotaka kutegemea madhumuni ya utafiti wake. Patton (1990 ) anasema kwamba usampulishaji dhamirifu unaweza kufanywa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kina. Mbinu hii huhusisha uteuzi wa sampuli ambayo ni bora zaidi na inatoa data ya kutosha na mwafaka ya kuchunguza suala linalotafitiwa. Kwa kuzingatia maoni ya wataalamu hawa kuhusu usampulishaji dhamirifu, riwaya zilizotajwa ziliteuliwa kwa sababu zina data toshelezi kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Data hii inatosha kujibu maswali ya utafiti na kuwezesha kuafikiwa kwa madhumuni ya utafiti huu. Usampulishaji dhamirifu wa kina huhitaji mtafiti kuwa na habari za awali na kufanya uchunguzi ili kutambua vitafitiwa vyenye habari zaidi zinazohitajika (Patton, 1990). Mtafiti anafaa kufanya uchunguzi mapema kubainisha sampuli ambayo ni bora zaidi kwa mujibu wa utafiti wake. Usampulishaji ulianza na uchunguzi kufanywa kuhusu riwaya ambazo zimesawiri changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Uchunguzi ulihusisha kusoma maktabani tafiti za awali katika fasihi ya Kiswahili, uhakiki kuhusu riwaya za Kiswahili na kusoma maandishii nyuma ya majalada ya riwaya za Kiswahili. Uchunguzi huu ulibaini kuwa riwaya hizi zina data toshelezi ya kuchunguzia suala linalotafitiwa. Patton (2002) anasema kuwa hakuna sheria inayomfunga mtafiti kuchagua idadi fulani ya sampuli, yuko huru kuchagua idadi ambayo itampa data mwafaka na ya kutosha kutegemea lengo na madhumuni ya utafiti wake. Mtafiti anayetumia mbinu hii lazima atoe sababu ya kuchagua sampuli. Suala la uwakilishi wa sampuli halitiliwi maanani, muhimu ni kuwa sampuli iweze kutoa data mwafaka na ya kutosha kwa utafiti (Tromp na Kombo, 2006). Uchunguzi uliofanywa kabla ya uteuzi wa sampuli ulibaini kuwa riwaya hizi tano zina data toshelezi ya kuweza kutumiwa kushughulikia suala la utafiti kikamilifu. Hii ni kwa sababu riwaya hizi zote tano zimesheheni changamoto mbalimbali za ndoa. Kati ya Riwaya hizi, riwaya ya *Unaitwa Nani?* Imesheheni data toshelezi kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Riwaya ya *Ua la Faraja* imesheheni data toshelezi kuhusu athari za changamoto za ndoa. Riwaya hii pamoja na riwaya ya *Kiu*, *Mwisho wa Kosa* na *Maisha Kitendawili* zote zimesheheni data toshelezi kuhusu athari za changamoto za ndoa na njia za kukabiliana nazo.

### 3.6 Ukusanyaji Data na Vifaa vya Kukusanya Data

Data ilikusanywa kwa njia ya maktaba kwa kutumia mbinu ya unukuzi. Riwaya teule zilisomwa na nukuu ambazo zina habari za kuweza kutumiwa kujibu maswali ya utafiti kundikwa katika daftari. Nukuu za kwanza ni maneno au sentensi zinazoonyesha changamoto, wahusika na matendo, usemi, mazingira au muonekano wao wa nje unaoijenga changamoto husika. Nukuu za pili ni zile zinazonyesha athari za changamoto za ndoa, wahusika na matendo, usemi, mazingira au muonekano wao wa nje unaozidhihirisha. Nukuu za tatu ni zile ambazo zinaonyesha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa na usimulizi wake. Vifaa vilivyotumiwa kukusanya data ni daftari, kalamu na orodha ya uchunzaji(Tazama kiambataniso A, Uk. 157). Katika daftari mliandikwa nukuu kutoka kwa riwaya teule kwa kalamu. Orodha ya uchunzaji ilitumika kuelekeza kuhusu sifa mahusi za nukuu zenye data inayohitajika kwa utafiti huu.

### 3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi na uwasilishaji wa data uliongozwa na madhumuni na mihimili ya nadharia zilizoongoza utafiti huu. Data zilichanganuliwa kimaudhui. Tromp na Kombo (2006) wanasema kuwa katika uchanganuzi wa kimaudhui, maudhui au mada ambazo zitazingatiwa katika uchanganuzi hubainishwa. Baada ya kukusanywa data zilihaririwa na kuchanganuliwa kimaudhui kwa kupangwa katika makundi ya mada kuu na mada ndogo kutegemea kuoana kwake kimaudhui. Utafiti huu ulibainisha mada tatu kuu kutokana na madhumuni ya utafiti. Mada ya kwanza ni changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimesawiriwa kupitia uhusika. Chini ya mada hii kuna mada ndogo kadha za changamoto mbalimbali za ndoa. Chini ya mada hizi data kuhusu changamoto husika ziliwekwa. Mada ya pili ni udhihirishaji wa athari za changamoto za ndoa kupitia uhusika. Chini ya mada hii kuna mada kadha ndogo za athari mbalimbali za changamoto za ndoa. Chini ya kila athari, zinazohusiana nayo ziliwekwa. Mada ya tatu ni njia za kukabiliana na changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Mada hii imegawanywa kwa mada ndogo za njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Data kuhusu kila njia za kukabiliana na changamoto za ndoa na mbinu za usimulizizi lizotumika kuiwasilisha zimewekwa chini ya hizi mada. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia mada kuu na mada ndogo zilizobainishwa. Data chini ya kila mada ilielezwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti huu. Maelezo yametolewa kuhusu changamoto mbalimbali za

ndoa na athari zake zimejengwa kupitia uhusika. Maelezo mengine yametolewa kuhusu namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.

### 3.8 Maadili Katika Utafiti

Mugenda (2011) anafafanua maadili mbalimbali ambayo yanafaa kuzingatiwa wakati wa kufanya utafiti ili kulinda hadhi ya utafiti na kuafikia matokeo sahihi. Maadili anayofafanua ni kuheshimu haki miliki. Anasema kwamba sharti machapisho au waandishi ambao maoni yao, maneno yao, matokeo au kazi zao zimetumika watambuliwe. Kufanya hivi kunafanya utafiti uwe kazi asili ya mtafiti au mwandishi. Utafiti huu ulizingatia maadili haya kwa kutambua waandishi wa vitabu au machapisho ambayo yalirejelewa katika utafiti huu. Maoni ya wataalamu waliorejelewa yalitambuliwa kwa kuwataja. Maadili mengine ambayo mtaalamu huyu anafafanua ni kutovuruga data, mchakato wa utafiti na matokeo. Mtafiti hafai kutumia data ya uongo, kujiundia data, kuacha kutumia data fulani, kubadilisha data au kubadilisha matokeo. Utafiti huu ulizingatia maadili haya kwa kuhakikisha kwamba data yote mwafaka imekusanywa, imerekodiwa kwa usahihi na kuchanganuliwa. Data ilikusanywa kutoka kwa kazi za waandishi wa riwaya teule na kufasiriwa kutokana na waliyoandika peke yake bila kuongeza au kuficha data zozote.

Sounders M, Lewis P. na Thornhill A. (2011) wanasema kuwa watafiti wanafaa kuzingatia maadili ya utafiti ya taasisi zao. Maadili haya yanafaa kuzingatiwa katika kuandika mapendekezo ya utafiti, kufanya utafiti na kuandika tasnifu. Utafiti huu ulizingatia maadili haya kwa kufuata hatua hizi kwa kuandika pendekezo, kulitetea, kufanya marekebisho kwenye pendekezo jinsi yalivyopendekezwa na wasimamizi, kuomba kibali cha kufanya utafiti. Baadaye utafiti ulifanywa kwa kuzingatia mbinu za utafiti katika pendekezo lililoidhinishwa.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI, UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii kuna uchanganuzi, uwasilishaji na mjadala kuhusu matokeo ya utafiti ili kuafikia madhumuni ya utafiti huu. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia zinazoongoza utafiti huu, maswali na madhumuni ya huu utafiti. Mhimili wa kawanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuwa jamii ni mfumo wa asasi na michakato ya kijamii ambayo hutekekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na ni muhimu kwa asasi na michakato hii kuwa thabiti ili itekeleze majukumu yake ipasavyo. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuwa uchanganuzi wa hadithi unaweza kufanywa kwa kutumia vipengele vya kinaratolojia kama vile matumizi ya lugha, mandhari, mbinu za usimulizi kama vile aina za usimulizi, aina za wasimulizi, aina za mitazamo, wakati, daraja za usimulizi, msuko na aina ya wasomaji na pia wahusika na mbinu za kuwasawiri kama vile usawiri bainishi, uhusika wa kimatendo, uhusika wa kiusemi, uhusika wa kimazingira, uhusika wa muonekano wan a uhusika wa analojia. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu changamoto zinazoikumba ndoa na kuifanya ikose uthabiti wa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo zimemebainishwa. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia, kipengele cha wahusika na mbinu za kuwasawiri kimetumiwa kueleza namna changamoto zilizobainishwa zimejengwa na wahusika kupitia mbinu za kuwasawiri. Matokeo ya uchanganuzi wa data kwa kuzingatia mihimili hii ulijibu swali la kwanza la utafiti na kuafikiwa kwa madhumuni ya kwanza ya utafiti.

Sehemu ya pili ya sura hii inahusu uchanganuzi, uwasilishaji data na mjadala wa matokeo kuhusu jinsi athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao. Shughuli hii imeongozwa na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu na wa kwanza wa nadharia ya naratolojia. Jamii, asasi na michakato ya kijamii inaweza kuwa na athari hasi au chanya kwa jamii, asasi au michakato mingine. Michakato na asasi za kijamii zinafaa kuchanganuliwa kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, watu binafsi, makundi ya kijamii, asasi au michakato mingine ya kijamii. Mhimili wa kwanza unaeleza kuwa uchanganuzi wa hadithi unaweza kufanywa kwa kuzingatia vipengele vya kinaratolojia kama vile wahusika na

mbinu za kuwasawiri. Kwa kuongozwa na mhimili wa nadharia ya umuundo-uamilifu athari za changamoto za ndoa kwa wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au watoto wanaolelewa nao zimebainishwa. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia maelezo yametolewa kuhusu namna athari zilizobainishwa zinadhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao.

Sehemu ya tatu ya sura hii inafafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaosisitiza haja ya asasi za kijamii kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo umetumika kubainisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Mhimili huu umetumika pamoja na mhimili wa pili wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuwa uchambuzi wa usimulizi katika hadithi unafaa kufanywa kwa kuzingatia namna unahusiana na masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi husika. Masuala haya ni maudhui au yaliyomo. Kwa kuzingatia mihimili hii miwili njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimebainishwa na ufafanuzi kutolewa kuhusu namna zimewasilishwa na mbinu za usimulizi.Mbinu za usimulizi ambazo zimezingatiwa ni aina za usimulizi, aina za mitazamo na aina ya wasimulizi jinsi wanavyofafanua Wamitila (2003b) na Genette (1980.

## 4.2 Changamoto za Ndoa na Jinsi ambavyo Zimejengwa Kupitia Uhusika

Sehemu hii inachanganua na kuwasilisha data kuhusu changamoto zinazotatiza majukumu ya ndoa ya kuzaa na kulea kizazi kipya na jinsi ambavyo zimejengwa kupitia uhusika. Shughuli hii imeongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaoleza umuhimu wa asasi za kijamii kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhimili huu umetumika kubainisha changamoto zinazoifanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhimili wa pili wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu matumizi ya wahusika na mbinu za kuwasawiri kuchanganua hadithi umezingatiwa katika kueleza namna changamoto zilizobainishwa zimejengwa kupitia uhusika. Mbinu za kuwasawiri wahusika zinazozingatiwa ni matendo, mazingira, muonekano wa nje na usemi jinsi zilivyofafanuliwa na Kenan (1983

### 4.2.1 Ulevi na Usawiri wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi, Kimatendo, Kimazingira na kwa Muonekano wa Nje

Ulevi umesawiriwa na wahusika katika riwaya teule kupitia usawiri wao kimatendo, kiusemi, kimazingira na kwa muonekano wa nje kama ulivyofafanuliwa na Kenan (1983). Mbinu ya usemi huhusisha mhusika kuzungumza au kuwaza kuhusu masuala yanayomkabili katika kazi ya kifasihi. Katika riwaya ya *Kiu* ulevi umesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi na kimatendo. Katika riwaya hii ulevi umejengwa kupitia uhusika wa Bahati na Idi. Bahati anaisawiri kupitia uhusika wake kiusemi. Anamwambia hivi mfanyikazi wake anayeitwa Mwajuma:

> Basi ndugu yangu nikueleze nini! Ilikuwa raha ya siku mbili tatu tu. Alianza kuchomoka na ulevi, si ulevi huo, mimi nikatupiliwa mbali, nikatafuta roho yangu pa kuiweka. Tangu akishinda nje, hata akilala nje, hata sasa hukaa nje wiki nzima sijamshuhudia. Na kila siku yanazidi. Na wewe unayaona. Miaka mitano yote nimeishi katika hali kama hii-mpaka leo (uk. 141).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unasisitiza umuhimu wa asasi za kijamii kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo (Merton, 1957). Data hii inabainisha ulevi kama changamoto inayofanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Usemi huu unaonyesha namna usawiri wa wahusika kiusemi kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia namna unavyofafanuliwa na Kenan (1983) unaijenga changamoto hii. Unatolewa kwa hisia za masikitiko yanaodhihirishwa na matumizi ya kihisisi mwisho wa sentensi ya kwanza ya dondoo hili. Ulevi wa Idi umemkosesha Bahati furaha siku nyingi za ndoa yake. Mbinu ya tabaini imetumiwa kusisitiza hiki kitendo cha ulevi, kupitia maneno ‘ si ulevi huo’. Usemi huu unaonyesha kuwa kitendo hiki ni cha mazoea na kimekuwa kikiendelea kwa miaka mingi. Aidha kitendo hiki kinatokea mara kwa mara, Bahati anaeleza namna Idi hushinda na hata kulala nje hata wiki nzima. Hii inasisitiza tendo hili la ulevi na kuonyesha namna linayumbisha ndoa.

Nyaosi (2008) katika utafiti wake kuhusu ndoa anabainisha ulevi kama changamoto inayowakumba wake katika ndoa sawa na utafiti huu. Utafiti huu unaonyesha namna changamoto hii inavyofinyangwa kupitia usawiri wa wahusika. Bahati kupitia usawiri wake

kiusemi anaonyesha namna ulevi unafanya ndoa yake kukosa uthabiti. Ulevi unafanya Idi kutomjali mkewe naye Bahati anabakia kuishi kwa upweke. Kauli ya Bahati inaonyesha namna ulevi hufanya ndoa kukosa furaha na mahusiano ya karibu kati ya wanandoa. Ndoa ya Idi na Bahati inakosa kuwekewa msingi bora mara tu baada ya kuoana kwa sababu ya Idi kuanza kushiriki ulevi na kuendelea kunywa kupindukia. Uraibu wa pombe unafanya wawili hawa kukosa mshikamano wa hisia ambao ni muhimu katika kujenga ndoa imara. Idi anashinda na kulala nje huku Bahati akibaki nyumbani peke yake. Usawiri wa Bahati kiusemi unaonyesha namna wake huathiriwa na ulevi wa waume zao. Kupitia usemi wake anaonyesha namna ulevi husababisha upweke katika ndoa.

Katika riwaya ii hii ya *Kiu* ulevi umejengwa pia uhusika wa kimatendo na kiusemi. Imejengwa kupitia uhusika wa Idi. Idi anajenga ulevi kupitia usawiri wake kwa kitendo na usemi wake kwa pamoja. Anaamka kutoka kitandani usiku, anaenda nje ya nyumba yao na kuendelea kunywa pombe huku akiimba wimbo ambao unaeleza jinsi anavyothamini pombe kuliko mkewe. Kitendo na usemi wake Idi unasimuliwa hivi:

> Bahati upesi alichungulia dirishani, na kumwona mumewe amekaa juu ya domo la gari, kaegemea kioo, miguu yake ameitandaza mbele yake; chupa moja tupu ilikuwa chini juu ya mchanga, karibu na gurudumu la mbele; chupa nyingine yenye ulevi shinda, ilikuwa imesimama juu ya mdomo wa gari kati ya mapaja yake; mkononi mwake alikuwa na bilauri tupu. Alipofika kwenye ubeti wa pili wa wimbo wake, aliinyanyua chupa na bilauri juu ya kichwa chake, na huko huko juu aliijaza bilauri yake na huku ulevi mwingine ukimwaikia usoni. Ni- bu-u- re- ma- ringo- yako. . . nib o- o- ra m- vinyo wangu. . .(Uk. 114)

Kitendo hiki kinatatiza uthabiti wa ndoa ambao ni muhimu katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kama inavyosisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu na (Talcot, 1951). Data hii inaonyesha namna Idi anavyoisawiri changamato hii kupitia usawiri wa wahusika jinsi unavyofafanuliwa na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia. Katika kitendo hiki taswira imetumika kueleza tukio la unywaji pombe kupindukia la Idi. Msimulizi amechora mandhari ya ulevi, yaani kuwepo kwa chupa tupu ya pombe juu ya

mchanga, chupa shinda ya pombe na bilauri ya kumwagia pombe. Kitendo cha Idi cha kumwaga pombe juu ya bilauri iliyopo juu ya kichwa chake na hata kujimwagia kinaonyesha mhusika aliyeshindwa kudhibiti unywaji wake wa pombe. Sehemu ya wimbo wa Idi imejumuishwa katika dondoo hili. Maneno ya wimbo huu yameandikwa kwa silabi za kutenganishwa kumaanishwa maneno haya yanavutwa. Hii inaonyesha kuwa amelewa chakari na hawezi kutamka maneno vizuri. Wimbo huu unaonyesha kuwa anathamini sana pombe na ana mtazamo hasi kumhusu mkewe. Anamuona kuwa mwenye maringo. Matendo na maneno ya Idi yanaonyesha namna ulevi hufanya ndoa kukosa uthabiti. Kitendo chake kinamkosesha utulivu na amani maishani mwake. Kinampatia wasiwasi na analazimika kukatiza kulala kwake ili kuenda kumuokoa.

Ulevi umejengwa na wahusika kupitia usawiri wao kimatendo katika riwaya ya *Ua la Faraja* na pia katika riwaya ya *Kiu*. Kenan (1983) anasema kwamba mbinu ya matendo huhusisha matumizi ya matendo kuwasawiri wahusika. Matendo haya yanaweza kuwa yale ambayo wahusika wanayatenda, wanakwepa kuyatenda licha ya kufaa kuyatenda au yale ambayo wananuia kuyatenda. Ngoma katika *Ua la Faraja* anaisawiri kupitia usawiri wake kwa kitendo kifuatacho. Kitendo hiki kinasimuliwa na msimulizi akirejelea mawazo ya Juma kumhusu babake Ngoma. Kinasimuliwa hivi:

> Alijua kwamba baba yake hunywa kuanzia bia sita na kuendelea ndipo aridhike. Bila shaka huwanunulia bia nyingi hao wanawake wa pembeni anaodaiwa kuwa nao (Uk. 34).

Kitendo hiki kinaonyesha namna ulevi hufanya ndoa kutatizika katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu (Talcot, 1951). Mawazo ya Juma yanaonyesha kuchukizwa na uraibu wa pombe wa babake, anatumia pato lake kwa pombe na hawatunzi. Kitendo cha Ngoma kinachoisawiri changamoto hii ni cha mazoea kama anavyofafanua Kenan (1983) na kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia.Masua (2016) katika utafiti wake amegundua kuwa unywaji pombe kupindukia ni chanzo cha mizozo katika ndoa na hufanya wake kuwataliki au kutengana na waume zao. Hii kwa sababu unawafanya kukosa kuwajibikia mahitaji ya familia zao. Unywaji pombe kuindukia wa Ngoma unafanya akose kuwatunza watoto wake pamoja na mkewe. Kitendo cha Ngoma kinaambatana na uasherati, anajinunulia bia na hata kuwanunulia wapenzi wake wa pembeni.

Msimulizi anatumia mawazo ya mwanawe Ngoma kueleza kitendo cha ulevi wa Ngoma. Inasikitisha kwamba ulevi na uasherati wa Ngoma unafahamika na mwanawe ilhali anatarajiwa kuwajibikia malezi yao na kuwa mfano bora kwao.

Ulevi katika riwaya ya *Kiu* unasawiriwa na Idi kupitia usawiri wake kwa muonekano wa nje. Muonekano wake wa nje unasimuliwa hivi :

> Alimkuta amelala vile vile kifudifudi. Koti lake jeusi lilikuwa limepiga peto mgongoni na kuwa na alama za mabaka kama lenye lililolaliwa penye unato wa kitu. Mguu mmoja wa suruali yake ulikuwa umekunjika, soksi yake imeteremka hadi kwenye kisigino cha kiatu ambacho nyuzi zake zilining'inia mpaka sakafuni. (Uk.109)

Muonekano huu wa Idi unaonyesha namna ulevi unamfanya mwanandoa kukosa kujidhibiti na kufanya ndoa kukosa uthabiti wa kuifanya itekeleze majukumu yake baraba kwa mujibu mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mbinu ya muonekano wa nje hudhihirishwa na maumbile na mavazi aliyonayo mhusika (Kenan, 1983). Mathalani mhusika akiwa amevalia matambara hii inadhihirisha kwamba yeye ni maskini. Dondoo hili linatupatia taswira ya hali ya ulevi ya Idi. Hii inatokana na maelezo ya msimulizi kuhusu mavazi yake, koti lenye mabaka, mguu mmoja wa suruali uliokunjika na soksi iliyoteremka. Muonekano wa Idi unaonyesha namna ulevi unaweza kumfanya mwanandoa kukosa kujali au kuwa mwangalifu kuhusu jinsi anavyovalia au anavyoonekana akiwa amelewa chakari. Anakosa nguvu za kumwezesha hata kufunga kamba za viatu na hata kuketi na inabidi ajitupe kitandani. Mawasiliano kati ya hawa wawili yanakatizwa na ulevi. Idi anarejea nyumbani na kimyakimya anajitupa kitandani na kulala bila kumjulia hali mkewe ambaye ameshinda nyumbani.

Ulevi umesawiriwa na Ngoma katika *Ua la Faraja* kupitia usawiri wake kimatendo na kimazingira. Ngoma amesawiri ulevi kupitia mazingira ya Malaika Bar ambamo anaenda jioni moja kunywa pombe. Mazingira haya yanasimuliwa hivi:

> Ngoma alikuwa amemaliza bia yake. Alipoondoka Malaika alipitia karibu ya Omolo na kumsalimu, " Vipi bwana mdogo. Leo waonekana ulevi umezidi kidogo?"

Mazingira haya yana  wanywaji pombe wengine kama vile Omolo, Chiku na pendo wanaitisha na kuendelea kunywa pombe. Anaondoka baada ya kunywa kwa muda. Kumwambia Omolo kuwa ulevi ulikuwa umemzidi kunaonyesha wanafahamiana na hukutana katika mazingira haya kila mara. Wazazi wana wajibu wa kuwafunza wanao kanuni na amali za jamii yao (Talcot, 1951).

Matokeo ya utafiti yamebainisha ulevi kuwa changamoto ambayo inaikumba ndoa na kuifanya ikose kutekeleza majukumu yake barabara kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili hueleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi ambazo hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Nyaosi (2008) pia ameijadili changamoto hii katika utafiti aliofanya kuhusu changamoto zinazowakumba wake katika ndoa. Gicuku (2012) ameeleza kuhusu namna wazazi hupotelea kwa unywaji pombe na kukosa muda wa kuwalea watoto wao. Utafiti huu tofauti na tafiti hizi,umechunguza namna ulevi umejengwa kupitia usawiri wa wahusika kiusemi, kimatendo, kwa muonekano wa nje na kimazingira. Katika riwaya ya *Kiu* ulevi umejengwa kwa uhusika wa kiusemi, kimatendo na wa muonekano wa nje. Kwenye riwaya ya *Ua la Faraja* umejengwa kwa uhusika wa kimatendo na kimazingira.

**4.2.2 Talaka na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi**

Kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu ndoa hutekeleza majukumu muhimu ya kuzaa na kulea kizazi kipya. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha talaka kama changamoto ambayo hufanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia talaka imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya teule. Talaka imejengwa katika riwaya ya *Kiu* kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi kwa pamoja. Talaka katika riwaya hii imejengwa na Bahati na Idikupitia usawiri wao kimatendo na kiusemi. Kitendo na usemi  wa Idi anaosawiriwa kwao unasimuliwa ifuatavyo na mtumishi wake Mwajuma:

> Ba…basi Idi akatoka- kimya…kimya…kimya… mara akaja hapo kwa kishindo: Darl, tayari; tazama! Akamwonyesha hiyo talaka. (Uk. 152)

Kitendo hiki kinaibua talaka ambayo ni changamoto inayoifanya ndoa kuvunjika na kufanya ikose kutekeleza majukumu yake kama yanavyofafanuliwa na Talcot (1951), na kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa naratolojia unaoleza kuhusu usawiri wa wahusika kimatendo wa Idi unaonyeshwa na dondoo hili unaijenga talaka. Idi anakitenda kitendo hiki kwa haraka na bila kuwazia athari zake kwa Bahati. Matumizi ya kihisishi baada ya neno tazama yanadhihirisha hisia nzito za hasira alizo nazo Idi anapochukua hatua ya kumtaliki mkewe. Marudio ya neno ‘kimya’ katika dondoo hili yanatilia mkazo kimya cha Idi anaposhughulika kumtaliki mkewe. Alama za mdokezo zinaonyesha kusitasita au kukata kwa usemi Mwajuma anaposimulia. Hii inaonyesha hisia za hasira au huruma za Mwajuma kutokana na kitendo anachosimulia.

Idi anamtaliki Bahati bila sababu muhimu. Anamtaliki Bahati baada ya kumfumania akiwa nyumbani kwao na hawara wake Rehema. Baada ya kufumaniwa Idi anaenda kwa shehe, anapewa barua ya talaka, anakuja nayo na kumuonyesha Rehema na kisha anamkabidhi mhudumu wao Mwajuma ampelekee Bahati nyumbani kwao. Talaka imesawiriwa na Idi kupitia usawiri wake kwa usemi ufuatao:

> Shahada yako, shahada yako! Kesho asubuhi utaipata. Siwezi kupoteza wakati wangu sasa hivi kumtafuta shehe. Kesho asubuhi nitakuletea huko huko…Haya toka! (Uk. 149)

Usemi huu unadhihirisha usawiri wa changamoto hii kupitia uhusika wa kiusemi kulingana na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia. Usemi huu unaonyesha hasira alizo nazo Idi kutokana na matumizi ya kihisishi mwishoni mwa sentensi ya kwanza na pia mwishoni mwadondoo. Matumizi ya alama za dukuduku yanaonyesha kwamba kuna maneno ambayo yamedondolewa au kukatizwa kwa usemi wa Idi. Msisitizo kuhusu talaka katika usemi wa Idi umedhihirishwa na marudio ya neno ‘shahada yako’. Maneno haya yanaonyesha mamlaka ambayo mume ako nayo juu ya mkewe katika ndoa. Wamitila (2002) anasema kuwa mwanamke ni mshirika wa pili katika ndoa. Idi anaamua kumtaliki mkewe ghafla na kumuamuru kuondoka ilhali hajamkosea. Hampatii Bahati nafasi ya kusikilizwa ili kujitetea kuhusu uamuzi anaofanya wa kumtaliki.

Katika *Ua la Faraja* talaka imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo peke yake. Ngoma katika riwaya hii ameijenga talaka kwa usawiri wake kimatendo. Kitendo hiki ni cha kutaliki kama kinachotendwa na Idi. Juma ambaye ni mtoto wa Ngoma anamsimulia Omolo kitendo hiki. Anasema:

> Sijui. Lakini bosi unajua baba aliyomtendea mama. Mama alipogundua kwamba baba kamwambukiza ugonjwa mbaya, hakufanya lolote ila alikabithi yote kwa Mungu. Lakini mama alipoamua kurudia dini yake ya kuzaliwa, bila huruma, baba akampa talaka na kumfukuza nyumbani. (uk. 236)

Kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu na mawazo ya Talcot (1951) ndoa ina jukumu la kulea kizazi kipya. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa na wa pili wa nadharia ya naratolojia usawiri wa Ngoma kupitia kitendo hiki unaibua talaka na kutatiza kutekelezwa kwa jukumu hili la kulea watoto. Matendo ya Ngoma ni ya kinaya kwa kuwa anatenda kinyume na mafundisho ya dini yake lakini anamtaliki mkewe kwa kuihama dini hii. Anashiriki uasherati, ulevi na kuitelekeza familia yake na anajifanya kwamba anaipenda sana dini yake. Matendo yake yanaonyesha uonevu kwa mkewe. Kwa mujibu wa nadharia ya umuundo- uamilifu mume anafaa kukidhi mahitaji ya familia lakini Ngoma anamwachia mkewe majukumu haya. Kusimuliwa kwa matendo yake na mwanawe kunaonyesha namna changamoto za ndoa huathiri watoto kimawazo. Maneno ya Juma yanaonyesha kuwa kitendo cha babake ni cha maonevu.

Charles (2008) anasema talaka huathiri wanandoa, watoto wao na jamii kwa njia hasi. Masua (2016) anajadili sababu ya wanawake kutengana au kutalakiana na waume zao. Sababu anazotoa ni wanawake kuamua kuvunja ndoa zao baada ya kushindwa kukabiliana na changamoto za ndoa kama vile ukatili. Hii ni tofauti na utafiti huu ambao sababu ya waume kuwataliki wake zao hazitokani na wao kushindwa kukabiliana na changamoto zinazokumba ndoa zaao. Wote wanawataliki wake zao kwa sababu za kibinafsi bila kuwazia athari zake kwa wake hawa na watoto. Ili ndoa iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo wanandoa hawana budi kuepuka talaka ijapokuwa pale ambapo pana sababu za kutosha kufanya hivyo kama vile ukatili. Talaka kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu inafanya ndoa kuvunjika na kukosa kutekeleza majukumu

ambayo inatarajiwa kutekeleza. Matokeo ya utafiti huu tofauti na mawazo ya Charles (2008) yanaonyesha namna changamoto hii imejengwa na wahusika kupitia uhusika wao kimatendo na kiusemi. Katika riwaya ya *Kiu* imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi kwa pamoja. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imejengwa kwa uhusika wa kimatendo peke yake. Katika riwaya hii kitendo kilichotumiwa kumsawiri Ngoma na kuibua changamoto hii kimeripotiwa na Juma ambaye ni mwanawe Ngoma.

### 4.2.3 Uasherati na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo

Kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia jamii imeundwa kwa asasi za kijamii zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na uthabiti wa asasi hizi ni muhimu katika kuziwezesha kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Utafiti huu umebainisha uasherati kama changamoto ambayo inaifanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Katika riwaya ya *Kiu* uasherati umejengwa kupitia uhusika wa kimatendo. Idi katika *Kiu* anaisawiri changamoto hii kupitia tendo la kumleta hawara wake Rehema na kuzini naye kwenye kitanda chake na Bahati. Bahati anafichuliwa tendo hili na mtumishi wao Mwajuma. Alimwambia kuwa Idi alikuwa akimleta hawara wake nyumbani wakati yeye hayupo. Bahati alifanya mpango wa kuwafumania kwa kwenda kwao na kumwambia Idi kuwa atarejea baada ya wiki moja. Alirejea mapema na kumfumania Idi akiwa na hawara wake nyumbani kwao. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Bahati aliuona uso wa mumewe, Idi, ukijongea kwenye uso wa yule mrembo, mkono wake wa pili ukiachia chupa na kumvaa shingoni; alikiona kile kisura kikijisalimisha kwa mumewe kwa hamu na shauku, akaiona midomo yao ikikutana. Mtume! Bahati hakuweza tena kusubiri. Alichomoka pale akawatokea uwanjani na kuwafumania. (Uk. 147)

Matendo haya yanaibua taswira ya uasherati unaohusisha Idi na Rehema. Idi kumvaa Rehema shingoni na wao wawili kukutanisha midomo yao kunaibua uasherati. Matendo haya yanapoonza kusimuliwa yanajenga taharuki, msomaji anakuwa na mvuto wa kujua yatakayotokea baadaye. Hatimaye Bahati anashindwa kuvumilia kushuhudia yanayoondelea na kuwafumania. Kihisishi ‘ Mtume!’ kimetumika katika dondoo hili kuonyesha hisia za mshangao wa Bahati kutokana na

anayoshuhudia. Anaona tukio hili kama usaliti kwa ndoa yao. Kitendo hiki cha Idi kinaonyesha kwamba Idi haiheshimu ndoa yake na anamdharau sana mkewe kwa kufikia kiwango cha kumleta Rehema nyumbani na kuzini naye juu ya kitanda chao. Hajali kuhusu mustakabali wa ndoa hii kutokana na kushiriki uasherati. Kitendo hiki kinafanya Bahati kupata uchungu moyoni kwa kuona mapenzi aliyoahidiwa yameelekezwa kwa mwanamke mwingine. Anashindwa kujizuia na kuamua kuwafumania badala ya kuendelea kushuhudia ingawa hatua hii haiokoi ndoa yao. Mbali na kitendo hiki kumsawiri Idi na kusawiri uasherati kinaonyesha madharau ya Idi kwa ndoa yao na kwa Bahati. Nyamete (2016) anasema kuwa madharau ya mwanandoa kwa mwenzake husababisha mizozo katika ndoa. Madharau ya Idi kwa Bahati kupitia kitendo hiki yanasababisha mzozo katika ndoa yao. Uasherati mbali na kuwa usaliti kwa mmoja wanandoa unaweza kuchangia katika kuvunjika kwa ndoa. Ndoa ya Idi inavunjika mara tu baada ya mkewe kumfumania akiwa na hawara wake Rehema. Idi anamtaliki mkewe kwa kumfumania ilhali yeye ndiye mwenye makosa.

Charles (2008) akirejelea taaluma ya Sosholojia anaeleza namna uasherati unatatiza uthabiti wa ndoa na kusababisha talaka. Gicuku ( 2012) japo hachunguzi namna changamoto za ndoa zinafinyangwa, anasema kuwa ili ndoa idumu lazima kuwe na heshima na uaminifu kati ya mume na mke. Usawiri wa kimatendo wa Idi unaonyesha kwamba hamheshimu mkewe na hii ndio sababu ya yeye kumleta hawara wake na kuzini naye juu ya kitanda chao kila mara Bahati anapokosa kuwa nyumbani. Uasherati wa Idi unamfanya amtaliki mkewe anapomfumania na hawara wake Rehema. Hii inafanya ndoa yao ya miaka mitano kuvunjika bila kutekeleza jukumu la ndoa la kuzaa na kulea watoto.

Uasherati katika riwaya ya *Ua la Faraja* umejengwa kupitia uhusika wa kimatendo. Ngoma katika riwaya hii ameijenga changamoto hii kupitia usawiri wake kimatendo. Anakuwa na wapenzi wengi nje ya ndoa yake. Kitendo anachotenda kinachosawiri changamoto hii kinasimuliwa hivi:

> Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumania nyumbani kwa Queen. Alikuwa anajua tabia ya uzinzi ya jirani yake (Uk. 71).

Dondoo hili linaashiria kuwepo kwa uasherati katika ndoa hii na kutatiza uthabiti wake. Hii inaathiri utekelezaji wa majukumu yake ya kulea watoto kwa mujibu wa mhimili wa kwanza nadharia ya umuundo- uamilifu na maoni ya Talcot (1951) kuhusu majukumu ya ndoa. Inasawiriwa na kupitia uhusika wa Ngona kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Kitendo hiki cha uasherati wa Ngoma kinasimuliwa kupitia kwa Omolo. Mhusika huyu ni jirani yake na amewahi kumfumania nyumbani kwa Queen. Aidha anakiri kuwa Ngoma ni muasherati. Kupitia usawiri wa mhusika huyu uasherati unaonyeshwa namna unaathiri ndoa na kuifanya ishindwe kulea kizazi. Ngoma anatumia pato lake kwa uasherati na ulevi na kuitelekeza famila yake. Hatimaye anapata ukimwi na kumuambukiza mkewe. Wote wanafariki na kuwaacha wanao yatima. Hii inaonyesha namna uasherati unaweza kuangamiza wanandoa na kutatiza malezi ya watoto.Wanandoa wanafaa kujiepusha na tamaa inayowasukuma kushiriki uasherati ili wasijiangamize na kutatiza malezi ya wanao. Nyaosi (2008) anatambua uasherati katika utafiti wake kuhusu ndoa japo utafiti wake unaegemea namna wake wanadhulumiwa na waume wao katika ndoa. Matokeo ya utafiti huu hayabainishi tu uasherati kuwa changamoto ya ndoa bali yanaeleza namna unasawiriwa na wahusika kupitia uhusika wao.

Kasina Usini Sina katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ( 2008) anaisawiri changamoto hii kupitia usawiri kwa  kitendo cha kuzini hata na wasichana wa kazi aliowaajiri mkewe na hata kuwaringa mimba. Matendo yake yanasimuliwa hivi:

> Tangu zamani Kasina Usini Sini alikuwa na tabia ya kuwanyemelea wanawake wengine wa nje. Watu waliomjua wakawa wanamshauri aache hiyo tabia ya jogoo kwa sababu ina madhara makubwa (Uk. 239)

Kulingana na nadharia ya umuundo- uamilifu uthabiti wa ndoa na utekelezaji wa majukumu yake barabara hutiliwa mkazo. Dondoo hili linadhihirisha kuwepo kwa uasherati katika ndoa ya Kasina na wakeze ambao unaifanya ikose uthabiti na kutotekeleza majukumu yake barabara. Msimulizi anasimulia namna changamoto hii inasawiriwa na Kasina kupitia uhusika wa kimatendo jinsi unavyofafanuliwa na Kenan(1983). Kwa mujibu wa dondoo hili haya matendo ya uasherati yameanza siku nyingi zilizopita na kuendelea.

Kitendo hiki kimepita mipaka hadi wanakijiji wanakilinganisha na cha jogoo. Uasherati unafanya ndoa ishindwe kutekeleza jukumu la malezi barabara. Kasina anapata watoto wengi nje ya ndoa ambao anashindwa kuwakimu. Watoto hawa wanamjia siku moja akihutubia umati kumtaka agharamie mahitaji yao.

Matokeo ya utafiti huu yanafanana na ya Nyaosi (2008) na ya Gicuku (2012) kwa kuwa yanabainisha uasherati kuwa changamoto ya ndoa. Hata hivyo matokeo haya hayabainishi tu hii changamoto bali yanaeleza namna ambavyo imejengwa na wahusika kupitia mbinu za kusawiri wahusika ambazo zimetumika kuwasawiri. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa uasherati umejengwa kwa uhusika wa kimatendo katika riwaya zote teule. Matendo yote yamehusisha wahusika waume ambao wanakuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa. Uasherati katika *Kiu* umejengwa kwa kitendo cha Idi kufumaniwa moja kwa moja akihusiana kwa karibu na hawara wake Rehema. Katika *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?* matendo ya wahusika ambayo yametumika kuwasawiri na hivyo kuijenga changamoto hii yameripotiwa na msimulizi. Msimulizi anaripoti matendo ya wahusika kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa zao.

### 4.2.4 Umaskini na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo, Kiusemi, Kimazingira na Muonekano wa Nje

Kulingana mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu na mawazo ya Talcot(1951) ndoa inatekeleza jukumu la kulea watoto na kukimu mahitaji yao. Umaskini umebainishwa kuwa changamoto ambayo inafanya wanandoa kushindwa kulea wanao barabara. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia na maoni ya Kenan(1983) kuhusu usawiri wa wahusika maelezo yametolewa kuhusu namna umaskini umejengwa kupitia uhusika. Umaskini umesawiriwa na wahusika wanandoa kupitia usawiri wao kimatendo, kiusemi kimazingira, na kwa muonekano wa nje. Katika *Kiu* umaskini umesawiriwa kupitia usawiri kiusemi wa Cheusi. Cheusi anasawiri umaskini kwa usemi ufuatao:

> Sasa mwanangu, arusi mnaitaka namna gani ? Nyinyi ndio vijana, semeni mpendavyo. Lakini mambo yenyewe yawe rahisi hali zetu ndogo- kila ndege huruka kwa mbawa zake…Ah, maskini baba yake Bahati, angekuwa ingeandaliwa arusi ya ndovu kumla mwanawe !...Ah , maskini miye, mkono mtupu haurambwi ! (Uk.73)

Kwa mujibu wa dondoo hili ndoa hii inakabiliwa na umaskini ambao unafanya itatizike kumudu gharama za harusi ya kufana anayotarajia Cheusi. Hii ina maana kwamba inatatizika katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Uhusika wa Cheusi kiusemi kwa mujibu mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia unasawiri umaskini unaoikumba ndoa hii. Usemi wa Cheusi unaonyesha wasiwasi alionao kuhusu arusi ya Bahati. Wasiwasi wake unatokana na umaskini unaomkumba. Katika usemi huu anatumia methali kurejelea uwezo wake mdogo. Kila ndege huruka kwa ubawa wake ina maana kila mtu hutenda jambo kulingana na uwezo wake. Yeye anataka gharama za arusi ziwe ndogo kwa sababu ya umaskini wake. Anasikitika kuwa Bahati hataandaliwa arusi ya kufana sana (Ya ndovu kumla mwanawe) kwa sababu ya umaskini unaochangiwa na kutokuwepo kwa mumewe Jaku. Cheusi anatumia methali, mkono mtupu haurambwi kuelezea hali yake ya umaskini.

Umaskini umesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika kiusemi katika riwaya ya Katika *Ua la Faraja* (2005). Umesawiriwa kupitia usemi wa Tabu unaosimuliwa hivi :

> Sisi tumezoea: nguo mpya ni wakati wa sikukuu ya Idd. Sasa eti kila leo utoke na nguo mpya, si watu watatushangaa! (uk. 134).

Kauli hii inaibua changamoto ya umaskini katika ndoa hii ambao unaifanya ishindwe kutekeleza barabara jukumu la kukimu mahitaji ya kimsingi ya watoto. Hii ina maana kuwa imeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Kauli hii inaonyesha hii changamoto namna imejengwa kwa uhusika wa kiusemi kama unavyofafanuliwa na Kenan (1983). Usemi wa Tabu unaonyesha kinaya, inatarajiwa afurahie kitendo cha Ngoma kuwanunulia yeye na watoto nguo kila mara lakini hafurahi. Madai yake kwamba watu watawashangaa kwa kuvalia nguo mpya kila siku yanaonyesha umaskini wa ndoa hii. Wamezoea kuvaa nguo zilezile kila siku. Tabu anakejeli tabia ya mumewe kuanza kuwanunulia nguo kila mara baada ya kuwatelekeza kwa muda mrefu licha ya kuwa na uwezo. Kauli hii ya Tabu inaonyesha namna hali ya umaskini huwafanya wanandoa kutamauka na kufikia hatua ya kuzoea na kukubali hali yao ya umaskini. Tabu na watoto wake walikuwa wanaona ukosefu wao wa mahitaji umekuwa jambo la kawaida na watu wamezoea kuwaona

katika hali hii. Hii huweza kutokea katika ndoa ambapo umaskini haujasababishwa na wanandoa wote kukosa pato zuri bali hali ambapo mmoja anapata pato zuri lakini analitumia kwa starehe na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi. Usemi huu wa Tabu unashadidia ya kauli ya Gicuku (2012) kwamba umaskini hufanya maisha ya ndoa kuwa magumu na unaweza hata kuivunja. Umaskini unafanya maisha ya Tabu na watoto kwa kuwa unafanya wakose mahitaji ya kimsingi kama nguo. Tofauti na utafiti huu, mtaalamu huyu alikuwa anatafiti kuhusu ndoa na wala si namna changamoto zake zinasawiriwa kupitia uhusika. Anasema kuwa umaskini hufanya wanandoa kukosa mahitaji muhimu na kufanya maisha yao kuwa magumu.

Usawiri wa wahusika kimatendo umechangia usawiri wa umaskini kibunilizi katika riwaya ya *Kiu* kupitia usawiri wa Cheusi. Mhusika huyu anasawiri umaskini kupitia kitendo cha kuomba kinu kila mara kutumia kutwanga mchele. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi :

> Alikuwa amekwenda kwa jirani kutwanga mchele wake wa biashara, ingawa siku zote akisema kuwa Mungu angemjalia angenunua kinu chake mwenyewe, kwani uso umeumbwa na haya, naye amechoka kupiga hodi kwa majirani. (Uk. 34)

Dondoo hili linadhihirisha kuwa ndoa hii inakumbwa na umaskini unaoikosesha uthabiti ambao ni muhimu kwa ndoa kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Linaonyesha namna unawasilishwa kwa uhusika wa kiusemi kama unavyofafanuliwa na Kenan ( 1983) na kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia kuhusu uhusika. Kitendo hiki kinaashiria unyonge wa Cheusi kutokana na kushidwa kununua vifaa vyake na kulazimika kuazima kutoka kwa majirani kila mara. Kitendo hiki kinatendeka kila mara, hii inathibitishwa na maelezo ya msimulizi kuwa Cheusi amechoka kupiga hodi kwa majirani na kuomba siku zote Mungu amjalie kununua kinu chake. Murungi (2013) anajadili kuhusu umaskini anahakiki mtindo katika tamthilia ya *Natala*. Anaeleza namna wahusika wanashindwa kumudu gharama ya kununua vifaa vya kutumia kwa sababu ya umaskini unaowakumba. Cheusi hakuweza kujinunulia kinu chake kwa sababu ya umaskini na analazimika kuomba kila mara. Hiki kitendo cha kuombaomba kinamsawiri na kuibua changamoto ya umaskini. Cheusi anaaibika kutokana na kitendo cha kuomba kila mara, hii ndio

sababu ya kusema uso una haya. Usemi huu unaonyesha namna umaskini unasababisha mahangaiko kwa wanandoa na kufanya washindwe kuendesha maisha yao barabara.

Umaskini umesawiriwa na wahusika kwa kusawiriwa kimazingira. Mbinu ya mazingira huzingatia makaazi ya mhusika na hata jamaa zake au watu anaoishi nao au wanaomzunguka ( Kenan, 1983). Kwa mfano mhusika anaweza kuelezwa kuwa anaishi katika nyumba chafu ili kuonyesha kutowajibika kwake. Cheusi katika riwaya ya *Kiu* anaisawiri changamoto hii kupitia mazingira ya nyumba duni ambamo anaishi yeye na mwanawe Bahati. Hali ya nyumba hii inasimuliwa hivi:

> Nyumba ya Bahati na mamake ilikuwa imezeeka sana. Haikuweza kubadilishwa kitu tangu marehemu baba yake isipokuwa mikono miwili au mitatu hivi ya chokaa nyeupe.
> Si kuta, si mlango, si paa, vyote vilionekana mfano wa kizee anayeomba mauti. (Uk. 18)

Mazingira haya yanaibua umaskini unaokumba ndoa hii. Akirejelea riwaya ii hii Nyaosi (2008) anabainisha umaskini kuwa moja ya changamoto za ndoa japo hachunguzi namna unafinyangwa kupitia uhusika na usimulizi kama utafiti huu. Hali ya nyumba hii inaonyesha kutatizika kwa ndoa hii kutekeleza jukumu la kulea kizazi kipya kulingana na Talcot (1951) na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Hali duni ya nyumba hii imesisitizwa kwa matumizi mbinu ya kifasihi ya tabaini. Hii inaashiriwa na matumizi ya 'Si kuta, si mlango, si paa'. Hii ina maanisha kwamba kila sehemu ya nyumba hii ilikuwa imezeeka. Aidha uduni wa nyumba hii umesisitizwa kwa kutumia tashibihi, kila sehemu yake inalinganishwa na kizee anayeomba mauti kumaanisha kuelekea kuharibika kabisa. Hali ya nyumba hii inatatiza jukumu la ndoa la kukidhi hitaji la makaazi bora kwa wanandoa na watoto. Cheusi hakuwa na pesa za kuweza kujenga nyumba nzuri au kuifanyia ukarabati. Tumaini lake lilibakia Bahati akue na amwauni kutoka kwa hili lindi la umaskini. Hata hivyo ndoto hii inakosa kufaulu Bahati anapotalakiana na mumewe na kutoweka asijulikane alipo.

Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* mbinu hii ya kusawiri wahusika kimazingira imetumiwa kumsawiri Mama Josii na kuchangia ujenzi wa umaskini. Mama Josii amesawiriwa kupitia mazingira ya nyumba duni anamoishi. Mazingira ya nyumba yake yanasimuliwa hivi:

> Nyumba yake yavuja maji paani na ukutani (Uk. 68)

Mazingira haya ni nyumba ndogo anamoishi na inayovuja maji paani na ukutani. Mazingira haya yanajenga umaskini ambao unaifanya ndoa hii kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kulea watoto barabara kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaoeleza kuhusu haja ya asasi za kijamii kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Ndoa hii inashindwa kugharamia nyumba nzuri. Mazingira kama haya ni hatari kwa afya ya watoto na hata wazazi wao. Mama Josii alifanya biashara ndogo ambayo haikumpatia faida ya kumwezesha kugharamia nyumba kubwa na nzuri. Mumewe alikuwa mgonjwa sana na kufanya mama huyu abebe mzigo wa kuilea familia peke yake.

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani ?* umaskini umejengwa na mamake Mwanamuka kwa kusawiriwa kwa muonekano wa nje. Kenan (1983) anasema kuwa mbinu hii huhusisha usawiri wa mhusika kwa kutumia maumbile yake au mavazi yake. Muonekano wake wa nje wa Mwanamuka unasimuliwa hivi :

> Siku ya pili akafukuzwa kwa kwenda kwa gauni lililokuwa na shimo begani na kuonyesha mabega yaliyoparara. Hawezi hata kujipaka sabuni ya kipanga ? Akarudi zake na kuamua kujivika fulana ya shule ya binti yake (Uk. 63)

Muonekano wa nje wa mamake Mwanamuka ambao unajenga umaskini ni mavazi duni ambayo amevalia. Mavazi haya ni gauni ambayo ina shimo mabegani na kuonyesha mabega yaliyoparara. Hii inaonyesha kushindwa kwake kujikimu kwa mahitaji ya kimsingi kama nguo bora. Analazimika kuvalia fulana ya shule ya binti yake kwa sababu hakuwa na nguo nyingine bora ya kuvalia ndipo arudi kuendelea kumtafutia bintiye msaada wa masomo. Muonekanowa mamake Mwanamuka unaonyesha jinsi umaskini unawafanya wazazi washindwe kugharamia hata mahitaji yao ya kimsingi kama nguo na kuikosesha ndoa uthabiti.

Nyaosi (2008) na Gicuku (2012) wanajadili umaskini kama changamoto ya ndoa katika matokeo ya tafiti ambazo walifanya kuhusu ndoa. Utafiti huu vile vile unajadili umaskini kama changamoto ya ndoa katika matokeo yake. Umaskini unafanya wanandoa kushindwa kukidhi

mahitaji yao na watoto na hivyo kushindwa kutekeleza ipasavyo majukumu ya ndoa ya kuzaa na kulea kizazi kipya. Hata hivyo, utafiti huu umeeleza namna umaskini umejengwa kupitia uhusika kwa kurejelea riwaya teule. Katika riwaya ya *Kiu* umaskini umejengwa kupitia uhusika wa kiusemi, kimatendo na kimazingira. Cheusi anatoa kauli ya kukiri kuwa yeye ni maskini, anaomba kinu kila mara na hata kuona aibu na pia anaishi katika nyumba duni. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* umaskini umesawiriwa kupitia uhusika wa kimazingira peke yake kupitia Mama Josii kuishi katika nyumba inayovuja paa na kuta. Katika *Ua la Faraja* umaskini umesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi. Tabu anakiri kuwa yeye na watoto huvaa nguo mpya kwa nadra. Katika *Unaitwa Nani ?* umaskini umejengwa kwa muonekano wa nje. Mamake Mwanamuka anavalia gauni ambayo ilikuwa na shimo begani na kuonyesha mabega yaliyoparara.

### 4.2.5 Kutowajibika na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi ambazo hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na asasi hizi zinafaa kuwa thabiti ili zitekeleze majukumu haya ipasavyo (Merton, 1957). Kutowajibika kumebainishwa kuwa changamoto ambayo inaifanya ndoa kukosa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kutowajibika kunaelezwa jinsi kumejengwa kupitia uhusika kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Kutowajibika kumesawiriwa kimatendo na kiusemi na wahusika ambao wanaacha kuwatunza watu wanaotarajiwa kuwatunza au wanaowategemea. Kutowajibika kumesawiriwa na Jaku katika riwaya ya *Kiu* kupitia uhusika wake kimatendo. Kitendo cha Jaku kinachosawiri changamoto hii kinasimuliwa hivi :

> Jaku ndiyo kayoyomea…Inasemekana alionekana miaka sita iliyopita akielekea upande wa Kongo. Alimwachia mkewe ulezi wa Bahati peke yake, na mkemtu alifunga mkaja akamlea mwanawe kwa vitanga vya mikono, kwa jasho na machozi, hata akafika sasa miaka kumi na minane. (Uk. 29)

Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia dondoo hili linaonyesha namna changamoto hii inasawiriwa na Jaku kupitia uhusika wake kimatendo. Kitendo hiki ni cha kukwepa kutenda yale ambayo mhusika anatarajiwa kutenda jinsi anavyofafanua Kenan (1983).

Jaku anakwepa kumlea Bahati na anamwachia mkewe jukumu hili. Gitau (2011) katika utafiti wake kuhusu kudhulumiwa kwa wanaume anaeleza kuwa baadhi ya wanaume hushindwa kutekeleza majukumu yao na kuondoka wakitarajia kujiinua kiuchumi wanakoenda. Wao huwaachia wake zao majukumu ya kujikimu na kuwakimu watoto. Jaku anakwepa kutenda kitendo cha kumtunza mkewe na Bahati kwa miaka sita. Katika dondoo hili maelezo yanatolewa kuhusu namna Cheusi alitelekeza jukumu la kumlea Bahati baada ya Jaku kutoweka. Anamlea kwa vitanga vya mikono, jasho na machozi. Hii ina maana anamlea kwa ukosefu wa mahitaji muhimu, kwa kutaabika kupata mahitaji haya na hata kwa huzuni au kukosa furaha. Cheusi analazimika kufanya kazi ya kupika maandazi na mikate hadi usiku wa manane wakati majirani zake wamelala. Msimulizi anaeleza kuwa baada ya Jaku kuondoka maisha ya Cheusi yalikuwa ya taabu na yalijaa upweke.

Nyaosi (2008) anajadili kutowajibika kwa waume kama changamoto inayokumba wanawake walio katika ndoa. Utafiti huu mbali na kuibainisha kama changamoto ya ndoa unaeleza namna imejengwa kupitia uhusika. Uhusika wa Cheusi unaonyesha namna kutowajibika kwa mmoja wa wanandoa huifanya ishindwe kutekeleza jukumu la malezi ya watoto. Ili ndoa iwe thabiti wanandoa hawana budi kuwajibika na kusaidiana kuendesha maisha ya ndoa yao. Maisha ya ndoa yanahitaji mchango wa kila mwanandoa kukabiliana na changamoto za ndoa na haifai mmoja kumwacha mwenzake kushughulika peke yake. Ingawa ndoa hii ilikumbwa na umaskini, ilifaa Jaku amsaidie mkewe kukabiliana nao na wala si kumwacha Cheusi kuhangaika peke yake.

Katika *Ua la Faraja* (2005) changamoto hii imesawiriwa na Ngoma kupitia usawiri wake kimatendo. Kitendo kinachoijenga changamoto hii ni cha kutomtunza mkewe na watoto. Kitendo hiki kinasimuliwa na Juma ambaye ni mtoto wa Ngoma. Juma anamsimulia jirani yao Omolo. Anasema :

> Sasa jinsi siku zilivyozidi kwenda, ndivyo baba alivyozidi kusahau wajibu wake kuitunza familia. Mzigo wote akamuelemea mama (Uk. 124).

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuhusu jamii kuundwa kwa asasi ambazo zinatekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na haja ya asasi hizi kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kutowajibika kwa Ngoma kunatatiza utekelezaji juku la

ndoa yake la kulea watoto. Kutowajibika kwake kunasawiriwa kupitia kitendo hiki ambacho kimetumika kumsawiri. Kulingana na dondoo hili kitendo cha kutowajibika kwa Ngoma kinaanza na kuendelea taratibu hadi inafikia hatua ya kumwachia Tabu mzigo wote wa malezi. Yeye alikuwa na pato zuri lakini analitumia kwa kushiriki ulevi na uasherati. Mkewe anahangaika kwa biashara ndogo ili kujikimu yeye na watoto ilhali Ngoma ana pato zuri kutokana na biashara yake ya uchukuzi wa abiria. Kitendo hiki kinasimuliwa na mtoto wake Ngoma, hii inaonyesha namna kukosa kwake kuwajibikia malezi kunaathiri watoto wake moja kwa moja. Kutowajibika kwa mmoja wa wanandoa kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu kunamfanya mwenzake kuubeba mzigo wa kulea familia na kufanya watoto kukosa kukidhiwa kwa mahitaji yao ipasavyo.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* kutowajibika kumejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi wa Hasani. Hasani anaijenga changamoto hii kupitia kitendo cha kuacha kumpatia mkewe pesa za matumizi katika ndoa yao na pia kupitia usemi wake Muna anapomuuliza sababu ya kufanya hivi. Muna anapomuuliza anasema :

> Pesa zote unazozipata hizo ! Basi unaona ubahili kutumia hapa nyumbani ? Lakini unafanya kazi nzuri, unapata pesa nzuri zaidi yangu mimi (Uk. 189).

Uhusika wa Hasani kupitia usemi huu unadhihirisha kwamba amekataa maksudi kumsaidia Muna kugharamia mahitaji yao. Sababu anazotoa za kikosa kuchangia hazina msingi. Anakataa kwa sababu Muna anafanya kazi nzuri kumliko na anapata pesa nyingi kumshinda. Hii ni sababu inayotokana na wivu anaomuonea mkewe. Si haki kwa mwanandoa mmoja kukosa kuchangia mahitaji ya ndoa yao kwa sababu mwenzake anapata pesa nyingi.

Changamoto hii imesawiriwa kupitia usawiri kiusemi wa Hasani na Muna katika riwaya ii hii ya *Mwisho wa Kosa*. Usemi wa wahusika hawa unaoisawiri changamoto hii unasimuliwa hivi :

> Lakini unafanya kazi, unapata pesa nzuri zaidi yangu mimi.
> Hiyo siyo sababu, na wewe unajua sijakataa kukusaidia, lakini kila jambo lina mpaka. Au ndiyo maana ukanioa?

Sikiliza mimi sina pesa. Ikiwa huwezi kutumia pesa zako basi, alisema Hasani na kutoka nje. ( Uk. 189)

Kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu utekelezaji wa majukumu na ndoa au wanandoa unatiliwa mkazo ili kufanya ndoa na jamii kuwa thabiti (Talcot, 1951). Usemi kati ya Hasani na Muna ambao umetumika kuwasawiriunatokea kama malumbano kati yao kuhusu kugharamia mahitaji yao. Ilomo (2015) anaieleza mbinu kama mazungumzo baina ya wahusika katika utafiti aliofanya kuhusu mbinu za kujenga wahusika. Malumbano haya yanaonyesha kuwa katika ndoa hii hakuna maelewano kuhusu matumizi yao ya pesa. Kauli ya Hasani inatolewa kwa hasira na inaonyesha nia yake ya kutaka kumnyanyasa Muna. Anakwepa mjadala zaidi kuhusu suala hili, anamtaka Muna aendelee kugharamia matumizi yao wote peke yake. Kulingana na Talcot(1951) mume anafaa kumkimu mkewe na watoto kwa mahitaji yao naye mke anafaa kuwajibikia shughuli za nyumbani na malezi ya watoto. Muna anaona kuwa Hasani anatenda kinyume kwa kumwachia jukumu hili. Swali analouliza Muna linaonyesha toni ya hasira. Anaona kwamba anaonewa na Hasani anapomtaka kugharamia matumizi ya nyumba peke yake. Muna ni mfano wa wanawake ambao wamepata elimu na wanapinga dhuluma kutoka kwa waume kama anavyosema Gicuku (2012). Kauli ya mwisho ya Hasani inaonyesha kuwa hataki kuendelea kujadili suala hili na amekwisha kata kauli kutomsaidia Muna. Dai kwamba hana pesa si la kweli kwa sababu haelezi sababu ya yeye kukosa pesa.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* changamoto hii imesawiriwa kupitia usawiri wa Tabu kiusemi. Usemi wa Tabu ni wa mawazo, tofauti na wa Hasani na Muna ambao ni wa mazungumzo. Anawaza kuhusu namna mumewe hamtunzi wala kuwatunza watoto wao. Yafuatayo ni mawazo ya Tabu yanayoisawiri changamoto hii.

Huyu mume hanipi matunzo wala hawatunzi wanawe. (uk.112)

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unatilia mkazo utekelezaji wa majukumu yaliyotengewa asasi za kijamii bararabara ili kujenga jamii thabiti. Hii ina maana kuwa wanandoa hawana budi kutekeleza majukumu yao barabara ili kuafikia lengo hili. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuhusu usawiri wa wahusika kiusemi. Kauli hii

inaonyesha kukosa kutekeleza kwa majukumu na Ngoma. Mawazo haya ya Tabu yanaonyesha uonevu ambao Tabu ameelekezewa na Ngoma. Amemtwika jukumu la kuwatunza watoto peke yake ilhali hana pato zuri la kuwatunza. Anaonyesha kumchukia mumewe kwa kutowajibikia malezi ya wanao. Keringe (2013) anasema kutowajibika hujitokeza wakati mwanandoa hukosa kusaidiana na mwenzake kutimiza majukumu ya ndoa yao. Hali inayojitokeza ni ya mwanandoa mmoja kutojali mwenzake na watoto. Ngoma anamwachia Tabu jukumu la kuhangaika kufanya biashara ndogo ili kujikimu yeye na watoto huku yeye akitumia pato lake kwa anasa. Kwa mujibu wa mawazo ya Tabu mume ana jukumu la kumtunza mkewe na watoto na hafai kumwachia mkewe jukumu hili. Hii inaona na mtazamo wa misingi ya nadharia ya umuundo-uamilifu.

Matokeo haya yanajadili kutowajibika kama changamoto inayoikumba ndoa na kuifanya ikose uthabiti ambao ni muhimu katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kila mwanandoa anafaa kujitahidi kukimu mahitaji ya ndoa badala ya kutoroka na kumwachia mwenzake kama anavyofanya Jaku katika *Kiu*. Wote wanafaa kujiepusha na ubinafsi kama wa Ngoma wa kutumia pato kwa starehe huku mke na watoto wakiteseka kwa kukosa mahitaji muhimu. Wanandoa wanafaa kuelewana kuhusu kugharamia mahitaji ya ndoa yao na kuzingatia makubaliano yanayoafikiwa ili kuepusha lawama kama inayotokea kati ya Hasani na Muna.

Kutowajibika kumejadiliwa na Nyaosi (2008), Gicuku (2012) na Keringe (2013) katika tafiti zao kuhusu ndoa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha namna uhusika kiusemi na kimatendo umetumika katika riwaya teule kujenga changamoto ya kutowajibika. Uhusika wa kimatendo umetumika katika riwaya ya *Kiu*, *Ua la Faraja* na *Mwisho wa Kosa*. Wahusika wote waliorejelewa katika riwaya hizi wamesawiriwa kwa kitendo cha kukwepa kutunza wake zao pekee au wake zao na watoto. Katika *Ua la Faraja* na *Mwisho wa Kosa* wahusika waliorejelewa wanakataa kimaksudi kuwatunza watu wanaowategemea licha ya kuwa na uwezo wa kifedha. Katika riwaya ya *Kiu* Jaku amejenga kutowajibika kwa kitendo cha kutokomea na kumwachia mkewe jukumu la kumlea Bahati peke yake. Tofauti na Ngoma katika *Ua la Faraja* na Hasani katika *Mwisho wa Kosa* Jaku hakuwa na uwezo wa kifedha wa kuitunza familia kabla ya kutokomea. Kutowajibika kumesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* na riwaya ya *Ua la Faraja*. Usemi uliotumika katika katika *Mwisho wa Kosa* ni wa

kauli ya Hasani na kauli ambazo Hasani na mkewe wanatoa wanapojibizana. Katika *Ua la Faraja* usemi unaomsawiri Tabu na kujenga kutowajibika ni wa mawazo yake kuhusu namna ambavyo ametelekezwa na mumewe. Kutowajibika katika riwaya teuele kumejengwa kuwa uhusika wa kimatendo na kiusemi japo matendo na usemi uliotumika unatofautiana.

### 4.2.6 Ukosefu wa Watoto na Usawiri wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa sasi ambazo hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Asasi hizi zinafaa kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Talcot(1951) anasema kuwa jukumu la ndoa ni kuendeleza kizazi. Ukosefu wa watoto unafanya ndoa ikose kutekeleza jukumu hili ipasavyo. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia maelezo yanatolewa kuhusu namna Changamoto hii imejengwa kupitia uhusika. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani ?* changamoto hii imejengwa kupitia usawiri wa wahusika kimatendo na kiusemi. Changamoto hii imesawiriwa na Kitonga na Mwanamuka kupitia tendo la wao kukaa muda mrefu bila kupata mtoto jambo ambalo linasababisha ugomvi katika ndoa yao. Hiki ni kitendo cha kunuia kama kinavyofafanuliwa na Kenan (1983) na kwa mujibu wa mhimili wa kwanza na wa nadharia ya naratolojia. Wahusika hawa vilevile wanasawiri changamoto hii kupitia usawiri wa kiusemi. Wanafanya hivi kupitia mazungumzo kati yao katika nyumba yao. Mwanamuka anamtembelea daktari kujua sababu ya wao kukosa kupata watoto na anaambiwa kwamba yeye hana shida ila anafaa kufanyiwa uchunguzi zaidi. Mwanamuka anapomwambia Kitonga ujumbe wa daktari na kumshauri aende kuchunguzwa anajibu kwa ukali:

> Upuzi gani? Hujui sina kazi nyingine niliyoifanya kwa mapana kama hiyo kabla hujafika hapa wewe? Unataka ushahidi, basi nami nitakupa. ( Uk. 69 )

Dondoo hili linaonyesha namna changamoto hii inasawiriwa na Kitonga kupitia uhusika wake kiusemi kama unavyofafanuliwa na Kenan (1983) na kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia. Toni inayojitokeza katika kauli hii ni ya hasira na inadhihirishwa na msemaji kupitia maswali anayouliza mwisho wa sentensi ya kwanza na ya pili ya dondoo hili. Ukali wake unadhihirishwa na kauli fupi anazotoa katika sentensi ya mwisho ya dondoo hili. Ukali huu wa ghafla unaonyesha kuwa kitonga amekuwa na fundo moyoni kuhusu kutopata

mtoto haraka anavyotaka. Ukali huu kwa mkewe unaonyesha kwamba katika mawazo yake amekwishachukulia kwamba mkewe ndio sababu ya wao kutopata mtoto haraka. Kauli hii inaonyesha mawazo potovu kwamba iwapo wanandoa wanakaa bila kupata mtoto basi tatizo huwa ni la mke na wala si la mume. Juhudi za Mwanamuka za kutafuta suluhu zinaambulia patupu kwa kuwa Kitonga anaamini kuwa yeye hana kasoro. Kupuuzwa kwa Mwanamuka kunashadidia maoni ya Katola (2006) kuwa mwanamke ananyimwa haki ya kutoa ushauri kuhusu maswala muhimu katika ndoa. Wanandoa wanapokosa kupata mtoto baada ya kuoana lawama haitokei baina yao bali pia kutoka kwa jamaa zao. Lawama hizi hutokea hata bila wao kuthibitisha kiini cha kukosa kupata mtoto. Mwanamuka analaumiwa na shemeji yake Kenzi anapokaa na Kitonga kwa muda bila kupata mtoto, hata anamwambia hafai kuitwa mwanamke kwa kuwa hazai. Matendo anayotendewa Mwanamuka yanashadidia maoni ya Gicuku (2012) kuwa kukosa watoto ni tatizo ambalo katika tamaduni nyingi za kiafrika halivumiliki. Jamaa wa Kitonga hawana subira ya kutafuta suluhu ya kimatibabu. Wanaanza kumsuta na kumkejeli Mwanamuka kwa kukosa kupata mtoto.

Ukosefu wa watoto unasawiriwa na Mwanamuka kupitia usawiri wake kiusemi. Anasawiri kupitia usemi huu:

> Msichana wa kazi hakuwa msichana tena bali mke mwenza na alichotapika hakikutokana na nyama za mjini. ( Uk. 70 )

Kauli hii ya Mwanamuka inadhihirisha kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa mtoto katika ndoa yake na kumfanya akose kutekeleza jukumu la ndoa la kuendeleza kizazi kulingana na Talcot(1951). Kauli hii inaonyesha namna uhusika wa Mwanamuka unaisawiri changamoto hii kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia. Usemi huu unadhihirisha uchungu katika moyo wa msemaji kutokana kuhisi kwamba amesalitiwa na mumewe. Kuwazia msichana wa kazi kuwa mke mwenza kunaonyesha kwamba Kitonga ameshiriki uasherati na msichana huyu jambo linalomuuma. Mwanamuka ametumia jazanda ya kutapika kwa msichana wa kazi katika kauli hii kumaanisha kwamba alikuwa na mimba ya mumewe. Matumizi ya jazanda yanalenga kuficha maana na kufikirisha msomaji na hivyo kuibua mvuto. Kauli hii inaonyesha

athari za kukaa muda kwa ndoa bila kupata mtoto. Imesababisha mumewe kudhania kwamba ndiye chanzo na kushiriki uasherati.

Kwa mujibu wa Karinge (2013) tatizo la ukosefu wa watoto linaweza kuyumbisha ndoa na hatimaye kuivunja. Anasema kuwa watoto walidhaminiwa sana na mtu asipopata mtoto au watoto hudharauliwa. Hii inatokana na jukumu muhimu la asasi hii katika kuendeleza kizazi. Mwanamuka na Kitonga wanaingiwa na wasiwasi baada ya kukaa muda mrefu bila kupata mtoto. Mwanamuka anaanza kulaumiwa na mumewe na jamaa za mumewe. Gichinga (2005) na Nyamete (2016) wanabainisha kukosa watoto kuwa kiini cha mizozo katika ndoa. Ukosefu wa watoto katika ndoa ya Mwanamuka na Kitonga unasababisha mzozo kati yao na kuingiliwa na jamaa za Kitonga. Ndoa kati ya Mwanamuka na Kitonga inavunjika wakati mke huyu anashindwa kuvumilia lawama kutoka kwa mumewe na jamaa zake. Wanandoa wanapokaa kwa muda bila kupata mtoto au kukosa mtoto kabisa hawafai kuanza kulaumiana. Badala yake wanafaa kufanyiwa uchunguzi ili kujua kiini cha tatizo hili na kupata matibabu. Iwapo hawatapata suluhu basi wanafaa kukubaliana na kuendelea kuishi pamoja jambo ambalo litawekezana iwapo ndoa yao imejengwa kwa mapenzi ya dhati na wala si matakwa ya kibinafsi. Jamii, wanandoa na jamaa za wanandoa wanafaa kushughulikia suala la ukosefu wa watoto kwa uangalifu ili kuepusha kuyumbishwa kwa asasi hii.

Kidawa katika riwaya ya *Kiu* ameijenga changamoto hii kupitia usawiri wake kimatendo na kiusemi. Tendo hili ni kukaa na mumewe kwa miaka mitano bila kupata mtoto na hata kufikia hatua ya kukosa matumaini. Mhusika huyu pia ameijenga changamoto hii kupitia mbinu ya usemi iliyotumika kumsawiri. Anaisawiri kupitia mazungumzo na shoga yake anayeitwa Bahati. Anapoulizwa na Bahati ikiwa hajapata mtoto Kidawa anajibu :

> Ah, mwaka wa tano huu hata alama. Hata hiyo Baraka imeondoka.’’ (uk. 69

Usemi huu unaashiria kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa watoto katika ndoa hii. Hii inaifanya ndoa hii kukosa kutekeleza jukumu lake katika jamii kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoasisiwa na Durkheim katika karne ya kumi na tisa. Dondoo hili linaonyesha namna changamoto hii inasawiriwa kiusemi kwa kurejelea mhimili wa

kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia na maoni ya Kenan (1983). Usemi huu unatanguliwa na kihisishi kuonyesha masikitiko ya Kidawa, ametarajia mtoto na imepita miaka mitano bila kupata. Anatumia neno ‘alama’ katika kauli kama fumbo. Alama hapa ni ishara ya kupata mtoto ambayo ni mimba. Kwa kusema kwamba hata hiyo baraka imepotea ina maanisha amekata tamaa. Usemi wa Kidawa unaonyesha umuhimu mkubwa ambao jamii imelipatia suala la wanandoa kupata watoto ili kuiendeleza.

Karinge (2013) na Gicuku (2012) wanajadili changamoto ya ukosefu wa watoto katika tafiti zao japo hawakuchunguza namna changamoto hii imejengwa kupitia uhusika. Utafiti huu umechunguza namna changamoto hii imejengwa kupitia uhusika katika riwaya teule. Changamoto hii imejengwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Kiu* na riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Kitendo ambacho kimetumiwa kusawiri wahusika na kuchangia kuijenga ni wahusika wanandoa kukaa muda mrefu bila kupata mtoto. Aidha katika riwaya hizi zote changamoto hii imejengwa kwa uhusika wa kiusemi. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kitonga anatoa kauli inayoonyesha kuwa anamkasirikia mkewe kwa kuona kuwa yeye ndio kiini cha wao kukosa kupata mtoto. Mkewe naye anatoa kauli ya kuonyesha kuudhika na kitendo Kitonga kumpatia msichana wao wa kazi mimba kwa kuwa yeye hazai. Katika *Kiu* Kidawa anaijenga changamoto hii kupitia kauli yake inayoonyesha ukosefu wa matumaini baada ya kukaa miaka mitano bila kupata mtoto.

### 4.2.7 Magonjwa na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo, Kiusemi, Muonekano wa nje na Kimazingira

Utafiti huu umebainisha magonjwa kama changamoto inayofanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu ya kulea kizazi kipya ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu ( Talcot, 1951). Kwa kuongozwa na mhimili wa naratolojia kuhusu dhana wa wahusika na mbinu za kuwasawiri maelezo yametolewa kuhusu namna changamoto ya magonjwa imejengwa kupitia uhusika. Magonjwa kulingana na matokeo ya utafiti huu yanafanya wanandoa kukosa nguvu ya kufanya kazi ili kujikimu na kuwakimu watoto wao. Katika *Ua la Faraja* changamoto ya magonjwa imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo wa Ngoma na Tabu. Katika riwaya hii ya *Ua la Faraja* imesawiriwa na Ngoma na Tabu kwa kitendo kifuatacho:

> Ngoma alikuwa na kifua kikuu. Aliogopa kuwaambukiza wanawe, akawaruhusu waondoke wakaishi kwa babu yao. Sasa alikuwa kitandani anakohoa na kujutia uhai wake (Uk. 213)

Tabu anasawiri magonjwa kwa kusawiriwa kwa kitendo kinachosimuliwa hivi:

> Alipofika alimkuta Tabu hoi, anahema upesiupesi, huku akitokwa na jasho jingi. Mwili wake haukuwa umedhuriwa mno na maradhi ya UKIMWI kwa kuwa alikuwa anapata chakula bora na kufuata maelekezo ya madaktari (Uk. 333)

Madondoo haya yanahusu matendo ambayo yanayojenga changamoto ya ugonjwa katika ndoa hii. Changamoto hii inaifanya hii ndoa kukosa uthabiti ambao kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa umuundo- uamilifu ni muhimu kwa utekelezaji wa majukumu yake. Wanashindwa kuendelea kutafuta pato la kuwakimu watoto wao. Ngoma anashindwa kuendesha biashara yake ya uchukuzi wa abiria naye Tabu anashindwa kuendesha biashara yake ndogo. Magonjwa haya yamewasilishwa kwa kusawiri hawa wahusika kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia na, ufafanuzi Kenan (1983) kuhusu usawiri wa wahusika kimatendo. Ngoma anaugua kifua kikuu ambao ni ugonjwa nyemelezi unaotokana na kuambukizwa virusi vya ukimwi. Anakohoa huku amelala kitandani na kujutia maisha yake. Tabu anaugua ghafla na anapopimwa baadaye anagunduliwa kuwa anaugua kichomi na kisukari. Maelezo ya msimulizi ya hali ya kupumua upesiupesi na kutokwa kwa jasho yanaibua wasiwasi mkubwa kwa wanaomzunguka Tabu na wasomaji.

Uhusika wa kimatendo umetumika katika *Unaitwa Nani?* kusawiri magonjwa japo magonjwa yanayojengwa ni tofauti na wanaogua Tabu na Ngoma. Changamoto hii imejengwa na Purupesa na Maria kupitia uhusika wao kimatendo. Purupesa anaisawiri kwa kitendo hiki:

> Akaanza kusumbuliwa na uvimbe wa tezi- shahawa, uliogunduliwa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa PSA, na ambao kwa maneno ya daktari ulikuwa umefika ngazi mbaya na " huenda ukaishia kuwa chanzo cha saratani." Akapendekeza alazwe hospitalini na tezi-shahawa yenyewe ikaishia kuondolewa (Uk. 220)

Maria anaisawiri kwa kusawiriwa kwa kitendo hiki:

> Alishindwa kuzuia haja yake ndogo. Kila mara akawa analazimika kwenda haja hata kabla hajafika msalani mkojo wenyewe ulikuwa umetoka. Na si hilo tu. Mwili wake ukawa umemwelemea harufu mbaya ajabu (Uk. 248)

Matendo haya yanaibua changamoto ya magonjwa ambayo inatatiza uthabiti wa ndoa hizi. Hii ni kinyume na unavyosisitiza mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu kuhusu haja ya ndoa kuwa thabiti ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Usawiri wa kimatendo wa Purupesa uhahusisha matendo kama vile kuugua, kupimwa, kulazwa hospitalini na kufanyiwa upasuaji. Anaugua tena na kufanyiwa upasuaji mara ya pili na kufanya afya yake kuathirika zaidi. Anaanza kuugua ugonjwa wa ukosefu wa nguvu za kiume jambo linalofanya mkewe kumtoroka kwa kushindwa kumtosheleza kwa tendo la ndoa. Ugonjwa unaweza kuathiri viungo vya mahusiano baina ya mke na mume na kuathiri mahusiano ya kimwili kati yao (Karinge, 2013). Kuvimba kwa korodani ya Purupesa na kupasuliwa kwake kunafanya ashindwe kumridhisha mkewe kimapenzi na kufanya amtoroke. Hii inaonyesha namna ugonjwa unaweza kusababisha ndoa kuvunjika. Maria anaisawiri changamoto hii kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kutokwa na mkojo ovyo na pia kutokwa na harufu mbaya. Hii inafanya watu kumtoroka. Analazwa katika hospitali na kuondoka baada ya kutibiwa na kupona.

Changamoto ya magonjwa imejengwa kupitia usawiri wa kiusemi wa Tabu na Ngoma katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Usemi wa Tabu unasimuliwa hivi:

> Mwenyewe mbishi! Toka wakati ule wa mwanzo mimi nilimshauri aje apimwe akakataa. Akaanza kunisingizia kwamba, kwa kuwa mimi nilipimwa na kuonekana na virusi, basi eti ni mimi nimemuambukiza (Uk. 248).

Ngoma ameijenga changamoto ya magonjwa kupitia usawiri wake kwa usemi huu:

> "Ninaumwa! Jana na leo ndio kweli nimejisikia naumwa. Kila mahali panauma kama kuna mtu alikuja akanipigapiga kwa virungu. Hicho kichwa ndiyo usiseme tena. Na

> mbavu zimeanza kubana toka leo asubuhi, ndiyo sababu hata kupumua imekuwa shida." (Uk. 274)

Madondoo haya yanaonyesha namna uhusika wa wahusika hawa kiusemi kwa mujibu wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri unajenga changamoto hii. Usemi wa wahusika hawa unadhihirisha kukumbwa kwao na changamoto ya ugonjwa katika ndoa yao. Usemi wa Tabu unaonyesha uchungu alio nao kumhusu mumewe Ngoma. Anamlaumu mumewe kwa kukataa kwenda kupimwa ili ajue ikiwa ana virusi. Uchungu wake unatokana na Ngoma kumsingizia kuwa ni yeye aliyemuambukizwa. Uchungu wake unadhihirishwa na sentensi ya kwanza ya kauli yake ambayo ina alama hisi mwisho. Katika dondoo la pili maneno ya Ngoma yanaonyesha maumivu makubwa ambayo ako nayo. Neno la kwanza la usemi wake limetamkwa kwa hisia za maumivu, limewekwa alama hisi mwisho kuonyesha hisia zinazoambatana na matamshi yake. Amefululiza vitendo ambavyo vinafafanua namna anavyougua.

Changamoto hii imejengwa kupitia usawiri wa wahusika kwa muonekano wa nje. Ngoma katika *Ua la Faraja* ameijenga changamoto hii kwa kusawiriwa kwa muonekano wa nje. Muonekano wake wa nje unasimuliwa hivi:

> Nywele zake zilikuwa zimenyonyoka kama za paka anayeugua ugonjwa wa ngozi. ( uk. 245). Mwili wake ulikuwa umesinyaa na kuwa kama wa mtoto. Kichwa kilikuwa kimekonda na nywele zilinyonyoka na kuacha msitu wa ndevu zisizochanwa. (uk.280)
> Uso ulikuwa umekonda , yaonekana macho tu: meupe na makali. ( Uk.240 )

Usimulizi huu unatupatia taswira ya Ngoma na kuibua changamoto ya magonjwa. Hali hii inaonyesha namna ugonjwa unatatiza uthabiti wa ndoa na kufanya wanandoa kushindwa kutekeleza ipasavyo majukumu yao kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Usawiri wa Ngoma kwa muonekano wa nje kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri unafanikisha usawiri wa changamoto hii. Maelezo kuhusu muonekano huu yanaibua taswira ya kudhoofishwa zaidi kwa mwili wa mhusika huyu kwa ugonjwa wa ukimwi na kuibua hisia za huruma kutoka

kwa msomaji. Muonekano wake umeelezwa kwa kutumia tashibihi na sitiari. Nywele zake zinafananishwa na za paka anayeugua ugonjwa wa ngozi. Hii ina maana zi dhaifu na chache kichwani. Mwili wake unalinganishwa na wa mtoto kumaanisha kuwa umekuwa mdogo sana. Ndevu zake zinaelezwa kuwa msitu kumaanisha ni nyingi na hazijatunzwa kwa kunyolewa. Uso wake umekonda, na kinachoonekana wazi ni macho. Maelezo haya yanaonyesha namna ugonjwa huweza kudhoofisha mwanandoa na kumkosesha nguvu ya kutekeleza majukumu ya ndoa ipasavyo. Muonekano wa nje wa Ngoma unalingana na maelezo ya Kinara ( 2012) kuhusu namna ugonjwa wa ukimwi hufanya miili ya waathiriwa kudhoofika na kukosa nguvu za kuendesha shughuli zao.

Ngoma na Tabu katika riwaya ya *Ua la Faraja* wanaisawiri changamoto hii kupitia usawiri wao kimazingira. Mazingira haya ni ya hospitali hasa wodi ya wagonjwa wa ukimwi wanamolazwa. Ngoma analazwa katika wodi ya wagonjwa wa ukimwi ambao wamekonda, wanakohoa sana na wamejaa vidonda mwilini. Tabu vile vile analazwa katika wodi ya wagonjwa wa ukimwi na anakufa baada ya muda mfupi. Mazingira haya ya hospitali yanasimuliwa hivi:

> Wodi ile ilisifika kuwa na wagonjwa wengi wa UKIMWI. Wengi walikuwa na kifua kikuu na madonda mwilini. Baadhi walikuwa wamerukwa na akili. Wodini mlikuwa na harufu mbaya ambayo ilimfanya Juma kila wakati akunje uso na kutaka kutema mate. ( Uk. 245 )

Mazingira haya yanaibua changamoto ya magonjwa ambayo inafanya wanandoa kukosa afya nzuri ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao barabara kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu na maoni ya Talcot (1951). Dondoo hili linaonyesha namna mazingira haya yanaijenga changamoto hii kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoleza kuhusu dhana ya wahusika na mbinu za kuwasawiri. Mazingira haya yanasawiri ugonjwa kupitia matumizi ya mbinu ya taswira kuyaeleza. Wodi imejaa wagonjwa wengi wa ukimwi wanaogua magonjwa nyemelezi yanayotokana na ukimwi. Kuwepo kwa harufu mbaya kunasisitizwa na kitendo cha Juma kukunja uso na kutaka kutema mate kila wakati. Katika dondoo hili neno ukimwi limeandikwa kwa herufi kubwa ili kumakinisha wasomaji kuhusu aina ya wagonjwa wanaolazwa hapa na kusisitiza kuhusu ugonjwa huu.

Usawiri wa Tabu na Ngoma unaonyesha namna magonjwa hufanya wanandoa kushindwa kutimiza jukumu kuu la ndoa la kulea watoto. Gichinga (2005) anasema kuwa magonjwa huathiri ndoa kwa sababu ya gharama za matibabu na kutatiza shughuli za wanandoa. Gicuku ( 2012 ) anaeleza ugonjwa wa ukimwi kuwa tatizo sugu linaloathiri asasi ya ndoa. Ugonjwa huu husababisha vifo na watoto kuachwa bila wazazi. Ugonjwa huu unamdhoofisha Ngoma na kufanya ashindwe kuendesha biashara yake na hatimaye kufa. Anamwachia mwanawe jukumu la kwendesha biashara hii ili kuwatunza wadogo wake. Baadaye wote wanaaga dunia na kuwaacha watoto wao yatima. Wanandoa wanafaa kujiepusha na mienendo ambayo inaweza kufanya waambukizwe magonjwa ya kama ukimwi ambayo huathiri afya yao na kufanya washindwe kutekeleza majukumu yao.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha namna magonjwa huathiri afya ya wanandoa na kuwafanya washindwe kutekeleza ipasavyo jukumu la kulea watoto. Aidha yanaathiri mahusianao kati ya mke na mume na kufanya watengane kama wafanyavyo Purupesa na mkewe.

Gicuku (2012), Kinara (2012) na Karinge (2013) wanajadili tatizo la magonjwa katika tafiti zao kuhusu ndoa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha jinsi changamoto ya magonjwa imejengwa kupitia uhusika katika riwaya zilizoteuliwa. Katika *Ua la Faraja* changamoto ya magonjwa imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo, usemi, muonekano wa nje na mazingira wa Tabu na Ngoma. Katika riwaya hii Tabu na Ngoma wanaijenga changamoto hii kwa kitendo cha kuugua ugonjwa wa ukimwi. Tabu ameijenga kupitia usemi ambao ni kauli anayotoa kukiri kuwa alikuwa na ukimwi. Ngoma anasawiriwa kwa usemi ambapo analalamikia maumivu anayopata anapougua. Ngoma inaijenga changamoto hii kwa kusawiriwa kwa muonekano wa nje, muonekano huu ni mwili wake ambao umedhoofishwa mno na ukimwi. Tabu na Ngoma wanaijenga changamoto hii kupitia mazingira ya wodi ya wagonjwa wa ukimwi ambamo wamelazwa baada ya kuzidiwa na ugonjwa. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*changamoto hii imesawiriwa kwa uhusika wa kimatendo peke yake wa Purupesa na Maria. Purupesa inaijenga kupitia uhusika wake kwa kitendo cha kuugua tezi- shahawa, kulazwa hospitalini kiungo hiki kuondolewa. Maria anaijenga changamoto hii kupitia kusawiriwa kwa kitendo cha kuugua

ugonjwa wa kushindwa kudhibiti haja ndogo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha namna tatizo hili kama changamoto ya ndoa linasawiriwa na wahusika kupitia usawiri wao.

### 4.2.8 Kifo na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo

Utafiti huu umebaini kuwa kifo kinafanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kulea watoto barabara. Hii ni kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaoeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na asasi hizi hazina budi kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu haya barabara. Kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri maelezo yanatolewa kuhusu namna kifo kimejengwa kupitia uhusika. Changamoto hii imejengwa na wahusika katika riwaya teule kwa kusawiriwa kwa kitendo cha kukata kamba. Omar na Kibibi katika riwaya *Maisha Kitendawili* wanasawiri kifo kupitia usawiri wao kwa kitendo cha kuaga dunia mmoja baada ya mwingine. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Alipoamka kesho yake, alimpata Mzee Omar kaganda, macho yamemtoka pima nzima, mkojo umejaa katika suruali pamoja na ngama. “ Kwa nini?” alijiuliza. Ujane ulimkodolea macho hakujua afanye nini ila kulia ovyo (Uk. 39)

Kitendo hiki kinaibua kifo kama changamoto inayoifanya asasi ya ndoa kukosa uthabiti na kutatizika katika utekelezaji wa majukumu yake jinsi inavyosisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Kitendo hiki kinatokana na usawiri wa Mzee Omar kimatendo kama anavyofafanua Kenan(1983) na kulingana na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia. Kitendo hiki kinaibua hisia za huzuni kutokana na taswira inayotokana na maelezo ya msimulizi kuhusu hali ya maiti ya kujiendea haja ndogo na macho kumtoka pima. Kushutusha kwa kitendo hiki kunadhihirishwa na kunukuliwa kwa swali la moja kwa moja na Kibibi akishangaa kuhusu kifo cha mumewe. Anashangaa kwa sababu memewe alikuwa amepata nafuu baada ya kutibiwa na mganga. Msimulizi ameeleza kitendo hiki cha kifo kwa njia isiyo ya moja kwa moja, amehuisha ujane kwa kusema unamkodolea Kibibi macho kumaanisha mumewe amekufa. Omar anaaga dunia baada ya kuugua ugonjwa wa pumu kwa muda mrefu. Ameugua ugonjwa huu tangu utotoni na alizidiwa sana wakati wa mvua na kipupwe.

Changamoto hii inasawiriwa na Kibibi, mke wa Mzee Omar kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kufa baada ya saa tisa za kuomboleza kifo cha mumewe. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Baada ya masaa tisa ya kuomboleza Kibibi alizidiwa na nguvu. Mwili wake ulimyong'onyea na kungwi aliyepewa kazi ya kumwangalia mpaka kifo cha mumewe na matanga yeshe akatangazia watu kuwa hata kibibi naye alikuwa kafa (Uk. 40)

Usimulizi huu unahusu kitendo cha kufa kwa Kibibi kinachosawiri changamoto hii ya kifo. Kifo hiki kinaitia kikomo ndoa hii na kutamatisha utekelezaji wa majukumu ya ndoa ya kulea kizazi kipya kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu usawiri wa wahusika, usawiri kimatendo wa Kibibi unafanikisha usawiri wa changamoto hii. Kitendo hiki kinashtusha jamaa na jamii ya Kibibi kwa kuwa kinatokea muda mfupi baada ya kifo mumewe. Tofauti na kifo cha Mzee Omar ambacho inajulikana kuwa kilisababishwa na ugonjwa wa pumu, sababu ya kifo hiki haijulikani. Inakisiwa kuwa kilisababishwa na kihoro cha kufiwa na mumewe au mpango wa Mungu kuwa wafe siku moja.

Changamoto hii pia imesawiriwa kwa usawiri wa Ngoma na Tabu kimatendo katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Omolo alipata taarifa za Kifo cha Ngoma saa kumi alasiri. Alikuwa anajiandaa kwenda hospitali kumuona mgonjwa, ndipo Grace alipompigia simu, " Boss usije tena hospitalini. Mgonjwa ameshafariki (Uk. 293)

Tabu anasawiri kifo kupitia kitendo cha kukata kamba baada ya kuugua magonjwa nyemelezi kwa sababu ya kuambukizwa ukimwi. Tofauti na vitendo vilivyosimuliwa hapo juu ambapo wahusika wanapatikana wamekufa au vifo vyao kuripotiwa baadaye, kitendo hiki kinasimuliwa kinapotokea. Kinasiumuliwa hivi:

> Alikuwa bado amefumba macho na midomo, lakini ametabasamu. Mwili wake ukaonyesha mishtuko mikubwa mara mbili, kisha ukatulia. Alikuwa bado anatabasamu lakini hakutingishika tena. Wale manesi wawili wakaenda kuchukua shuka na kumfunika huku wakisema, " Ameshafariki." (Uk. 338)

Madondoo haya yanaonyesha uhusika wa kimatendo wa Tabu na Ngoma ambao unajenga changamoto ya kifo. Maelezo kuhusu namna uhusika wa kimatendo unajenga changamoto hii yameongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri kwa mujibu wa Kenan (1983). Wanajenga kifo kupitia kitendo cha kufa. Tabu na Ngoma wanakufa kutokana na ugonjwa wa ukimwi, kufa kwao hakutokei siku moja kama kufa kwa Mzee Omar na mkewe. Kifo cha Ngoma kinaripotiwa na Grace baada ya kupata mwili wa Ngoma umekwishapelekwa kwa mochari. Usimulizi wa kitendo hiki unahusisha sauti ya moja kwa moja ya Grace kupitia kwa simu. Kitendo cha kufa kwa Tabu kinasimuliwa jinsi kinavyotokea. Kauli ya manesi kuonyesha kukamilika kwa kitendo hiki imenukuliwa. Kitendo hiki kinaonyesha kinaya kwa kusimuliwa kwamba Tabu anatabasamu anapofariki. Kifo cha wanandoa waliotajwa kimawaacha watoto wao yatima na kufanya malezi yao kutatizika.

Changamoto ya kifo katika ndoa imejadiliwa katika tafiti kuhusu ndoa na tafiti ambazo hazihusu ndoa. Kinara (2012) anaeleza shida ambayo huwapata watoto baada ya kufiwa na wazazi anapojadili maudhui ya ukimwi katika *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*. Wao hukosa mlezi na hulazimika kukatiza masomo ili kujitafutia riziki. Gicuku (2012) anaeleza namna vifo kutokana na ugonjwa wa ukimwi vinawaacha watoto bila walezi. Anasema baadhi ya watoto hutoroka nyumbani, huingilia matumizi ya dawa za kulevya na kufanya ukahaba ili kujikimu. Keringe (2013) anaeleza namna watoto hubakia yatima na kuteseka baada ya wazazi kufa. Wataalamu hawa wameeleza namna kifo hutatiza jukumu la ndoa la kulea watoto kulingana na nadharia ya umuundo- uamilifu inayoeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Utafiti huu umeeleza namna changamoto ya kifo imejengwa kupitia uhusika kwa kurejelea riwaya teule za Kiswahili. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na riwaya ya *Ua la Faraja* kifo kimejengwa kwa uhusika wa kimatendo. Katika *Maisha Kitendawili* uhusika kimatendo umefanywa kwa mwanandoa kufa kisha mwingine anafuatia saa tisa baada ya kuomboleza kifo cha mwenzake. Katika *Ua la Faraja* kifo kimejengwa kwa kusawiriwa kwa

Tabu na Ngoma kupitia kitendo cha kufa kwa ugonjwa wa ukimwi. Ngoma ndiye anakufa kwanza kisha anafuatwa na mkewe Tabu. Kitendo cha kufa kwa Ngoma kinatokea na kuripotiwa baadaye. Kufa kwa Tabu kunasimuliwa jinsi kunavyotokea. Ni dhahiri kuwa kifo katika riwaya hizi mbili kimejengwa kwa uhusika wa kimatendo. Kitendo chenyewe ni kufa kwa wanandoa. Hata hivyo vyanzo vya vifo vya wahusika wanandoa vinatofautiana. Aidha jinsi vifo vyenyewe vinavyotokea inatofautiana katika riwaya hizi.

### 4.2.9 Kushikilia kwa Utamaduni Hasi na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Utafiti huu umegundua kuwa ushikilizi wa utamaduni hasi unafanya ndoa ishindwe kutekeleza majukumu ya kulea watoto ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi ambazo zinatekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na uthabiti wa asasi hizi ni muhimu katika kuziwezesha asasi hizi kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu dhana ya wahusika na uhusika, utafiti huu unaeleza namna changamoto hii imejengwa kupitia uhusika. Changamoto hii imejengwa na wahusika ambao wanashikilia utamaduni unaotatiza uthabiti wa ndoa na kuifanya ishindwe kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Changamoto hii imejengwa na Kamende kwa kusawiriwa kimatendo katika riwaya ya *Unaitwa Nani ?* Kitendo hiki kinasimuliwa hivi :

> Kamende aliyedhani kuwa atampata mvulana wa kuongeza kikoa chake akachukia mchezo aliochezewa na maumbile. Mama akampokea mtoto wake aliyejaliwa na Muumba wake baada ya kukabidhiwa na wakunga waliomzalisha. Kwa kuona jinsi babake na ulimwengu wenyewe ulivyompokea mwanawe, akaamua kumpa jina Kamene ( babake ambaye kitamaduni ndiye aliyepaswa kupendekeza jina lake hakujali anaitwa nani). (Uk. 90)

Mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu unaeleza kuwa jamii ni mfumo ambao umeundwa kwa asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Mhimili huu unaeleza haja ya asasi hizi kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Kwa kuzingatia mhimili huu utafiti huu umebainisha ushikilizi wa utamaduni wa kupendelea watoto wa kiume kama

inavyodhihirika katika dondoo hili kuwa changamoto inayotatiza jukumu la ndoa la kulea watoto. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuhusu dhana ya wahusika na mbinu za kuwasawiri maelezo yanatolewa kuhusu namna changamoto hii imejengwa kupitia uhusika wa Kamende kimatendo. Uhusika wa Kamende kupitia kitendo ambacho kinasimuliwa katika dondoo hiliunaonyesha ushikilizi wa utamaduni hasi wa kupendelea watoto wa kiume. Matendo ya Kamende yanaonyesha kujawa na chuki na hata kufikia kiwango cha kulaumu maumbile kwa kupata mtoto msichana badala ya mvulana aliyetarajia. Katika dondoo hili ulimwengu umehuishwa na kutazamwa na mkewe Kamende kama wenye kuonea mtoto huyu kwa kutompokea vyema. Matendo ya mama huyu baada ya mumewe kumbagua mtoto yanaonyesha unyonge alionao. Kamende anakwepa jukumu la kupendekeza jina la kuitwa mtoto huyu. Hii inatokana na kukasirika kwa kupata msichana badala ya mvulana. Usawiri wa Kamende kwa kitendo hiki unashadidia maoni ya Wamitila (2002) kuwa ndoa inampendelea mume na kumkandamiza mke kwa sababu ya mila na desturi zinazoijenga. Mila na desturi zinazompendelea mume zinamfanya Kamende kumchukia mtoto wake msichana mara tu anapozaliwa. Wanandoa hawana budi kutupilia mbali utamaduni unaopendelea jinsia moja na kuinyima haki jinsia nyingine.

Changamoto hii pia imejengwa na Kamende kupitia usawiri wake kimatendo. Kitendo anahoshiriki ni ushikilizi wa utamaduni wa ndoa za mapema na za lazima. Kitendo anachosawiriwa kwacho ni kumuoza Kamene kwa lazima wakati angali na umri mdogo. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi :

> Kumbe alikuwa tayari amekwisha kusikilizana na mzee mwenzake, huko kwenye vigenge vyao vya kunywa dengelua kijijini, kumwoza Kamene kwa mwanawe. Habari yenyewe ikawa imehifadhiwa kama siri kubwa (Uk. 90)

Dondoo hili linaonyesha namna uhusika wa kimatendo wa Kamende unajenga kushikilia kwa utamaduni wa ndoa za mapema na za lazima katika ndoa hii. Hii inatatiza utekelezaji wa majukumu ya ndoa ya kuzaa na kulea jinsi yanavyoelezwa na Talcot (1951). Kitendo hiki ni cha kutendwa na mhusika kama anavyoeleza Kenan (1983). Kitendo hiki kinapangwa kisiri na Kamende kwenye shughuli yao ya unywaji pombe kijijini. Kimechochewa na utamaduni ambao

unamthamini mtoto wa kiume na kumuona wa kike kuwa mwenye thamani ya chini. Anakatiza masomo ya Kamene na kumuoza angali na umri mdogo ili kujipatia mahari. Nakhumicha (2013) anasema kuwa wanaume na wanawake wanahitaji elimu ili kuwapatia uwezo wa kuboresha familia zao. Kwa kukosa elimu ya juu watoto kama hawa hukosa maarifa ya kuajiriwa au kujiajiri ili kujikimu maishani. Mwanandoa hafai kumlaumu mwenzake baada ya mtoto wa jinsia asiyotarajia kuzaliwa. Wanandoa wanafaa kukubali jinsia ya watoto wao na kuwatendea haki wanapowalea.

Changamoto hii imejengwa kupitia uhusika wa wazazi wa Kaseli Nzeli katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Mamake Kaseli Nzeli anaisawiri kupitia usawiri wake kimatendo na kiusemi. Anaisawiri kupitia usawiri wake kwa kitendo na usemi wa kumshihinikiza bintiye kushiriki ukeketaji:

> "Siku ulipozaliwa nilijua yatanifika haya!"
> " Lakini mama nimefanya nini?"
> " Hujui umefanya nini?"
> " Hukukataa kupashwa tohara?"
> " Sikukataa, ngariba wenyewe walitimua mbio" Nilichofanya nikucheka tu!" (Uk. 113-114)

Kauli za wahusika hawa na kitendo chao kinathibitisha kuwepo kwa changamoto ya kushikilia utamaduni hasi wa kukeketa wasichana. Ushikilizi wa utamaduni huu unatatiza ndoa hii katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuhusu mfumo wa jamii ambao ni wa asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Dondoo hili linaonyesha namna uhusika wa kimatendo kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaijenga changamoto hii. Mhimili huu unaeleza kuhusu dhana ya wahusika na mbinu za kuwasawiri. Usemi huu unatolewa kwa hisia za hasira kutokana na shughuli ya kumkeketa Kaseli Nzeli kufeli. Hisia za hasira za mama huyu zinadhihirishwa na matumizi ya vihisishi na mfululizo wa maswali. Anamlaumu bintiye ilhali yeye alikubali na kushirikiana na ngariba lakini wao wakashindwa kumkeketa na kutoroka. Hakujatolewa sababu ya ngariba hawa kushindwa kutekeleza shughuli hii. Ushikilizi wa

utamaduni huu unaathiri jukumu kuu la ndoa la kulea watoto. Akipinga utamaduni huu Nakhumicha (2013) anasema kuwa suala la kukeketa wasichana ni tatizo la kiafya, la haki za kibinadamu na ni njia ya kumdhalilisha mwanamke. Haki za Kazeli Nzeli zinakiukwa kwa kulazimishwa kushiriki kitendo hiki na masomo yake kutatizwa. Kaseli Nzeli anatatizika kimasomo baada ya mamake kutoroka naye kutoka kwao na kuenda kuishi kwa babu yake. Utamaduni huu unahusishwa na ndoa za mapema jambo ambalo pia hutatiza masomo ya mtoto msichana na kuathiri afya yake.

Changamoto hii imesawiriwa na Lusweti katika riwaya ya *Unaitwa Nani ?* Kupitia usawiri wake kimatendo. Kitendo kinachitumiwa kumsawiri nikukwepa kumsaidia mkewe kazi za nyumba na kukaa sebuleni kutaka kuhudumiwa. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Hakutaka kusikia habari za operesheni au nini. Alichotaka ni kuhudumiwa kama mwinyi amekaa, kwenye kochi lake alilozoea, linalotazamana na mlango wa chumba, huku mguu mmoja kauweka juu ya mwingine kashika kifaa cha kuwashia runinga. (Uk. 102)

> Kila Kamene alipomuuliza kwa nini alipotea, akamuacha kwenye upweke, akaruka juu kama mtu aliyekalia msumari kwa kusema kuwa katika maisha yake hajasikia " mwanamume kuulizwa alikuwa wapi." Hata mamake ( ' ah mamake tena') hakuwahi kumwuliza babake anatoka wapi. ( Uk. 97)

Dondoo hili linaonyesha namna ambavyo uhusika wa kimatendo wa Lusweti unajenga huu utamaduni hasi wa mume kumchukulia mke kama mtumwa wa kumhudumia. Dhana ya uhusika wa kimatendo inatokana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Kushikilia utamaduni huu kunaifanya ndoa hii kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuhusu asasi za kijamii ambazo zinaunda mfumo wa jamii na hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Lusweti anaijenga changamoto hii kupitia kusawiriwa kwa kitendo cha kukaa sebuleni huku mkewe akihangaika kufanya kazi za nyumba. Kitendo hiki kimeelezwa kwa kutumia mbinu ya taswira na kutuchorea picha ya akili ya mume anayestarehe huku mkewe akihangaika kumpikia na kulea mtoto.

Kitendo chake kinalinganishwa na mtu ambaye ni mwinyi kwa kuwa anastarehe huku mke wake akihangaika naye anasubiri tu kuletewa chakula mezani. Hamsaidii mkewe aliyejifungua siku chache zilizopita kufanya kazi za nyumba au kulea mtoto na anafahamu hana msichana wa kazi. Anapofika nyumbani baada ya shughuli za mchana anakaa sebuleni huku mkewe aking'ang'ana kumlea mtoto na kumwandalia chakula. Anapochelewa kumletea chakula anamzaba kofi. Nyamete (2016) anasema kuwa kushikilia desturi zilizoitwa na wakati husababisha mizozo katika ndoa. Ndoa ya Lusweti na Kamene inakabiliwa na mzozo kwa sababu ya Lusweti kuamini kazi anayofanya mkewe ni ya jinsia ya kike na anafaa kumhudumia licha ya changamoto anazopitia.

Changamoto hii pia imesawiriwa na Lusweti kupitia kitendo na usemi wake katika dondoo la pili. Usemi wa Lusweti unatolewa kila mara anapoulizwa na mkewe kuhusu mienendo yake. Namna anavyojibu kunalinganishwa na mtu anavyofanya anapokalia msumari. Hii inaonyesha mshtuko au mshangao kutokana na imani yake ya kiutamaduni kwamba mke hafai kuuliza kuhusu mienendo ya mume. Anamrejelea mamake kama mfano kwa sababu amethibiti maisha yake hadi sasa. Usemi wa Lusweti unashadidia maoni ya Wamitila (2002) kuwa ndoa inampendelea mume na kumkandamiza mke kwa sababu ya mila na desturi zinazoijenga. Kauli ya Lusweti inaonyesha kuwa mume amepewa mamlaka makubwa sana katika ndoa. Yeye ana uhuru wa kuondoka na kurudi atakapo na mke hafai kumuuliza kuhusu matendo haya. Imani hii ni potovu kwa kuwa wanandoa ni washirika sawa katika ndoa na kila mmoja anafaa kumjali mwenzake. Kwa sababu hii hakuna makosa kwa mwanandoa kumuuliza mwenzake kuhusu mienendo yake. Kukerwa kwa Lusweti anapoulizwa kunatokana na utamaduni ambao unampa mume hadhi ya juu na mwanamke hadhi ya chini katika jamii.

Suala la kushikilia utamaduni hasi limejadiliwa na wataalamu wa fasihi na wa taaluma nyinginezo. Wamitila (2002) anasema kuwa ndoa imetawaliwa na utamaduni ambao unamkandamiza mke. Nakhumicha (2013) anajadili kuhusu utamaduni wa ukeketaji na athari zake. Utafiti huu umebainisha ushikilizi wa utamaduni hasi kuwa changamoto ambayo inafanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha jinsi changamoto hii imejengwa kupitia uhusika katika riwaya teule. Changamoto hii imejengwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi.

Kushikilia utamaduni wa kumpendelea mtoto wa kiume kumejengwa kupitia uhusika wa kimatendo wa Kamende. Anaujenga kupitia kitendo cha kumbagua mtoto wake wa kike na kukataa kumpa jina mara tu anpozaliwa. Anaujenga utamaduni wa ndoa za mapema na za lazima kupitia uhusika wake kimatendo. Kitendo ambacho kinamsawiri na kujenga utamaduni huu ni kumuoza binti yake akiwa na umri mdogo. Mamake Kaseli Nzeli anaujenga utamaduni wa ukeketaji wa wasichana kupitia uhusika wake kiusemi na kimatendo. Anaujenga kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kumshinikiza bintiye kushiriki ukeketaji. Aidha anaujenga kupitia usawiri wake kwa usemi wa kumgombeza bintiye kwa kukosa kukeketwa hata baada ya kushiriki shughuli hii na ngariba kushindwa kumkeketa. Lusweti anaujenga utamaduni wa mume kumchukulia mke kama mtumwa wa kumhudumia kupitia uhusika wa kimatendo. Anafanya hivi kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kustarehe sebuleni huku mkewe akihangaika kupika na kulea mtoto. Lusweti pia anaujenga utamaduni wa kutomtaka mke kufuatilia mienendo ya mumewe kupitia uhusika wake kimatendo na kiusemi. Anafanya hivi kupitia kitendo na usemi ambao umetumika kumsawiri. Anaruka juu na kusema hajawahi kumsikia mamake akiuliza babake kuhusu mienendo yake. Hii ni baada ya mkewe kumuuliza sababu ya kuadimika nyumbani na kumuacha na upweke.

### 4.2.10 Ugomvi na Usawiri Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Utafiti huu umebaini kuwa ugomvi ni changamoto ambayo hufanya ndoa kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza jukumu la kijamii la kulea watoto ipasavyo. Kubainishwa kwa changamoto hii kumefanywa kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi ambazo hutekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na asasi hizi hazina budi kuwa thabiti ili ziweze kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri maelezo yanatolewa kuhusu namna ugomvi umejengwa kupitia uhusika. Ugomvi umesawiriwa na wahusika wanandoa wanaorushiana maneno makali, kuzua vurugu na hata kupigana. Ugomvi unasawiriwa na Tabu na Ngoma katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia usawiri wao kiusemi na kimatendo kwa pamoja. Matendo na usemi ambao umetumika kuwasawiri unasimuliwa hivi:

> Ngoma akaenda kumshika bega kutaka kumtuliza. Akazabwa kofi, akaachia. "Nimesema usiniguse!" Tabu alimwambia kwa hasira (Uk. 28)

Kitendo na usemi huu unaibua ugomvi unaofanya ndoa hii kukosa uthabiti ambao unasisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Ugomvi huu unasababisha ukosefu wa utulivu kati ya wanandoa hawa. Dondoo hili linaonyesha namna changamoto hii inasawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi kama unavyofafanuliwa na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia. Kitendo hiki ni cha kutenda na kinatendeka mara moja kwa mujibu wa Kenan (1983). Ngoma anamtuliza Tabu kwa kumshika bega lakini anamzaba kofi. Hii inatokana na hasira nyingi alizo nazo kwa kuwa Ngoma alikuwa amemwambukiza ukimwi. Kauli yake inamhusu yeye na wala si mhusika mwingine. Katika dondoo hili usemi wa moja kwa moja wa Tabu unanukuliwa na kuhitimishwa kwa alama hisi. Hii inaonyesha hisia za hasira alizonazo.

Ngoma na Tabu wanaisawiri changamoto hii kupitia usawiri wao kiusemi. Usemi wao unasimuliwa hivi:

> Sikugusi Ma' Juma.
> Nataka tujadiliane.
> Tujadiliane nini? Umeniua halafu wataka tujadiliane! Nani kakwambia una ukimwi? Ngoma aliuliza kwa sauti ya kubembeleza. Ulevi wote umekwishamtoka. ( Uk. 27 )
>
> Kila siku nimekuonya : Acha! Acha! Hukunisikia, kila , ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike ulioukuta. Sasa umeniletea ugonjwa. Eti tujadiliane na mtu ambaye hata sasa ananuka harufu za uasherati…!(uk. 27)

Kauli hizi zinaonyesha jinsi uhusika wa kiusemi wa wahusika hawa unajenga ugomvi katika ndoa hii na kuikosesha uthabiti ambao ni muhimum kwa utendakazi wake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuhusu mfumo wa jamii ambao ni asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha. Unaeleza kuwa uthabiti wa asasi hizi ni muhimu ili kuziwezesha kutekeleza majukumu haya ipasavyo.

Changamoto hii inasawiriwa kwa uhusika wa kiusemi wa wahusika hawa kwa mujibu wa mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia. Usemi huu ni wa majibizano kati ya wahusika hawa. Katika usemi huu Tabu anamgombeza Ngoma kwa hasira kwa kupuuza maonyo yake na kuendelea kushiriki uasherati na hatimaye kumuambukiza ukimwi. Katika kauli hii neno 'acha' limerudiwa kuonyesha jinsi alivyomsisitizia Ngoma kuacha uasherati. Neno hili litamkwa kwa hisia za hasira jambo linalothibitishwa na matumizi ya alama hisi mwisho mwa neno hili. Katika usemi wake Tabu anafananisha matendo ya Ngoma yaliyokithiri ya uasherati na kuvamia mizoga ya kike kwa kujiona rijali. Hii inamaanisha alishiriki uasherati hata na wale ambao walikisiwa kwamba wana ukimwi ambao hauna tiba.

Ngoma na Tabu wanasawiriwa kwa usemi unaohusisha majibizano kati yao na kujenga ugomvi kupita majibizano haya. Majibizano haya yanasababishwa na kutoroka nyumbani kwa mwanao anayeitwa Juma. Majibizano haya yanasimuliwa hivi:

> Na wewe kazi vitunguu na genge, genge na vitunguu, mwanao aka! We' huna habari, kama vile hayakuhusu. "Au pengine lenu moja? Umemshauri atoroke?
>
> Tafadhali wewe bwana usin'usinihusishe na mashauri yako na mwanao. Wewe mwenyewe jana ulimgombeza mtoto, ukataka kumpiga. Sasa amekimbia wanigeukia mimi… (uk.129)

Dondoo hili linaonyesha namna ugomvi umesawiriwa na Tabu na Ngoma kupitia uhusika wao kiusemi. Maelezo kuhusu namna ugomvi umejengwa kupitia uhusika yameongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Usemi wa wahusika hawa unaonyesha jinsi ugomvi unaikosesha ndoa hii utulivu ambao ni muhimu katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Nadharia ya umuundo- uamilifu husisitiza haja ya asasi za kijamii kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Usemi huu unahusisha mazungumzo baina ya wahusika hawa wawili. Ngoma anazungumza kwa hasira anapoanza kumgombeza mkewe. Anarudia neno 'genge' na 'vitunguu' kusisitiza kwamba Tabu amezingatia biashara na kupuuza kutoweka kwa mwanao. Anaonyesha hasira zake kwa kihisishi aka! Usemi wake una maswali mawili ambayo anayatumia kumwelekezea mkewe lawama. Kauli ya Tabu ni

ya kujitoa lawamani, anamwona Ngoma kama mwenye makosa na hafai kimlaumu. Jibu lake ni la ukali na la kumwonya mumewe asimlaumu. Matamshi ya Ngoma yanaonyesha hasira anayomwelekezea mkewe kuhusu kupotea kwa mwanao Juma. Marudio ya maneno vitunguu na genge na kuhitimisha kwa sentensi ya kwanza katika dondoo hili kunadhihirisha fundo la hasira alilonalo moyoni. Kurudia maneno haya kunaonyesha anachukizwa na hatua ya Tabu kujishughulisha na biashara hii badala ya kuhangaikia kutoweka kwa Juma. Maswali anayofuatisha yanaonyesha hasira na lawama yake kwa Tabu. Majibu ya Tabu yanaonyesha chuki aliyonayo kwa mumewe kwa kumtelekeza hapo awali na watoto na sasa kujifanya anawajibikia malezi yao na kuwatatiza. kuendelea na shughuli zake bila kuwa na wasiwasi kuhusu alikotorokea. Anajua mahali yupo na hataki kumfahamisha Ngoma kwa sababu ya kumtelekeza na kumwambukiza ukimwi. Kauli ya Tabu inaonyesha mgawanyiko katika familia. Ni wazi kwamba anampendelea Juma na anaona kwamba babake anamdhulumu. Wanandoa wanafaa kuwa na uwazi katika mahusiano yao na kushauriana kuhusu masuala yanayowakabili badala ya kulaumiana. Kulaumiana huzidisha uhasama na hakutoi suluhu kwa shida inayowakabili.

Tabu na Ngoma pia wanajenga changamoto ya ugomvi kupitia usawiri wao kiusemi. Wanasawiriwa kwa majibizano katika nyumba yao usiku baada ya Ngoma kuwasili nyumbani. Majibizano haya yanasimuliwa hivi :

> Mimi kesho nasafiri
>
> Unasafiri ? Mbona hatujapanga ?
>
> Bwana, leo sitaki tugombane. Kesho nakuachia nyumba yako na watoto wako, mimi naondoka.“Kwenda wapi?” “Hiyo siyo kazi yako kujua (uk. 25)

Usimulizi huu unadhihirisha kuwepo kwa changamoto ya ugomvi katika ndoa hii ya Tabu na Ngoma. Hii inatatiza jukumu la ndoa la kulea watoto kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoasisiwa na Durkheim katika karne ya kumi na tisa. Mhimili huu unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi za kijamii ambazo zinafaa kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu yake ya kijamii barabara. Dondoo hili linaonyesha namna changamoto hii inasawiriwa na wahusika kupitia usawiri wao kiusemi kwa kurejelea mhimili wa kwanza

wanadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Majibizano haya yanatokea baada ya Ngoma kufika nyumbani usiku na kumkuta Tabu amefunga virago tayari kuondoka keshoye. Majibizano haya yanahusisha matumizi ya maswali na kauli fupifupi. Maswali anayouliza Ngoma yanaonyesha kushangazwa na safari ya ghafla ambayo Tabu amepanga bila kumuarifu. Kauli fupi za Tabu zinaonyesha hayuko tayari kumuelezea mumewe kiini cha safari yake ya ghafla. Kauli yake ya mwisho ni ya kumpuuzilia mbali ngoma na inadhihrisha hasira alizo nazo.

Hasani na Muna katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* wanachangia ujenzi wa changamoto ya ugomvi katika ndoa kupitia usawiri wao kimatendo. Kitendo hiki kinasimuliwa kama ifuatavyo:

> Ala ! Na kwa mara ya kwanza Hasani alinyanyua mkono na kumpiga Muna kofi kali la uso. Badala ya kushindana, Muna alifunga mdomo na kujitupa juu ya kiti, akiwa amepigwa na mshangao, lakini Hasani alipojaribu kumsogea tena, alinyanyuka na kuanza kupigana naye…Hasani alizidi kuona kuwa kupiga ndiyo njia nyepesi ya kushinda katika mabishano yake na mkewe, kwa hivyo aliichukua njia hiyo kila mara. (Uk. 224).

Kitendo hiki kinathibitisha kuwepo kwa changamoto ya ugomvi katika ndoa hii. Hii inatatiza uthabiti na utendakazi wa ndoa hii kama inavyosisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Dondoo hili linaonyesha namna uhusika wa kimatendo kama unavyofafanuliwa na Kenan (1983) unaisawiri changamoto hii. Kitendo hiki kinashtusha kutokana na matumizi ya kihisishi 'Ala !' mwanzoni mwa dondoo hili. Kitendo hiki kinatendwa na wahusika wote wawili. Kitendo hiki kinaanza na kutendeka kila mara Hasani anaposhindwa kuendelea kujibizana na Muna. Muna anaanza kupigana na Hasani anapomsogea kuendelea kumpiga. Katola (2006) japo hahakiki ndoa, anasema kuwa kupigwa ni mojawapo ya dhuluma kwa wanawake walio katika ndoa. Hii inatokana na ubabedume ambao unaendelezwa na utamaduni unaompatia mwanamume uwezo mkubwa. Hasani anampiga Muna kwa sababu ya kutaka kumdhibiti. Matendo ya Hasani yanashadidia maoni ya Zastro (2008) kuhusu wanaume kuwapiga na kuwatisha wanawake. Anasema kuwa wanaume hufanya hivi ili kuwadhibiti wanawake. Hii inatokana na imani ya kitamaduni kuwa waume wana haki ya kudhibiti wanachofanya wake zao na kuwafanya watiifu. Anampiga kwa kuvunja masharti aliyompatia ya

kutoenda kwao bila ruhusa yake. Kitendo cha Muna kuanza kupigana na mumewe kinaonyesha kwamba wake hawako tayari kukubali kudhulumiwa na waume zao kulingana na matokeo ya utafiti wa Gicuku (2012). Wanaamua kutetea haki zao katika ndoa.

Ugomvi umejengwa kupitia usawiri wa Muna na Hasani kimatendo na kiusemi katika riwaya ii hii. Usawiri wao kiusemi na kimatendo unasimuliwa ifuatavyo.

> Umefanya wazimu nini ? Au hujui kuwa vitu hivyo vimenunuliwa kwa pesa.
> Tena vikinunuliwa ? Ndiyo ninavivunja hivi !
> Makusudi ! Makusudi unavunja vitu ? Au una pesa nyingi za kutupa ? ( Uk. 186)

Usemi wa wanandoa hawa na kitendo cha Muna kinaonyesha ukosefu wa utulivu katika ndoa yao. Usemi na kitendo hiki kinaibua ugomvi unaotatiza uthabiti wake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuwa jamii imeundwa kwa asasi zinazotekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na uthabiti wa asasi hizi ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu haya. Uhusika wao kiusemi na kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaijenga changamoto hii. Mhimili huu unaeleza kuhusu dhana ya wahusika na uhusika. Usemi wao ni wa majibizano kati yao. Majibizano haya yanahusisha matumizi ya maswali na kauli zinazohitimishwa kwa alama hisi katika dondoo hili. Hii inaonyesha hisia nzito za hasira zinazoonyeshwa na hawa wahusika. Neno 'makusudi' limerudiwa na Hasani kuonyesha kukasirishwa sana na kitendo cha Muna cha kuvunja vyombo bila kujali gharama ya kuvinunua. Swali la mwisho la Hasani linaonyesha kwamba mbali na kukerwa na kuvunjwa kwa vyombo suala la Muna kumshinda kwa mshahara linamkera pia. Kitendo cha Muna kuvunja vyombo kinaonyesha kushindwa kwake kudhibiti hasira zake kwa kuona anaonewa na Hasani kwa kukatazwa kwenda harusini. Alikuwa amekasirishwa na tabia ya Hasani kumnyima uhuru wa kutangamana na watu wengine. Ingawa kitendo chake ni cha uharibifu pengine, kulingana naye kilikuwa njia bora ya kuonyesha Hasani kwamba amechukizwa mno na tabia ya kumyima uhuru. Ugomvi vile vile umesawiriwa na Hasani kupitia usawiri wake kiusemi. Muna anapomshauri Hasani kuhusu umuhimu wa kusoma vitabu na magazeti ili kujiongezea maarifa ambayo yanaweza kumfanya apandishwe cheo kazini anamjibu :

> Nisome! Nisome nini tena? Mimi kazi yangu ninaijua vizuri sana. Unafikiri ninaifanya vipi kazi hiyo miaka hii yote? ( Uk. 187 )

Dondoo hili linaonyesha kuwa ndoa hii ilikumbwa na ugomvi ambao unatatiza uthabiti wake na kuifanya isitekeleze ipasavyo majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Usemi huu kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia unamsawiri Hasani na kuibua ugomvi kupitia usawiri wake. Usemi wa Hasani unahusisha matumizi ya alama hisi na swali kuonyesha hisia za hasira alizonazo anapozungumza. Amerudia neno nisome kusisitiza kupinga kwake kwa pendekezo hili kutoka kwa Muna. Swali analouliza la mwisho katika dondoo hili linaonyesha kwamba anaona Muna anamdunisha kwa kumpendekezea apende kusoma. Kupuuzilia mbali ushauri wa Muna kuhusu kusoma vitabu na magazeti hata kabla ya kutafakari kunaonyesha haja yake ya kumkandamiza mkewe kimawazo. Anaogopa kukubali wazo zuri kutoka kwa mkewe kwa kuwa anadhani ataonekana duni au kuwa na upungufu.

Ugomvi umesawiriwa na mke wa Marufuku katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* kupitia usawiri wake kiusemi. Usemi huu unasimuliwa hivi :

> Wewe mizigo yako imekushinda na hicho kilimo chako cha mihogo umekwenda mbali huko kutafuta mengine. Au ukiwa mwanamume unaona mzigo wowote waweza kuubeba ? Wengine mna uume wa kuzaa wala si uume wa fikira !'' (Uk. 42)

Kauli hii inadhihirisha ukosefu wa uthabiti katika ndoa jambo linalosisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu inayoongoza huu utafiti. Ufafanuzi kuhusu jinsi changamoto hii imejengwa kupitia uhusika yameongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Ugomvi unajengwa kupitia usawiri wa mke wa Marufuku kwa mbinu ya kiusemi kama inavyofafanuliwa na Kenan (1983). Ugomvi huu unasababishwa na ndoa hii kushindwa kutekeleza majukumu yake yakukidhi mahitaji ya watoto kikamilifu umaskini. Usemi huu unadhihirisha hisia za hasira alizonazo mke wa Marufuku. Zinaashiriwa na matumizi ya maswali na kauli zinazoishia kwa alama hisi katika dondoo hili. Anaona mahitaji ya ndoa yao kama mzigo wa Marufuku na ameshindwa kuyakimu

kwa sababu ya pato lake dogo.  Katika usemi huu anamdunisha mumewe kwa kudhihaki jinsia yake ya kiume na kudai hana uwezo wa kufikiria bali kupata tu watoto.

Baada ya matusi haya Marufuku anambembeleza mkewe kwa kumwita mpenzi ili atulie apate kumweleza sababu ya yeye kulazimika kuwachukua hawa watoto. Badala ya kutulia anaongeza tusi jingine. Anamwonya mumewe asithubutu kumwita mkewe.  Anatamka :

> Usiniite mpenzi na usithubutu kuniita mkeo. Wewe mshenzi. Unikome… (Uk. 43)

Dondoo hili linaonyesha usemi ambao unamsawiri mke wa Marufuku na kujenga changamoto ya ugomvi. Changamoto hii inaikosesha ndoa hii utulivu ambao unahitajika ili kuifanya itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili huu unaeleza kuwa jamii ni mfumo wa asasi ambazo zinatekeleza majukumu muhimu ili kuidumisha na zinahitajika kuwa thabiti ili kutekeleza majukumu haya ipasavyo. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri kauli ya mke wa Marufuku inaonyesha namna ugomvi umejengwa kupitia uhusika wa kiusemi. Usemi huu unatolewa kwa ukali na hasira nyingi. Chuki ya mke huyu inaonyeshwa na kukataa mumewe asimuite mpenzi wala mkewe. Anakamilisha kauli hii kwa kumtusi na kumuonya asijishughulishe naye. Usemi wa Mkewe marufuku unaonyesha madharau ambayo anayo kwa mumewe kwa sababu ya umaskini unaokumba ndoa yao. Anaona kwamba mume hafai kuwa mume wa kupata watoto tu bali pia mwenye fikira au hekima. Mtazamo wake ni wa kibinafsi kwa kuwa anaona mumewe amefanya uamuzi mbaya kuamua kuwalea wapwa wake. Anaona kuwa kuafanya hivi kutawazidishia mzigo wa ulezi wakati ambapo wanakumbwa na umaskini. Anamwita mumewe mshenzi kwa kufanya uamuzi huu na hata anakataa kuitwa mke wa Marufuku. Gitau (2011) anasema kuwa wanaume katika ndoa hudhulumiwa na wake zao kwa kutukanwa na kudharauliwa kwa sababu ya kushindwa kutekeleza majukumu yao. Marufuku anatukanwa na kudharauliwa kwa kukosa uwezo wa kukimu mahitaji ya ndoa yao kikamilifu. Mkewe Marufuku anakataa kuonana kimwili na mumewe kwa sababu ya kuwachukua wapwa wake kuwalea. Odhiambo (2013) anasema kuwa mizozo katika ndoa huweza kusababishwa na mmoja wa wanandoa kususia majukumu ya ndoa kama vile kushiriki mapenzi na mumewe na pia kupika. Kitendo cha mke wa Marufuku kinashadidia maelezo ya mtaalamu huyu.

Matusi na madharau si suluhu kwa changamoto zinazokumba ndoa yoyote ile. Anayetukanwa huona amedunishwa na hii hufanya wanandoa kukosa nafasi ya kuzungumza na kutafuta suluhu mwafaka kwa shida inayowakabili.

Ugomvi umejadiliwa katika utafiti wa Katola (2006), Zastro (2008), Gitau (2011) na Gicuku ( 2012). Matokeo ya utafiti huu yamebainisha ugomvi kama changamoto ya ndoa lakini tofauti na wataalam hawa yameeleza namna changamoto hii inasawiriwa na wahusika kupitia usawiri au uhusika wao. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba changamoto ya ugomvi imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya teule. Hata hivyo matendo au usemi ambao umetumika unatofautiana kutoka riwaya moja hadi nyingine. Katika riwaya ya *Ua laFaraja* ugomvi umejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi. Tabu katika riwaya hii anaijenga kupitia kitendo ambacho kimetumiwa kumsawiri cha kupiga Ngoma kofi. Tabu na Ngoma wanaijenga kupitia usemi ambao umetumiwa kuwasawiri. Usemi huu ni majibizano kati yao wanapogombana. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* ugomvi umejengwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi wa Hasani na Muna. Wahusika hawa wote wanajenga ugomvi kupitia kitendo cha kupigana ambacho kimetumika kuwasawiri. Muna anaijenga kupitia kitendo cha kuvunja vitu vya nyumba yao na majibizano kati yao anapofanya hivi. Hasani anaujenga ugomvi kupitia kauli ya kumkemea Muna anapomshauri kujenga tabia ya kupenda kusoma. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* ugomvi umejengwa kupitia uhusika wa usemi wa mke wa Marufuku. Mkewe anajenga ugomvi kupitia kitendo kumgombeza mumewe na kumtusi kwa kuchukua wapwa wake kuwalea baada ya wazazi wao kufa na yeye ni maskini.

### 4.3 Udhihirishaji wa Athari za Changamoto za Ndoa Kupitia Usawiri wa Wahusika

Sehemu iliyotangulia imeshugulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa data kuhusu changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimesawiriwa na wahusika kupitia uhusika. Sehemu hii inachanganua na kuwasilisha data kuhusu athari za changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data hizi umeongozwa na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu na mhimili kwanza wa nadharia ya naratolojia.

Kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu asasi za kijamii kama vile ndoa zinaweza kuwa na faida au hasara kwa jamii, asasi au vipengele vingine katika jamii.

Lazima kipengele au vipengele vinavyoathiriwa na asasi fulani vibainishwe. Vipengele hivi vinaweza kuwa jamii nzima, watu binafsi au kikundi cha wanajamii (Merton, 1957). Watoto wa wanandoa au wanaolelewa nao kama kipengele cha jamii huathiriwa kwa njia mbalimbali na changamoto za ndoa za wazazi wao. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Kwa kuongozwa na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu na kwanza wa nadharia ya naratolojia sehemu hii inatathmini namna wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au wanaolelewa nao wanadhihirisha athari za changamoto za ndoa za wazazi au walezi wao kupitia mbinu za kusawiri wahusika jinsi zilivyofafanuliwa na Kenan (1983). Mbinu hizi ni matendo, usemi, mazingira na muonekano wa nje.

### 4.3.1 Kutatizika Kimasomo na Udhihirishaje Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu, asasi na michakato ya kijamii inaweza kuwa na athari hasi au chanya kwa jamii, asasi au michakato mingine. Michakato au asasi za kijamii zinafaa kuchanganuliwa kwa kuzingatia athari zake kwa jamii nzima, watu binafsi, makundi ya kijamii, asasi au michakato ya kijamii. Kwa kuongozwa na mhimili huu utafiti huu umebainisha kutatizika kwa masomo kuwa athari ya changamoto za ndoa kwa wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au wanaolelewa nao. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri ufafanuzi unatolewa kuhusu namna athari hii imejengwa kupitia uhusika.

Katika riwaya ya *Kiu* athari hii imejengwa kupitia uhusika wa kimatendo wa Bahati. Kitendo ambacho kimetumika kumsawiri na kujenga athari hii kinasimuliwa hivi :

> Yalianza dhiki na umaskini punde baba yake akapotea; punde akafeli shule; mara idi na tumaini zake akatokea…(Uk. 118).

Dondoo hili linaonyesha namna athari ya kutatizika kimasomo inadhihirishwa na Bahati kupitia usawiri wake kimatendo kulingana na mawazo ya Kenan (1983) kuhusu usawiri wa aina hii. Kitendo cha kufeli mtihani kinatanguliwa na umaskini na kutoweka kwa babake. Msimulizi

anaeleza changamoto ambazo zinachangia kuanguka kwa mtihani yaani kutowajibika kwa Jaku na umaskini wa ndoa hii. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa ndoa huathiri watoto kwa sababu ya changamoto zinazoikumba kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Cheusi hakuweza kumnunulia mwanawe mafuta ya kutosha ya kusoma wala taa nzuri ya kutumia. Tunasimuliwa kuwa alikosa mafuta taa ya kusoma na kulazimika kwenda kulala badala ya kusoma. Hii ilichangia kuanguka kwake katika mitihani kwani alikosa muda wa kutosha kudurusu ili kujiandaa vyema kwa mitihani. Baada ya kuanguka mtihani Bahati hapati fursa ya kuendeleza masomo yake, badala yake anaanza kuchumbiana na Idi na kuishia katika ndoa ambayo inavunjika hatimaye.

Kwenye riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) Juma anadhihirisha athari hii ya kutatizika kwa masomo kupitia usawiri wake kimatendo. Kitendo ambacho anasawiriwa kwacho na kuibua changamoto hii kinasimuliwa ifuatavyo :

> Alipoingia sokoni alivua shati lake jeupe la shule lisichafuke, akavaa shati jekundu. Sasa akavua lile jekundu, akamkabidhi mama yake, kisha akavaa shati lake la shule baada ya kujikausha jasho kwa lile alilovua. Akamuaga mama yake, akachukua mfuko wa vitabu, tayari kuelekea shuleni (Uk. 112)

Kitendo hiki kinaonyesha athari ya kutatizika kimasomo kwa Juma. Athari hii inasababishwa na kutowajibika, uasherati na ulevi wa Ngoma, babake Juma. Hii inasababisha umaskini ambao unaibua athari hii. Athari hii inathibitisha kuwa asasi au michakato ya kijamii inaweza kuwa na athari chanya au hasi kulingana na maoni ya Merton (1957). Kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri kitendo hiki kinamsawiri Juma na vilevile kudhihirisha athari hii. Juma badala ya kuenda moja kwa moja shuleni kusoma analazimika kuenda sokoni kumtafutia mamake bidhaa za kuuza na kusubiri aje kuzichukua ndipo aelekee shuleni. Anatoa shati jekundu alilokuwa amevaa na kuvalia jeupe ambalo ni sare ya shule. Shughuli ya kutafuta bidhaa kutoka kwa wauzaji wa jumla harakaharaka inamfanya atokwe na jasho. Anafanya hivi ili kumsaidia mamake apate pato la kuwakimu. Hii inamkosesha utulivu wa akili ambao anauhitaji ili kumakinika darasani. Gicuku (2012) anaeleza kuhusu wazazi kuwashirikisha watoto katika shughuli za kutafuta pato ili kukabiliana na

umaskini unaowakumba. Anaeleza kuhusu wao kuwatuma watoto wao kushiriki ukahaba mahotelini na kuwaletea pesa. Japo shughuli hii inatofautiana na ya Juma, zote zinawanyima watoto utulivu wanaohitaji wanapokua.

Juma katika *Ua la Faraja* amedhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kwa usemi ambao ni mazungumzo yake na jirani yake Omolo. Juma kupitia usemi wake anamsimulia Omolo namna hakumakinika shuleni na jinsi matokeo yake katika masomo yalianza kudidimia. Mazungumzo haya yanasimuliwa hivi:

> Nikabaki kivuli kilichokuwa kinatembea. Karibu mwezi mzima nilikuwa naenda shule alimuradi tu niende. Hata maendeleo yangu shuleni yakawa mabovu kuanzia hapo hadi sasa. (Uk. 126).

Usemi huu unaonyesha athari ya kimasomo inayosababishwa na ugomvi na uasherati kwa kurejelea mawazo ya Merton (1957) kuhusu athari za asasi na michakato ya kijamii. Juma anakosa kumakinika shuleni jambo ambalo linafanya matokeo yake kuanza kudidimia. Kwenda shule kunakuwa jambo la kawaida tu bila kutilia maanani faida yake. Dondoo hili linaonyesha namna athari hii inadhihirishwa kupitia uhusika wa kiusemi kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Usemi huu unaonyesha hisia za huzuni na masikitiko ya Juma kuhusu kutatizwa kwa masomo yake. Anajilinganisha na kivuli kinachotembea kumaanisha alikosa makini kabisa katika masomo na akendelea kwenda shule bila kutilia maanani umuhimu wake. Hii inatokana na changamoto ya ugomvi katika ndoa ya wazazi wake. Ugomvi huu unazushwa na babake. Matokeo ya kukosa kwake kuwa na utulivu na makini masomoni ni kudidimia kwa matokeo yake.

Aisha katika *Ua la Faraja* anadhihirisha athari hii kupitia uhusika wake kimatendo. Kitendo anachoshiriki na kinachodhihirisha athari hii kinasimuliwa hivi :

> Aisha alijifunza ukarani baada ya kumaliza darasa la saba, akapata ajira kwenye kiwanda hichohicho kama karani msaidizi. Mapato yao hapo nyumbani yakawa mazuri (Uk. 360)

Athari hii inasababishwa na changamoto ya kifo. Hii inashadidia mawazo ya Merton (1957) na maelezo ya mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu kuwa asasi za kijamii zinaweza kuwa na hasara. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri dondoo hili linaonyesha jinsi uhusika wa kimatendo wa Aisha unadhihirisha athari hii. Aisha anaacha kuendelea na masomo zaidi, anajifunza ukarani na kuajiriwa ili kusaidia kuwalea wadogo zake. Wazazi wa Aisha wanakufa kwa ukimwi na kumfanya akatiza masomo yake. Kinara (2013) anajadili kukatizwa kwa masomo ya watoto kama mojawapo ya athari za kifo cha wazazi kutokana na ukimwi. Anasema kuwa ukimwi huwaacha watoto yatima na kuwafanya walazimike kukatiza masomo yao na kutafuta njia ya kujipatia pato la kuwawezesha kulea wadogo zao. Jamii inafaa kuweka mikakati ya kuwezesha watoto kuendelea na masomo baada ya wazazi wao kufariki.

Agnes, Jane na Josii katika *Maisha Kitendawili* wamedhihirisha athari hii kwa kutohudhuria masomo. Athari hii imetokana na changamoto ya umaskini katika ndoa ya wazazi wao. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi kupitia Kasu:

> Walipokuwa wanakunywa chai Kasu alijiuliza kwa nini watoto wakubwa wa mama Josii, Agnes na Jane, walikuwa hawaendi shule. Lakini je, ikiwa baba yao aliyekohoa alipoimimina chai ya moto mdomoni mwake hawezi kwenda hospitali sembuse watoto kupata elimu? (Uk. 69)

Kwa mujibu wa Merton (1957) asasi za kijamii zina athari na kutohudhuria masomo kwa wahusika hawa kunadhihirisha athari ya changamoto za ndoa ya wazazi wao. Wahusika hawa wanatarajiwa kwenda shuleni lakini hawaendi kwa sababu ya umaskini wa wazazi wao. Baba yao alikuwa mgonjwa sana na mama yao alifanya biashara ndogo ambayo haikupatia pato la kuweza kuwasomesha. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia hasa maelezo yake kuhusu wahusika na uhusika kusawiriwa kwa wahusika hawa kwa kitendo hiki kunadhihirisha athari hii. Kwa mujibu wa dondoo hili tofauti na wahusika wengine wanaokumbwa na athari hii, hawa hawahudhurii shule hata kidogo. Hii inafanya watoto hawa wakose kujua kusoma na kuandika jambo ambalo huenda litafanya maisha yao kuwa magumu wanapotagusana na wanajamii kwa shughuli mbalimbali.

Hali hii inaweza kufanya watoto kama hawa kukosa kuihudumia jamii ipasavyo na kuendesha maisha yao barabara. Swali balagha limetumika katika dondoo hili kueleza sababu ya hawa watoto kutohudhuria shule. Ndoa hii ilikosa pesa za hata kumpeleka baba ya watoto hawa hospitalini.

Athari hii imedhihirishwa na Maria kupitia usawiri wake katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Anaisawiri athari hii kupitia wahuhusika wake kimatendo. Maria ameidhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kutolewa shuleni akiwa darasa la tano na babake, kukeketwa kwa lazima na kuozwa. Athari hii imesababishwa na changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Mama hujui yaliyomfika Maria alipotolewa shuleni akiwa darasa la tano na kuozwa? (Uk. 114)

Kitendo hiki kinaonyesha namna ushikilizi wa utamaduni unaathiri masomo ya watoto na hivyo kudhihirisha athari za asasi ya ndoa kwa watoto kulingana na mawazo ya Merton (1957) kuhusu athari za asasi na michakato ya kijamii. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri dondoo hili linaonyesha uhusika wa kimatendo wa Maria ambao unadhihirisha athari hii. Wazazi wa Maria wanashikilia utamaduni hasi wa kukeketa wasichana na ndoa za mapema. Hawathamini elimu ya mtoto msichana na hii ndio sababu ya Maria kutoendelea na masomo yake kukatizwa licha ya kutaka kuendelea nayo. Kitendo hiki kimesimuliwa kwa kutumia swali balagha kuvuta makini ya mhusika anayesimuliwa na pia msomaji mtarajiwa kuhusu maradhi ya kutodhibiti haja ndogo yanayompata Maria baada ya kujifungua. Babake alithamini watoto wa kiume kuliko wa kike. Anaona kuwa kumsomesha mtoto msichana si jambo muhimu kama ilivyo kumsomesha mtoto mvulana. Babake aliona kwamba kilicho muhimu kwa mtoto msichana ni kuolewa na kuwafaidi wazazi wake kwa mahari. Haya ni mawazo potovu kwa sababu elimu inafaa kumpa mtu maarifa ya kumfaa maishani na watoto wa jinsia zote wanahitaji maarifa haya. Nakhumicha (2013) anasema kuwa jinsia zote yaani wanaume na wanawake wanahitaji elimu ili kuwapatia uwezo ili kuboresha maisha ya familia zao. Mawazo ya babake Maria yanakinzana na mawazo haya.

Kukosa kuendelea na masomo kunafanya Maria ashindwe kuelewa maelezo ya daktari kuhusu ugonjwa wa kushindwa kuzuia haja ndogo baada ya kuolewa na kujifungua.

Matokeo ya utafiti huu yanaangazia athari ya kutatizika kwa masomo ya watoto kutokana na changamoto zinazowakumba wazazi wao. Kinara (2012) anaeleza namna watoto hulazimika kukatiza masomo ili kutafuta pato la kuwalea wadogo wao baada ya wazazi wote kufa kwa ukimwi. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha athari hii na kufafanua namna inadhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Masomo ni muhimu katika kuimarisha maisha ya watu na yanafaa kutolewa kwa jinsia zote kama anavyosema Nakhumicha (2013). Jamii inafaa kuweka mipango ya kuhakikisha kuwa watoto wote wanapewa nafasi sawa ya kuendeleza masomo yao. Wataalamu hawa japo hawakulenga kutafiti kuhusu athari za changamoto za ndoa, wanaeleza kuhusu kutatizika kwa masomo ya watoto na haja ya kutoa elimu kwa watoto bila kuwabagua kijinsia. Utafiti huu umetathmini jinsi athari ya kutatizika kwa masomo imedhihirishwa kupitia uhusika katika riwaya teule. Kwa kiwango kikubwa athari hii imedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wa kimatendo. Hata hivyo vitendo ambavyo vimetumika kusawiri wahusika na kuidhihirisha vinatofautiana katika baadhi ya riwaya teule. Katika riwaya ya *Kiu* imedhihirishwa kupitia kusawiriwa kwa Bahati kwa kitendo cha kuanguka mitihani na kutoendelea na masomo. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imedhihirishwa kupitia usawiri wa Juma kwa kitendo cha kulazimika kuenda sokoni kwanza kumnunulia mamake bidhaa za kuuza kabla ya kuelekea shuleni. Pia katika riwaya hii imedhihirishwa na Aisha kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kukatiza masomo yake katika darasa la saba, kujifunza ukarani na kuajiriwa ili kuwalea wadogo wake baada ya wazazi wao wote kufa. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* imedhihirishwa na watoto wa Mama Josii ambao wamesawiriwa kwa kitendo cha kutohudhuria masomo. Kwenye riwaya ya *Unaitwa Nani ?* imedhihirishwa na Maria kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kutolewa shuleni, kukeketwa na kuozwa kwa lazima. Athari hii imedhihirishwa kupitia uhusika wa kiusemi katika riwaya ya *Ua la Faraja* peke yake. Imedhihirishwa kupitia usawiri wa Juma kwa usemi anapozungumza na jirani yake ambaye anaitwa Omolo kuhusu matokeo yake shuleni kuwa mabovu.

### 4.3.2 Ukosefu au Upungufu wa Mahitaji ya Kimsingi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi, Kimazingira na Kimatendo

Athari hii imesababishwa na changamoto ya umaskini na kudhihirishwa na wahusika wanaokosa chakula kizuri au kukosa chakula kabisa, kukosa nyumba nzuri na ya kutosha na pia makao thabiti. Wanadhihirisha athari hizi kupitia usawiri wao kiusemi, kimazingira na kimatendo.

Rose katika *Maisha Kitendawili* anadhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kiusemi. Kauli ya Rose kwa Farida inasimuliwa hivi:

> Wajua mimi nilikulia katika umaskini wa kutisha. Baba yangu ana mkono mmoja na mama hana kazi. Mama ndiye aliyejaribu kutulea. Kila siku tulikula mboga za majani mpaka majirani zetu wakatubandika majina… Siku fulani tungelala bila kula chochote jioni. Asubuhi tukienda shuleni katika matope ya baridi bila viatu tuliyumbayumba kama walevi. (Uk.105)

Dondoo hili linadhihirisha athari ya ukosefu wa chakula kabisa au chakula bora na viatu kutokana na umaskini ulioikumba ndoa ya wazazi wa Rose. Kwa kuzingatia mhimili wa pili umuundo- uamilifu athari hii inathibitisha kwamba asasi za kijamii kama vile ndoa zinaweza kuwa na hasara. Umaskini unafanya Rose kukosa chakula bora au kukosa chakula kabisa na viatu. Jambo hili linafanya yeye na ndugu zake kuchekwa na majirani na kutembea kwa matope baridi miguu mitupu wakielekea shuleni. Dondoo hili linaonyesha namna athari hii imedhihiriswa na mhusika huyu kupitia uhusika wake kiusemi kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia. Mhimili huu hueleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Rose anasisitiza kuhusu umaskini ulioikumba familia yake kwa kuelezea kuwa wa kutisha. Anaeleza chanzo cha umaskini huu kuwa ni ulemavu wa babake na mamake kubakia kuubeba mzigo wa kuwalea. Usemi wake unaibua hisia za kuhurumiwa anapoeleza kuhusu kula mboga za majani kila siku hadi wanachekwa na majirani na pia kwa kulala njaa. Anakamilisha usemi wake kwa kumithilisha kutembea kwao wakiyumbayumba na kutembea kwa mlevi. Hii inatokana na kutembea kwa matope baridi wakienda shuleni. Kukosa chakula bora au kukosa chakula kabisa bila shaka kunaathiri ukuaji wa Rose na ndugu zake na hata kutatiza masomo yao. Kukanyaga matope baridi kwa miguu mitupu kunafanya miili yao kuingia baridi jambo ambalo linaweza kuathiri afya yao. Matatizo haya yanaonyesha namna umaskini unatatiza jukumu la ndoa la

kukidhi mahitaji ya watoto kama inavyofafanuliwa na nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoongoza utafiti huu.

Athari hii imedhihirishwa na wahusika watoto wa wanandoa kupitia usawiri wao kimazingira. Imesawiriwa na waandishi wa riwaya teule kwa kutumia mazingira mbalimbali kuwasawiri. Mazingira haya ni nyumba duni wanamoishi. Bahati katika riwaya ya *Kiu* anadhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kimazingira. Hali ya chumba cha Bahati inaelezwa hivi:

> Mara aligeuka na kutazama chumba chake. Kanzu ya waridi yenye maua makubwa na nyingine ya makunguru, zilining'inia ukutani juu ya msumari, na nyingine moja ilikuwamo ndani ya kasha chini ya mvungu wa kitanda chake cha mayowe. Ukuta wa pili ulikuwapo msala uliochakaa ambao haukuwa ukitumiwa kutwa mara tano kama inavyopasa, na kando yake alikuwapo mende akipapasa kwa mashurubu yake- kapoa, yuko kwake. (Uk. 28)

Mazingira haya yanadhihirisha athari ya umaskini na kutowajibika kwa watoto wa wanandoa. Athari hii inaonyesha kuwa umaskini na kutowajibika huathiri watoto wa wanandoa. Hii inathibitisha kwamba asasi za kijamii zinaweza kusababisha hasara kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Chumba hiki ni kidogo na analazimika kuweka kasha la nguo chini ya kitanda. Ina msala uliochakaa na pia kuna mende wanaoishi ndani. Athari hii imedhihirishwa na Bahati kupitia usawiri wa wahusika kimazingira kama unavyofafanuliwa na Kenan (1983). Maelezo ya chumba hii yanatupatia taswira ya mahali duni ambapo hapafai kwa Bahati. Kinakosa vitu muhimu kama mahali pa kuweka nguo, zinaning'inizwa kwa msumari. Kuna kitanda cha mayowe na msala uliochakaa na pia chumba hiki kina mende kuonyesha hali duni ya chumba inayokifanya kuvamiwa na wadudu kama hawa. Hali duni ya chumba hiki haimpatii Bahati mazingira mazuri na tulivu ya kulala au kukaa. Mawazo ya Bahati anapokitazama chumba hiki yanaonyesha kwamba anasumbuliwa kimawazo kutokana na kuishi katika chumba duni kwa sababu ya umaskini wa wazazi wake.

Athari hii imesawiriwa na Agnes, Jane na ndugu zao tisa na Kasu katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* kupitia usawiri wao kimazingira. Hali ya nyumba hii inasimuliwa hivi:

> Nyumba yake yavuja maji paani na ukutani. Chakula chake cha taabu na mumewe alikuwa mgonjwa sana kwa mnamo miaka saba ni baadhi ya mambo yanayomfikirisha Kasu (Uk. 68)

Athari hii inatokana na changamoto ya umaskini ambayo inaikumba ndoa hii na kushadidia maoni ya Merton (1957) kuwa asasi za jamii zinaweza kuleta hasara kwa watu binafsi au asasi nyingine. Watoto hawa katika *Maisha Kitendawili* wanaishi katika nyumba ndogo na inayovuja maji paani na ukutani. Mazingira ya nyumba hii yanawaweka watoto hawa katika hatari ya kuweza kuambukizwa magonjwa. Mazingira haya yanaonyesha namna usawiri wa wahusika kimazingira, kwa kurejelea mhimili wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Mbali na kukosa nyumba nzuri wanakosa chakula na pesa za kugharamia matibabu. Nyumba hii inakosa samani bora, ina meza iliyolemaa na inayocheza aina ya densi ambayo mtunzi ainaiita brekidansi. Kasu ameidhihirisha athari hii kupitia mtaa wa mabanda ambamo anaishi. Mazingira haya yanasimuliwa ifuatavyo:

> Yasmini na mwenzake Kasu wamepata kibanda katika mtaa wa Soweto. Kibanda hiki ni kimoja katika vibanda vyenye  vyumba vingi na vilivyokaa kwenye mteremko mkali ajabu (Uk. 26).

Mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuwa asasi za jamii zinaweza kuwa na faida, hasara, au zisiwe na athari yoyote kwa asasi nyingine, jamii au watu binafsi. Mazingira haya yanaonyesha athari ya umaskini, kifo na ugomvi kwa watoto wa wanaolelewa na wanandoa. Yanaonyesha namna ndoa ya wazazi wa Kasu na ya mjombake inamathiri. Anaishi katika mtaa wa mabanda wa Soweto baada ya kutoroka kwa mjombake Marufuku. Kusawiri wa kwake kwa kutumia mbinu ya mazingira inayofafanuliwa na Kenan (1983) kunadhihirisha athari hii. Maelezo haya yanaibua taswira ya mazingira duni ambayo yanawakosesha utulivu wakazi wake. Mbali na udogo wake, chumba hiki kimejengwa kwa mteremko mkali na kukifanya kukosa uthabiti. Hii inafanya Kasu na mwenzake kuishi kwa wasiwasi. Mtaa huu hauna utulivu. Kasu anashuhudia jibwa linalopita na mtoto ambaye alitupwa baada ya mamake kuavya. Soweto kulikuwa na kelele, uasherati, fitina, uchawi, uganga, ulevi, unafiki, uchafu na magendo.

Mazingira haya yanashadidia maelezo ya Gicuku (2012) kuhusu maisha wanayoishi watoto wanaotorokea mjini. Anasema kuwa kuvunjika kwa ndoa hufanya watoto kutorokea mjini na kuishi katika mazingira hatari kama wanyama. Wanakosa mtu wa kuwakimu na kudhulumiwa na wanajamii wasio na huruma.

Athari hii imedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao kwa matendo mbalimbali. Agnes, Jane na ndugu zao tisa wanasawiri athari kwa kusawiriwa kupitia kitendo cha kulalia malazi duni. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi na msimulizi wa nafsi ya tatu:

> Mama Josii aliendа kuvua makaratasi mvunguni mwa kitanda na kujongeza meza iliyolemaa na kucheza brekidansi daima. Aliijongeza pembeni na kuwatandikia watoto wake pamoja na mgeni wake (Uk. 67)

Farida na Kasu pia wanasawiri athari hii kupitia usawiri wa kimatendo, kitendo hiki ni kulalia malazi duni. Kitendo hiki kinasimuliwa kama ifuatavyo:

> Huko katika chumba cha kukaa ndiko Farida walikokuwa wamelazwa kwa jamvi kuuukuu lililotandikwa magunia na maleso yaliyozeeka. Jamvi hili lilichekesha lilivyokuwa limeliwa na mchwa ungedhani ni ramani ya Afrika (Uk. 34)

Kulalia malazi duni kunaonyesha athari ya umaskini katika ndoa ya Mama Josii na ya Marufuku. Kitendo hiki kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu kinaonyesha athari ya asasi ya ndoa hizi kutokana na umaskini unaozikumba. Usawiri wa wahusika hawa kwa kitendo hiki kulingana na mhimili wa kwanza nadharia ya naratolojia  unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri unaidhihirisha athari hii. Katika madondoo haya mawili wahusika wamesawiriwa wakilalia malazi duni ishara kwamba hawakupata mapumziko ya kutosha. Taswira inayojengeka kutokana na kitendo hiki ni ya usumbufu kwa watoto ambao ndoa inatarajiwa kuwajibikia malezi yao kikamilifu. Athari hii kwa upande wa Farida na Kasu inatokana na kufa kwa wazazi wao na baadaye kuchukuliwa na mjomba wao ambaye alikuwa maskini.

Ukosefu au upungufu wa mahitaji ya kimsingi umedhihirishwa na wahusika wanaokosa makao thabiti. Juma katika *Ua la Faraja* anaidhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kimatendo. Imesababishwa na changamoto ya ugomvi inayokumba ndoa ya wazazi wake. Kitendo ambacho kimetumika kumsawiri na kudhihirisha athari hii kinasimuliwa ifuatavyo:

> Baada ya kuondoka nyumbani miaka minne iliyopita, Juma alikwenda kuishi Buguruni Malapa, kwa babu yake, kwa muda wa mwaka mmoja. Akafanikiwa kufanya mtihani na kumaliza darasa la saba (Uk. 214).

Kasu katika *Maisha Kitendawili* ameidhihirisha kupitia usawiri wake kimatendo. Anaisawiri kupitia kitendo cha kuhamahama kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Kasu alipofika darasa la nne hata hivyo alikimbia shule na kwenda kuishi na mwanamke mwengine katika kijiji jirani. Baada ya siku chache akakimbilia mjini. Hakuna aliyejua sababu yake ya kukimbia pale nyumbani kwa mjomba. Wote walilaumiana (Uk. 43).

Kuhama kutoka mahali pamoja hadi pengine kwa wahusika hawa kulingana na maoni ya mwana umuundo- uamilifu uamilifu Merton (1957) kuhusu athari za asasi za kijamii kunadhihirisha athari ya ndoa kwa watoto wa wanandoa. Athari hii inasababishwa na ugomvi katika ndoa ya Tabu na Ngoma kwenye *Ua la Faraja* na kifo, umaskini na ugomvi katika ndoa ya Marufuku na mkewe kwenye *Maisha Kitendawili*. Usawiri wa wahusika Juma na Kasu kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri unadhihirisha athari hii. Juma anatoroka nyumbani kwao kwa sababu babake alizua ugomvi kwa kumtaka ahudhurie sala zote licha ya kwamba yeye ni mwanafunzi na anafaa kuzingatia shughuli za shule kikamilifu. Baadaye anarudi baada ya babake kuugua na kuwa mahututi na kuanza kuendesha biashara zake na kuwalea wadogo zake. Kukosa makao thabiti kunafanya Juma akose utulivu ambao ni muhimu kwa masomo yake. Matokeo yake masomoni yanaanza kudidimia na hatimaye anaacha kuendelea na masomo ya shule ya upili.

Kasu anatolewa kutoka kwao na kuanza kuishi na majombake Marufuku baada ya wazazi wake wote kufariki. Mjombake anamnajisi baada ya mkewe kuzua ugomvi na kumyima malazi kwa

kuwachukua watoto hawa kuwalea ilhali walikumbwa na umaskini. Baadaye anahamia kijiji jirani kuishi na mwanamke fulani baada ya mjombake kumnajisi. Kitendo hiki kinazua maswali kuhusu kinachomsukuma Kasu kuenda kuishi na jirani badala ya mjombake na hatimaye kuguria mjini na kuishi katika mtaa wa mabanda. Maswali haya yanaibua taharuki kwa upande wa msomaji. Kasu hawaelezi walezi wake sababu ya kutoroka. Baadaye tunasimuliwa kwamba alitoroka kwa sababu ya mjombake kumnajisi. Kuna kinaya katika kitendo cha Kasu kutoroka mjombake na kuenda kuishi maisha ya taabu mjini bila mtu wa kukimu mahitaji yake. Kasu anatorokea mjini na kuishi katika mtaa wa mabanda wa Soweto. Baadaye anahama Soweto baada ya kushindwa kulipa kodi na mzee mwenye nyumba kuwafukuza. Anawatusi yeye na rafikiye kwa kuwaita malaya jambo ambalo halikuwa na ukweli wowote. Mama Josii anampata njiani na kwenda naye kwake. Anaishi kwa mama huyu kwa muda na baadaye anaolewa na Mjomba. Kukosa makao thabiti kunafanya Kasu akatize masomo yake, aishi katika mtaa duni wa mabanda, atukanwe na mwenye nyumba na hatimaye kuolewa kama njia ya kujinusuru. Wanandoa wanafaa kujizatiti kuwa na mazingira bora ya kulea watoto wao ili wasilazimike kutorokea kwingine na kuathiri vibaya maisha yao.

Gicuku (2012) katika utafiti wake kuhusu ndoa ameeleza athari ya watoto kutorokea mjini na kuishi katika mazingira hatari baada ya ndoa kuvunjika. Utafiti huu umeshughulikia athari hii na nyingine kama vile ukosefu wa chakula bora au ukosefu wa chakula kabisa, malazi duni na makazi duni. Maelezo yametolewa kuhusu namna kila athari imedhihirishwa na wahusika kupitia mbinu zilizotumika kuwasawiri au uhusika wao. Waandishi wa riwaya teule wametumia njia mbalimbali kusawiri wahusika ili kudhihirisha athari hii. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* imedhihirishwa kupitia uhusika wa kiusemi, kimazingira na kimatendo. Rose kupitia uhusika wa kiusemi anaeleza namna yeye na ndugu zake walikula mboga za majani kila siku, namna walilala nja na kuenda shuleni bila viatu. Watoto wa Mama Josii wamedhihirisha athari hii kwa uhusika wao kimazingira. Mazingira haya ni nyumba ndogo ambamo wanaishi na inayovuja paa na kuta. Yasmini na rafiki yake wanaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwao kupitia mazingira ya kibanda wanamoishi katika mtaa wa Soweto. Watoto wa Mama Josii wanaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kulalia karatasi. Farida katika riwaya hii anaidhihirisha kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kulalia jamvi kuukuu. Kasu anadhihirisha athari hii kwa kusawiriwa kwa kitendo cha kuhamahama kutoka mahali pamoja kwenda kwingine. Katika riwaya ya *Kiu* athari

hii imedhihirishwa na Bahati kupitia mazingira duni ya chumba chake ambayo yametumika kumsawiri. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* athari hii imedhihirishwa na Juma kupitia uhusika wake kimatendo. Amefanya hivi kupitia kitendo ambacho kimetumika kumsawiri cha kutoroka kwao kwenda kuishi kwa babu yake kasha kurudi kwao baadaye.

### 4.3.3 Ajira ya Watoto na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo

Ajira ya watoto imesababishwa na changamoto ya kutowajibika, uasherati, ulevi, umaskini na kifo. Ajira ya watoto imedhihirishwa na Juma na Aisha katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia usawiri wao kimatendo. Juma anadhihirisha hii athari kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kuacha kuendelea na masomo ili kumsaidia mamake kuikimu familia. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Juma alikataa akasema " Mama anahitaji msaada wangu. Sekondari itanichelewesha kumsaidia mama." Huu ulikuwa msimamo wake. Hata mama yake alipomhimiza kuuvunja alikataa. Kwa shingo upande, Omolo akamridhia, akampatia ajira kwenye kiwanda chake (Uk. 214)

Kitendo hiki kinamsawiri Juma kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaotoa maelezo kuhusu usawiri wa wahusika. Kusawiriwa kwake kwa kitendo hiki kunadhihirisha athari za asasi za kijamii kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Athari hii inatokana na changamoto ya kutowajibika na umaskini katika ndoa ya wazazi wa Juma. Katika dondoo hili usemi halisi wa Juma umenukuliwa kuonyesha sababu yake ya kuamua kukatiza masomo yake na kutafuta ajira. Anakataa hata himizo la kuendelea na masomo kutoka kwa mamake ambaye anadai kutaka kumsaidia. Usemi wa Juma ambao umenukuliwa katika dondoo hili unaonyesha sababu zinazowasukuma watoto kuingia katika ajira. Umaskini na kutowajibika kwa Ngoma ndiko kunakomsukuma Juma kuingia katika ajira ya watoto. Baba yao alipata pesa nyingi kutokana na biashara ya matatu lakini alizitumia kwa ulevi badala ya kuikimu familia. Ngoma ni mfano wa wazazi anaongazia Gicuku (2012), wazazi ambao wanapuuza malezi ya wanao na kuzama katika shughuli za kutafuta pesa na anasa. Juma anaisawiri kupitia kitendo cha kuacha kuendelea na masomo na kuanza kufanya kazi aliyotafutiwa na jirani yao Omolo katika kiwanda akiwa na umri mdogo. Juma anakataa kuendelea na masomo hata baada ya jirani yao Omolo kuahidi kumlipia karo. Anaajiriwa ili

kumsaidia mamake kuikimu familia. Athari hii imedhihirishwa na Aisha kupitia usawiri wake kwa kitendo kifuatacho.

> Aisha alijifunza ukarani baada ya kumaliza darasa la saba, akapata ajira kwenye kiwanda hichohicho kama karani msaidizi (Uk. 360)

Aisha anaanza kufanya kazi katika kiwanda anakofanya kazi Omolo na mamake mdogo Grace. Anafanya hivi ili kupata pato la kuwatunza wadogo zake baada ya wazazi wao wote kufa. Kinara (2012) anaeleza namna watoto yatima hulazimika kuajiriwa wakiwa na umri mdogo ili kupata pato la kuwawezesha kuwalea wadogo zao. Usawiri huu wa Aisha kimatendo unashadidia maelezo yake kuhusu ajira ya watoto.

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* athari hii imedhihirishwa na Wamae na ndugu zake kupitia usawiri wake kimatendo. Athari hii imesababishwa na changamoto ya umaskini inayokumba wazazi wake. Kitendo kinachoisawiri athari hii kinasimuliwa ifuatavyo:

> Ndugu zake wadogo walikuwa wakifanya kazi kwenye mashamba ya mkonge yaliyokuwa karibu na nyumbani; mdogo, kitinda mimba keshakimbilia kwenye mashamba ya mananasi kulikokuwa na nafuu kidogo.(Uk. 11)

Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu athari hii inathibitisha kuwa asasi za kijamii zinaweza kusababisha hasara. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia uhusika wa kimatendo wa Wamae na nduguze unadhihirisha athari hii. Katika riwaya hii ya *Unaitwa Nani?* matendo yanayosawiri wahusika hawa yanahusu kufanya kazi katika mazingira hatari ya mashamba ya mkonge. Katika mazingira haya huenda wanafanyishwa kazi za sulubu za kulima, kukata mkonge, kupanda na hata kubeba makonge baada ya kukatwa. Kufanya kazi katika mashamba ya mananasi kunaelezwa kuwa nafuu kidogo. Hii inamaanisha kazi kwa mashamba ya mkonge ilikuwa ngumu. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha ajira ya watoto kama mojawapo ya athari za changamoto za ndoa. Kinara (2012) anaeleza kuhusu athari hii katika utafiti wake kuhusu madhara ya ukimwi. Utafiti umeibainisha

ajira ya watoto kama athari inayosababishwa na changamoto za ndoa kama vile umaskini na kutowajibika mbali na ugonjwa wa ukimwi.

Aidha matokeo ya utafiti huu yanafafanua namna athari hii inadhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao kimatendo. Athari hii imesawiriwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?*. Katika riwaya hizi mbili athari hii imedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao kimatendo. Wote wameajiriwa kazi wakiwa na umri mdogo. Hata hivyo wamesawiriwa kwa kitendo cha kufanya kazi katika maeneo tofauti. Katika *Ua la Faraja* Aisha na Juma wanafanya kazi kiwandani. Katika *Unaitwa Nani?* Wamae na ndugu zake wanafanya kazi katika mashamba ya mkonge na mananasi. Kuajiriwa kwa watoto mbali na kuathiri ukuaji wao kunawanyima fursa ya kusoma au kuendeleza masomo yao hadi viwango vya juu. Kuajiriwa kwa Juma, Aisha na nduguze Wamae kunafanya wakatize masomo yao. Jamii kwa ujumla inafaa kuweka na kutekeleza mikakati ya kukomesha ajira ya watoto kwa kuwa inaharibu maisha ya baadaye ya watoto na ya jamii kwa ujumla.

### 4.3.4 Chuki ya Watoto kwa Wazazi, Huzuni, Ukiwa na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Athari ya chuki ya watoto kwa wazazi, huzuni na ukiwa imedhihirishwa na watoto wa Ngoma na Tabu. Imesababishwa na changamoto ya uasherati, kutowajibika, kifo na magonjwa. Juma anadhihirisha chuki kwa babake kupitia usawiri wake kiusemi. Kauli yake anapozungumza na jirani yake Omolo inasimuliwa hivi:

> Kusema kweli, toka zamani mimi na baba hatuivi chungu kimoja. Yeye kule, mimi huku. Mama tu, ndiye aliyenihimiza kumpenda baba na kumnyenyekea hata akija amelewa (Uk. 125)

Aidha Juma anaidhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kimatendo. Anakataa kuenda kumuona na kusameheana na babake anapougua. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Siku hiyo ya pili alidhihirisha chuki dhidi ya baba yake kwa jazba aliyoionyesha. Akatishia kuacha kazi kama Omolo atazidi kumsisitiza kwenda kumuuguza baba yake (Uk. 235)

Dondoo hili linaonyesha chuki ya Juma kwa babake kwa sababu ya changamoto ya kutowajibika iliyokumba ndoa ya wazazi wake. Hii chuki inaonyesha athari za asasi za kijamii kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Juma anaidhihirisha athari hii kupitia uhusika wake kiusemi na kimatendo kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Juma anaeleza kuwa chuki kati yake na babake imedumu kwa muda mrefu. Ilibidi mamake aingilie na kumhimiza kumpenda babake. Anatumia viashiria kuonyesha utengano ambao ulikuwa kati yao. Usemi wa Juma unatolewa kwa kutumia vipumuo kadha na kwa kutumia msemo kueleza chuki kati yake na babake. Anatumia msemo wa wao kutopikika katika chungu kimoja kueleza chuki kati yao. Usemi wake unatolewa kwa kauli fupifupi, labda hii inadhihirisha hisia za hasira zinazoombatana na matamshi haya.

Matendo ya Juma katika dondoo la pili yanadhihirisha chuki kubwa kwa babake. Anahiari kuwacha kazi nayofanya kwa kiwanda anakofanya kazi Omolo ikiwa ataendelea kumsihi amtembelea babake anayeugua. Watoto hujifunza kupenda kutoka kwa wazazi wao na inakuwa vigumu wao kupenda watu wengine ikiwa hawapendwi na wazazi (Gicuku, 2012). Chuki ya Juma kwa babake imetokana na baba yao kutowapenda na kutowajali.

Juma katika riwaya ii hii ya *Ua la Faraja* anadhihirisha chuki kwa babake na huzuni kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kulia usiku anapofikiria jinsi babake alivyomwambukiza mamake ugonjwa wa ukimwi. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Machozi ya uchungu na chuki yalishuka usoni mwake na kudondokea kwenye mto aliokuwa ameulalia. Hakujali kuyafuta (Uk. 37)

Kitendo hiki kinaonyesha chuki ya Juma kwa babake kwa kumuambukiza mama yao ugonjwa wa ukimwi. Anaona kwamba mama yao ambaye alijitolea kuwalea baada ya baba yao

kuwatelekeza amedhulumiwa. Anahofia wao kuachwa yatima hatimaye baada ya mama yao kufa kwa ugonjwa huu.

Huzuni katika riwaya ya *Ua la Faraja* umedhihirishwa na Juma kupitia usawiri wake kupitia kitendo cha kulia mfululizo baada ya mamake kufariki. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Siku tatu mfululizo, tokea mama yake alipofariki, Juma alipendelea kukaa juu ya matofali yale saa za jioni akimkumbuka mama yake huku akilia (Uk. 356)

Aisha katika riwaya ya *Ua la Faraja* anaisawiri athari hii kupitia usawiri wake kimatendo. Anafanya hivi kupitia kitendo cha kulia anaposikia mamake akilia kwa kuambukizwa ukimwi na baba yao. Kitendo hiki kinasimuliwa hivi:

> Aisha akatazamana na kaka yake. Mama yao alipoanza kulia naye alilala kitandani na kuanza kulia kwa uchungu…Nguvu zilimwisha Abu. Machozi yalikuwa yanamlengalenga. Juma aliwatazama. Hasira ikaongezeka. ( Uk. 35- 36)

Matendo yaliyonukuliwa yanaonyesha athari ya huzuni ya changamoto ya kifo na uasherati katika ndoa ya wazazi wa Juma na Aisha. Athari hii inaonyesha kuwa asasi za jamii zinaweza kusababisha athari kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Matendo haya yanaonyesha jinsi usawiri wa wahusika kimatendo kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unadhihirisha athari hii. Mhimili wa kwanza wa nadharia hii unaeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawirijinsi anavyofafanua Kenan(1983). Kitendo katika dondoo la kwanza kinatendeka mfululizo kwa siku tatu. Ni kitendo cha maombolezi baada ya Juma kufiwa na mamake. Kitendo hiki kinadhihirisha hisia za huzuni ambazo Juma ako nazo. Juma alikuwa na uhusiano wa karibu sana na mamake kwa sababu alijitolea kuwalea baada ya baba yao kuwatelekeza. Kitendo cha pili kinatokea usiku na kinasababishwa na masikitiko ya Aisha na ndugu zake. Wanasikitika kuwa baba yao amemuambukiza baba yao ukimwi na angekufa baadaye na kuwaacha yatima. Matendo ya Juma na Aisha yanaonyesha jinsi mienendo isiyofaa ya wazazi inaweza kuathiri watoto wao. Kama Ngoma angejiepusha na uasherati ambao

unafanya aambukizwe ukimwi na kuambukiza mkewe hii hali ya huzuni haingewakumba watoto wake.

Ukiwa unadhihirishwa na Juma na ndugu zake kupitia usawiri wao kwa kitendo cha kubaki peke yao baada ya mama yao kufa na wao kubaki bila mzazi yeyote. Vile vile kinadhihiriwa na usawiri wa Juma kupitia mawazo yake kuhusu hali yake ya ukiwa. Mawazo yake yanasimuliwa ifuatavyo:

> Mawaidha ya Dkt Hans yalimvutia, lakini hayakutosha kumfariji. Yalimpa matumaini, yalimpa maana, sababu na kiasi cha faraja, lakini hayakuweza kulijaza pengo, uwazi wa pendo uliotokana na kuondoka kwa marehemu mama yake (Uk. 356).

Mawazo haya yanamsawiri yanamsawiri Juma kiusemi kulingana na maelezo ya Kenan (1983) kuhusu usawiri wa wahusika kwa kutumia mbinu hii. Athari hii inasababishwa na changamoto ya kifo inayokumba ndoa hii. Ukiwa unaodhihirishwa na Juma unathibitisha kuwa asasi za kijamii zinaweza kuwa na athari kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Katika dondoo hili mawazo ya Juma yanadhihirisha pengo la upendo ambalo limewachwa na kifo cha mama yao. Anaona hili ni pengo au ukiwa ambao hauwezi kujazwa na mawaidha au kufariji kokote. Mawazo haya yamemesimuliwa kwa kauli fupifupi ambazo zimetangulishwa na koma na nukta. Mazingira ya huzuni, ukiwa na chuki yaliyosababishwa na uasherati wa Ngoma katika riwaya hii yanaathiri malezi na ukuaji wa watoto waliorejelewa. Huzuni unafanya Juma kukosa furaha wakati wazazi wao wangali hai na hata baada ya kufariki. Hisia hizi zinawasababishia usumbufu wa kiakili kutokana na kufahamu kwamba baba yao ndio wa kulaumiwa kwa kumwambukiza mama yao ukimwi. Chuki ya watoto kwa wazazi hujenga uadui na kukatiza mawasiliano kati yao. Juma anamwona babake kama adui kwa kuwatelekeza na kumwabukiza mamake ukimwi. Uadui huu unajenga ukuta kati yao na kuzuia mawasiliano baina yao. Wajibu wa wazazi wa kuwaelekeza watoto, kuwafunza amali na kanuni za jamii unakatizwa na huu ukosefu wa mawasiliano. Wazazi wanafaa kuwapenda na kujitahidi kutimiza mahitaji ya wanao. Wanafaa pia kujiepusha na maovu kama uasherati na ulevi. Kufanya hivi kutaepusha chuki kati yao na wanao. Gicuku (2012) anaeleza chuki ya watoto kwa wazazi kama athari ya ndoa kushindwa kutekeleza wajibu wake. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha athari

hii mbali na athari nyingine ambazo ni ukiwa na huzuni. Matokeo haya hayaonyeshi tu athari hizi bali yanafafanua namna zimedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Athari hii imedhihirishwa tu katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Katika riwaya hii Juma ameidhihirisha kupitia usawiri wake kiusemi na kimatendo. Amesawiri chuki kupitia usawiri wake kwa kauli kwamba hakuwa anampenda babake na kitendo cha kukataa kwenda kumuuguza babake. Huzuni umedhihirishwa na Juma na Aisha kupitia kusawiriwa kwa kwao kitendo cha kulia. Ukiwa umesawiriwa na Juma na ndugu zake kupitia usawiri wao kwa kitendo cha kubaki katika hali ya upweke baada ya wazazi wao wote kufariki. Juma amedhihirisha huzuni kupitia kusawiriwa kwake kwa mawazo hali ya ukiwa inayomkumba baada ya mama yao kufa.

### 4.3.5 Watoto Kuachiwa Jukumu la Ulezi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo

Athari hii imesababishwa na changamoto ya kifo na imedhihirishwa na Juma na Aisha katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia usawiri wao kimatendo. Juma ameidhihirisha athari hii kupitia kusawiriwa kwa kitendo kinachosimuliwa ifuatavyo:

> Sasa alikuwa anaendesha moja ya magari aliyoridhi kutoka kwa marehemu baba yake. Baada ya kifo cha Ngoma haikuwezekana tena kuuza magari yote kama ilivyokusudiwa. Wanafamilia kwa upande wa Tabu walipendekeza magari hayo yaendelee kuzalisha pesa, na pesa hizo ziwekwe kwenye akaunti ya pamoja ya watoto wote ( Uk. 359)

Aisha ameidhihirisha kupitia usawiri wake kupitia matendo yanayosimuliwa ifuatavyo:

> Aisha alijifunza ukarani baada ya kumaliza darasa la saba, akapata ajira kwenye kiwanda hichohicho kama karani msaidizi. Mapato yao hapo nyumbani yalikuwa mazuri (Uk. 360)

Madondoo haya yanaonyesha uhusika wa kimatendo wa wahusika hawa kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri. Uhusika wa Juma na Aisha kama inavyoashiriwa na madondoo haya unaonyesha athari ya watoto kuachiwa jukumu la malezi kwa sababu ya kufa kwa wazazi.

Hii inathibitisha kwamba asasi za kijamii zinaweza kusababisha athari hasi au chanya kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Katika madondoo haya yote Aisha na Juma wanashiriki shughuli ya kupata pato la kutumia kukidhi mahitaji ya wadogo wao baada ya wazazi wao wote kufariki. Pesa anazokusanya Juma kutoka kwa biashara za matatu anaziweka katika benki na kuzitumia kugharamia mahitaji ya watoto. Aisha naye anatumia mshahara wake kufanya vivi hivi. Wanalazimika kutekeleza jukumu la malezi licha ya umri wao mdogo.

Suala la watoto kuachiwa jukumu la malezi limejitokeza katika utafiti aliofanya Kinara (2012) kuhusu ukimwi. Watoto yatima hulazimika kukatiza masomo yao kama Aisha ili kutafuta pato la kuwawezesha kuwakimu wadogo wao. Utafiti huu mbali na kubainisha athari kuwa athari ya changamoto za ndoa umefafanua namna imedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Athari hii imesawiriwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia uhusika wa kimatendo peke yake. Juma na Aisha na Juma wameidhihirisha kupitia usawiri wao kwa kitendo cha kutafuta njia ya kuleta pato na kulitumia kuwakimu wadogo zao baada ya wazazi wao kufariki. Athari hii inatatiza jukumu la ndoa la kulea watoto kama anavyeleza Talcot (1951). Juma na Aisha ambao bado ni watoto wanalazimika kuanza kulea wadogo zao badala ya wao kulelewa. Hii ina maana kuwa wanakosa muda wa kutosha wa kupumzika kwa sababu baada ya kushinda kazini wanaporudi nyumbani wanalazimika kuwashughulikia wadogo zao. Masomo ya Aisha yanakatika kwa sababu ya athari hii. Jamaa za wanandoa na jamii kwa jumla inafaa kuwasaidia watoto yatima ili wasiathirike na hali ya kulelewa na wenzao

**4.3.6 Ndoa za Mapema na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo**

Athari hii inasababishwa na changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi, kutowajibika na umaskini. Athari hii imedhihirishwa na Kamene, Mwanamuka na Maria kupitia usawiri wao kimatendo kwenye riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kamene anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kutekwa nyara na kuozwa kwa lazima. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Siku moja alipokuwa anaenda kukata kuni kwenye pori la serikali karibu na nyumbani, Kamene akatekwa nyara na hatimaye kutoswa kwenye bwawa la ndoa. Maskini hana hata maarifa ya kuogelea. Akalia jamaa yake isimwokoe. Hata jamii nayo (Uk. 90- 91).

Mwanamuka naye anaidhihirisha kwa kusawiriwa kwa kitendo kinachosimuliwa ifuatavyo:

> Ndoa ikaandaliwa. Mama akapewa kiasi fulani cha fedha alizotumia kuwaelimisha wadogo zake Mwanamuka. Mahari ikalipwa, mbuzi watatu. Mwanamuka licha ya umri wake mdogo akagomba. Hivi thamani yangu imekuwa ni mbuzi watatu?" (Uk. 68)

Maria anadhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kutolewa shuleni akiwa katika darasa la tano. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo na mmoja wa wahusika Kaseli Nzeli:

> Mama hujui yaliyomfika Maria alipotolewa shuleni akiwa darasa la tano na kuozwa. Mama akaniangalia na kusema kuwa hakuna anayejua ukweli kama hayo yaliyosemwa yalimfika kusumbuliwa na maradhi fulani- yaliyotokana na kuolewa mapema. (Uk. 114)

Mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaeleza kuwa asasi za kijamii zinaweza kuwa na athari hasi au chanya. Matendo yaliyosimuliwa yanaonyesha athari ya ndoa za mapema ambayo imesababishwa na changamoto za ndoa. Kwa kurejelea maoni ya Kenan( 1983) kuhusu uhusika wa kimatendo madondoo haya yanaonyesha namna athari hii imesawiriwa na Kamene, Mwanamuka na Maria kupitia uhusika wao kimatendo. Kitendo cha kuozwa kwa Kamene kwa lazima na mapema baada ya kukatiziwa masomo kinaonyesha kwamba kinachothaminiwa kwa mwanamke ni mahari na ndoa na wala si elimu. Ndoa inachukuliwa kuwa bwawa kumaanisha ni asasi yenye masuala mengi ambayo anayeshiriki anafaa kuwa na maarifa ya kuyashughulikia. Inaonekana kwamba jamii na jamaa wanaendeleza ubaguzi dhidi ya wanawake kwa sababu kutekwa nyara na kuozwa kwa lazima na mapema kwa Kamene hakupingwi.

Katika dondoo la pili kitendo cha kuozwa kinafuata utaratibu, maandalizi ya ulipaji mahari yanafanywa na Mwanamuka anaoelewa. Hata hivyo kauli ya moja kwa moja imetolewa na Mwanamuka kulalamikia kiasi kidogo cha mahari. Kauli yake inaonyesha mwanamke anathaminiwa kulingana na kiasi cha mahari kinacholipwa katika jamii hii. Kitendo cha mahari kutumiwa kulipia wadogo wa Mwanamuka kinaonyesha kwamba jamii hii inamchukulia mtoto msichana kama kitu cha kuiauni kutokana na matatizo ya kifedha. Dondoo la mwisho linadokeza

athari za ndoa za mapema. Maria katika riwaya hii anakabiliwa na ugonjwa wa kushindwa kudhibiti haja ndogo. Kaseli Nzeli anarejelea huu ugonjwa anapozungumzia ndoa za mapema.

Suala la ndoa za mapema limejadiliwa na wataalamu wa fasihi katika tafiti zao. Katola (2006) anasema ndoa za mapema na za lazima ni njia moja ya kudhulumiwa kwa mwananke na kumyima haki zake. Kuozwa mapema kwa Maria kunamkosesha fursa ya kuendelea na masomo ambayo yangemsaidia kupata kazi ya kuajiriwa na kujitegemea. Wazazi wa Maria wanamuoza mapema kwa sababu ya kushikilia utamaduni potovu wa kuthamini watoto wa kiume kuliko wa kike. Kulingana nao faida ya mtoto wa kike ni mahari na hawaoni haja ya kuendelea kumsomesha. Gicuku (2012) anaeleza namna ya kukabiliana na matendo yanayokiuka haki za watoto kama hili la ndoa za mapema. Anasema serikali inafaa kuimarisha juhudi za kulinda haki za watoto kwa kuwachukulia hatua za kisheria wanaozikiuka. Wanandoa wanafaa kutupilia mbali utamaduni huu ambao unadhalilisha mtoto wa kike kwa kumnyima haki yake. Utafiti huu umetambua ndoa za mapema kuwa athari ya changamoto za ndoa na kuonyesha jinsi ambavyo imedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Athari hii imedhihirishwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kupitia usawiri wa wahusika kupitia kitendo cha kuozwa wakati wangali na umri mdogo.

### 4.3.7 Matatizo ya Kiafya na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kiusemi na Kimatendo

Athari hii imesababishwa na changamoto ya umaskini. Imedhihirishwa na Wamae katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kwa kusawiriwa kiusemi na kimatendo. Msimulizi anasimulia usemi wake kama usemi taarifa siku alipozumgumza na katibu muhtasi wa mbunge wao. Usemi huu unasimuliwa hivi:

> Kwamba umaskini haukuwapata tu bali hata funza, ishara kuu ya umaskini wenyewe, waliamua kujizika kwenye vyanda vyake vya miguu na kama hilo halitoshi wakaamua kuharibu mwendo wake, ni kama hata hana haki ya kutembea kwenye ulimwengu wenyewe (Uk. 181).

Athari hii pia inadhihirishwa na Wamae kupitia usawiri wake kimatendo. Kitendo anachosawiriwa kwacho ni kutembea kwa shida kwa kuvamiwa na funza. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Wamae alipokuwa kijana alisumbuliwa na funza waliomvamia miguu na hata kumfanya ashindwe kutembea vizuri. Wakati walipokwenda shuleni, wanafunzi wenzake, kwa kutambua kuwa alikuwa na funza, walianza kumfanyia stihizai na kumwimbia nyimbo za kumkera:
>
> Wamae, ee Wamae, ana ndutu maguru;
> Wamae ee Wamae, ana ndutu maguru;
> Wamae ee Wamae ana ndutu maguru;
>
> (Wamae, ee Wamae, ana funza miguuni
> Wamae, ee Wamae, ana funza miguuni
> Wamae, ee Wamae, ana funza miguuni) (Uk. 177)

Usemi wa Wamae na kutembea kwake kunadhihirisha kuathiriwa kwake na ndoa ya wazazi wake kulingana na mawazo ya Merton (1957) na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Wazazi wake hawakuwa na pesa za kugharamia matibabu yake kwa wakati unaofaa. Anatembea kwa shida anapokwenda shuleni jambo ambalo linafanya wanafunzi wenzake kumwimbia nyimbo za kumkera. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza nadharia ya naratolojia unaobainisha wahusika kama kipengele cha kuchunguzia na kufafanua mbinu za kuwasawiri wahusika uhusika wa Wamae unachangia udhihihirishaji wa athari hii. Katika dondoo la kwanza usemi wa Wamae unaripotiwa na msimulizi. Usemi huu unaibua hisia za kufedheheka kwa Wamae. Anahuisha funza na kuwalaumu kwa kumdhulumu. Anawalaumu kwa kujizika katika vyanda vyake vya miguu na kumharibia mwendo.

Katika dondoo la pili uhusika wa kimatendo wa Wamae unaonyesha namna kuvamiwa na funza kunatatiza masomo yake. Mbali na kutembea kwa shida akienda au akiwa shuleni anaimbiwa nyimbo za kukejeli na wanafunzi wenzake. Hii inamwongezea fedheha zaidi kuongezea kwa hii ya kuvamiwa na funza. Wamae anatembea kwa shida na hii inafanya ashindwe kutangamana na

kucheza na watoto wenzake jinsi inavyofaa. Kuhudhuria kwake kwa masomo kunatatizwa kwa kuwa analazimika kutoenda shule ili atafute matibabu, pia mwendo wake kwenda shuleni ni wa polepole kwa sababu ya funza miguuni mwake. Athari hii ya matatizo ya kiafya inadhihirishwa tu katika riwaya hii ya *Unaitwa Nani?* kupitia usawiri wa Wamae kimatendo na kiusemi.

### 4.3.8 Ukeketaji wa Wasichana na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo na Kiusemi

Athari hii imesababishwa  na changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi wa kuwakeketa wasichana. Athari hii imedhihrishwa na Kaseli Nzeli katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Ameidhihirisha athari hii kupitia mbinu ya matendo ambayo mwandishi ameitumia kumsawiri. Chatman (1978) anasema kuwa wahusika hushiriki katika matukio ya hadithi na kwa kufanya maudhui ya msanii hudhihirika. Kaseli Nzeli anadhihirisha ukuketaji kwa usemi wake na kwa kushiriki kitendo hiki cha kukeketa. Kitendo hiki kinasimuliwa ifuatavyo:

> Hatimaye niliketi na kufanya nilivyotakiwa kufanya. Nilisogea karibu na alipokuwa ameketi yule mwanamke aliyekuwa na bangili nyingi ajabu. Wenzake wakawa wananiangalia. Kiongozi akajaribu akashindwa. Mara ya pili akiwa amekiuma kidomo chake cha chini, mishipa ya uso imetokeza na kuyang'ariza macho (Uk.111- 112).

Merton (1957) anasema kuwa asasi za kijamii husababisha athari kwa jamii, asasi nyingine za kijamii au watu binafsi. Ndoa ya wazazi wa Kaseli Nzeli inasababisha athari ya ukeketaji kwa kushikilia utamaduni hasi. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia usawiri wa Kaseli Nzeli kwa kitendo kinachosimuliwa katika dondoo hili anadhihirisha athari hii. Kaseli anasimulia namna alishiriki katika kitendo hiki kutokana na shinikizo kutoka kwa wazazi wake, jamaa na jamii kwa ujumla. Anajisalimisha na kufuata maagizo kutoka kwa ngariba. Taswira inayoibuliwa na maelezo ya kitendo cha kuzungukwa na wakeketaji wanaokazana kumkeketa kinaonyesha unyonge wa mhusika. Hata hivyo kwa sababu ambazo hazikuelezwa anashinda wakeketaji kumtahiri na wanatoroka bila kumtahiri. Kitendo anachoshiriki mhusika huyu kinadhihirisha dhuluma wanazotendewa watoto wasichana kutokana na ushikilizi wa huu utamaduni.

Akijadili kitendo hiki Gitau(2011), anasema kuwa kitamaduni ukeketaji wa wasichana ulidhamiria kuthibiti hisia zao za kimapenzi. Haya ni mawazo ya wanajamii ambao wanaendeleza utamaduni huu bila kujali madhara yake kwa wasichana. Nakhumicha (2013) anasema kuwa suala la kukeketa wasichana ni tatizo la kiafya,la haki za kibinadamu na ni njia ya kumdhalilisha mwanamke. Juhudi za kumkeketa Kaseli Nzeli zinatatiza masomo yake na kumkosesha utulivu maishani. Nakhumicha (2013) na Gitau(2011) wanajadili suala hili ingawa utafiti wao hauhusu asasi ya ndoa. Utafiti huu mbali na kujadili athari hii unaeleza namna inadhihirishwa na Kaseli Nzeli kupitia uhusika wake. Jamii na hasa wanandoa wanafaa kuukomesha utamaduni huu hasi kwa kuwa unaathiri maisha ya watoto wasichana. Unatatiza masomo yao, unafanya waolewe wangali wadogo na pia kuwatatiza kisaikolojia. Athari hii imesawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* peke yake na imedhihirishwa na Kaseli Nzeli kupitia uhusika wake kiusemi na kimatendo.

### 4.3.9 Kubaguliwa Kijinsia kwa Watoto na Wazazi na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika wa Kimatendo

Ubaguzi wa watoto kijinsia umedhihirishwa na usawiri kimatendo wa Kamene katika riwaya ya *Unaitwa nani?* Changamoto hii inasababishwa na changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi unaompendelea mtoto wa kiume. Kamene anasawiri athari hii kupitia usawiri wake kwa matendo yafuatayo: Kitendo cha kwanza kinasimuliwa hivi:

> Kamende aliyedhani kuwa atampata mvulana wa kuongeza kikoa chake akachukia mchezo aliochezewa na maumbile. Mama akampokea mtoto wake aliyejaliwa na Muumba wake baada ya kukabidhiwa na wakunga waliomzalisha. Kwa kuona jinsi babake na ulimwengu wenyewe ulivyompokea mwanawe, akaamua kumpa jina Kamene ( babake ambaye kitamaduni ndiye aliyepaswa kupendekeza jina lake hakujali anaitwa nani). (Uk. 90)

Kitendo cha pili ambacho kinamsawiri na kudhihirisha athari hii kinasimuliwa ifuatavyo.

> Shule hakuwahi kuimaliza kama ndugu zake. Babake alisema kuwa elimu ndogo ya shule a msingi ilimtosha (Uk. 90).

Matendo haya mawili yanaonyesha athari ya kubaguliwa kwa watoto kijinsia. Athari hii kwa kurejelea mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu kuhusu athari za asasi za kijamii, inasababishwa na changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi katika ndoa. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia usawiri wa Kamene kimatendo umedhihirisha athari hii jinsi inavyoonekana katika madondoo haya. Kamene anakosa kupewa jina na babake kulingana na utamaduni kwa sababu yeye ni msichana na babake alitarajia mtoto mvulana. Kamende alikuwa tayari ana watoto wavulana na alitarajia kupata kumpata mwingime. Msimulizi anaeleza kuwa Kamende aliona maumbile yamemchezea. Hii inaonyesha matarajio makubwa aliyokuwa nayo ya kupata mtoto mvulana hadi anafikia kiwango cha kulaumu maumbile.

Katika dondoo la pili Kamene anadhihirisha athari hii kwa kusawiriwa kwa kitendo cha kutoendelea na masomo yake licha ya kuwa na nia ya kufanya hivyo. Katika dondoo hili kauli ya babake kuhusu sababu ya kukatiza masomo yake imeripotiwa. Kulingana na babake elimu ya msingi inamtosha. Hii ni kinyume na ndugu zake wa kiume ambao wanapewa fursa ya kuendelea na masomo. Elimu ni muhimu kwa watoto wa jinsia zote kwa kuwa huwafanya kuboresha familia zao (Nakhumicha, 2013). Kumnyima Kamene fursa ya kusoma zaidi kwa kuwa yeye ni msichana ni ubaguzi na unaharibu maisha yake ya baadaye. Karinge (2013) anajadili namna jamii humpendelea mtoto wa kiume na kumyima mtoto wa kike haki yake kama vile haki ya kusoma. Kuwanyima watoto fursa ya kendeleza masomo yao kunakiuka majukumu ya asasi ya elimu jinsi yanavyofafanuliwa na nadharia ya umuundo-uamilifi. Elimu inafaa kuwafunza watoto maarifa, kaida na mali za jamii. Kukatiza masomo ya watoto kunawanyima fursa ya kufaidi jukumu hili. Ubaguzi huu una msingi wake katika utamaduni ambao unamwona mtoto wa kiume kama mrithi wa familia. Matendo anayotendewa Kamene yanatokana na imani kitamaduni kwamba watoto wa jinsia moja ni bora kuliko wa nyingine. Utamaduni unaobagua mtoto wa kike umepitwa na wakati na unafaa kutupiliwa mbali. Haifai wazazi kuwabagua watoto kijinsia na kuwanyima haki, kufanya hivi ni kuwaonea kwa kuwa wao hawakuchagua kuwa wa jinsia ya kiume. Wazazi wanafaa kukubali jinsia ya watoto wanaozaa na kuwatendea haki ili kuwaandaa kwa maisha yao ya baadaye. Ubaguzi wa Kamene unafanya anyimwe haki ya kusoma zaidi  mbali na kuozwa mapema.

Kubaguliwa kwa watoto kijinsia kumejadiliwa na Katola (2006), Nakhumicha 2013) na Karinge (2013) katika tafiti walizofanya. Utafiti huu umebainisha hii kuwa athari ya changamoto ya ushikilizi wa utamaduni hasi. Ufafanuzi umetolewa kuhusu namna athari hii imesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika. Athari hii imedhihirishwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kupitia usawiri wake kwa kitendo cha kukosa kupewa jina na babake baada ya kuzaliwa na masomo yake kukatizwa.

### 4.3.10 Kunajisiwa na Udhihirishaji Wake Kupitia Uhusika Kiusemi

Kunajisiwa kumedhihirishwa na Kasu katika *Maisha Kitendawili* kupitia usawiri wake kiusemi. Usemi huu ni mawazo yake kuhusu kitendo cha kunajisiwa na mjombake. Mawazo haya yanasimuliwa ifuatavyo.

> Mshale wa uchungu ulimfuma Kasu, akakumbuka mjomba wake hasa, nduguye mamake ambaye tayari ameshamtenda yanayokuwa tu siri tu baina yake yeye Kasu na Mola wake (Uk. 72)

Kulingana na mhimili wa pili wa nadharia ya umuundo- uamilifu na maoni ya Merton (1957) asasi za kijamii kama vile ndoa zinaweza kuwa na athari hasi au chanya. Kunajisiwa kumebainishwa kuwa athari ya changamoto za ndoa kwa mujibu wa utafiti huu. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia kuhusu wahusika na mbinu za kuwasawiri, dondoo hili linaonyesha usawiri kiusemi wa Kasu ambao unadhihirisha athari hii. Kunajisiwa kwa Kasu kunadhihirisha kuathiriwa kwake na changamoto ya kifo katika ndoa ya wazazi wake na umaskini na ugomvi katika ndoa ya Marufuku ambaye ni mjombake. Marufuku anamchukua Kasu na Farida ambao ni wapwa wake ili awalee baada ya wazazi wao wote kufariki. Mkewe anaona haikufaa yeye kufanya hivi kwani kutawazidishia mzigo wa kulea kwa kuwa walikuwa maskini. Anaamua kumgombeza Marufuku na kumyima malazi yaani kukataa kuonana naye kimwili. Hii ndio sababu anayoitoa Marufuku ya kumnajisi Kasu. Katika dondoo hili Kasu anawaza kuhusu machungu ya kunajisiwa na mjombake. Anaulinganisha uchungu huu na uchungu wa kufumwa na mshale. Anasikitika kwamba aliyemnajisi ni mjombake, ndugu ya mamake. Anauweka uovu huu siri kubwa. Gicuku (2012) anajadili athari hii anapoijadili ndoa kama asasi liyoshindwa kutekeleza jukumu la kulea watoto. Anasema kuwa kunajisiwa kwa

watoto kuna msingi wake katika kuzorota kwa maadili ya kijamii. Kuzorota kwa maadili kunafanya wazazi na walezi wa watoto kuanza kuwadhulumu badala ya kuwatunza. Anatoa mfano wa baba kumbaka binti yake na mwalimu kumbaka mwanafunzi ambaye anafaa kumlinda. Kasu ananajisiwa na mjombake ambaye anatarajiwa kumpatia ulinzi baada ya wazazi wake wote kufariki. Baada ya Kasu kunajisiwa na mjombake anazongwa na mawazo na kuamua kuacha masomo na kutorokea mjini. Alimwona mjombake kama mnyama na hangestahimili kuendelea kuishi naye. Mjini anakosa kazi na makao thabiti na hatimaye anaolewa na Mjomba kama njia kujiepusha na mahangaiko zaidi maishani mwake.

Matokeo ya utafiti huu yanaibainisha athari hii na kueleza namna inavyosawiriwa na Kasu kupitia uhusika wake kiusemi. Hii inaonyesha namna kifo cha wazazi na umaskini wa walezi wao unaweza kuharibu maisha ya watoto. Wanajamii wote wanafaa kuwajibika kukomesha dhuluma hii kwa kuwafichua wanaoendeleza uovu huu na hatua za kisheria kuchukuliwa. Ulinzi wa kutosha unafaa kutolewa kwa watoto wa kike ili kuzuia visa hivi. Si haki kwa hatua ya kisheria kutochukuliwa dhidi ya mjombake Kasu baada ya kumnajisi. Baada ya Kasu kunajisiwa hatua ya kisheria haichukuliwi dhidi ya mjombake. Jamii haichukui hatua kumfanyia Kasu ushauri nasaha na kumsaidia kuendelea na masomo yake.

Gicuku (2012) anajadili kunajisiwa kwa watoto kama ishara ya ndoa kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kutunza watoto. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kunajisiwa kama athari ya changamoto za ndoa. Mbali na kufanya hivi yanafafanua namna kunajisiwa kunadhihirishwa kupitia usawiri wa wahusika. Katika utafiti huu athari hii imedhihirishwa tu katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* kupitia usawiri wa Kasu kiusemi. Usemi ambao umetumika kumsawiri ni mawazo yake kuhusu jinsi alivyonajisiwa na mjombake.

### 4.4 Njia za Kukabiliana na Changamoto za Ndoa na Jinsi ambavyo Zinawasilishwa na Mbinu za Usimulizi

Sehemu hii inahusu uchanganuzi na uwasilishaji wa data kuhusu njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Mchakato huu unaongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu unaosisitiza umuhimu wa asasi za kijamii kuwa thabiti na kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Umeongozwa pia mhimili wa kwanza na wa tatu wa nadharia ya

naratolojia. Mhimili wa kwanza unabainisha na kufafanua vipengele vya kuchunguzia hadithi kama nafsi za usimulizi, aina za wasimulizi na aina za mitazamo. Mhimili wa tatu unaelezea haja ya kuchambua hadithi kwa kuzingatia masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi husika. Kwa kuongozwa na mihimili hii mitatu changamoto za ndoa zimebainishwa kasha maelezo kutolewa kuhusu mbinu za usimulizi ambazo zimetumika kuziwasilisha. Mbinu za usimulizi ambazo zimezingatiwa ni aina za usimulizi, aina za mitazamo na aina ya wasimulizi jinsi zinavyofafanuliwa na Genette (1980).

Asasi za kijamii ikiwemo ndoa zinafaa kutekeleza majukumu yake ya kijamii ipasavyo ili kuijenga jamii thabiti. Changamoto za ndoa hazina budi kukabiliwa ili kuifanya asasi hii kuwa thabiti na kutekeleza barabara majukumu yake ya kuzaa na kulea kizazi kipya. Sehemu hii inabainisha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zinazojitokeza katika riwaya teule na jinsi ambavyo zimesimuliwa na mbinu za usimulizi. Mbinu za usimulizi ambazo zimezingatiwa ni aina za usimulizi, aina za mitazamo na aina ya wasimulizi. Maelezo yaetolewa na wataalamu mbalimbali kuhusu mbinu hizi. Wamitila (2003b) anatoa ufafanuzi ufuatao kuhusu usimulizi wa nafsi ya tatu, msimulizi horomo na mtazamo wa nje. Usimulizi wa nafsi ya tatu ni aina ya usimulizi ambao unahusisha kuelezea mambo au matukio yanayohusu mtu mwingine. Katika usimulizi huu msimulizi si mmoja wa wahusika katika hadithi inayosimuliwa. Yeye huwa nje ya ulimwengu wa hadithi na kusimulia matukio ya hadithi. Usimulizi wa nafsi ya kwanza hufanywa na mhusika wa nafsi ya kwanza ambaye anaweza kuwa mshiriki au asiwe mshiriki katika hadithi anayosimulia. Msimulizi wa nafsi ya pili hupatikana katika hadithi zinazosimuliwa kwa nafsi ya pili. Mtazamo wa nje unamaanisha kwamba msimulizi anayatazama na kuyasimulia matukio akiwa nje ya hadithi anayosimulia. Mtazamo huu unajitokeza katika hadithi ambayo imesimuliwa kwa nafsi ya tatu. Msimulizi horomo ni msimulizi ambaye hutoa habari tu na kuwaacha wahusika wazungumze wao wenyewe bila kuwaingilia kati au kutoa ushauri na maamuzi fulani ya kimsingi.

Genette (1980) anasema kuwa msimulizi wasifu husimulia matukio ya hadithi ambayo yeye hashiriki naye msimulizi tawasifu husimulia matukio ya hadithi ambayo yeye anashiriki. Katika sehemu hii njia ya kukabiliana na changamoto za ndoa inabainishwa na changamoto ambazo

inatumika kukabiliana nazo kuelezwa na baadaye mbinu za usimulizi zinazotumika kuiwasilisha kuchanganuliwa.

### 4.4.1 Mazungumzo na Jinsi ambavyo Yanawasilishwa na Mbinu Zausimulizi

Mazungumzo yanatumika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya teule. Changamoto hizi ni ukosefu wa uaminifu, kutowajibika, ushikilizi wa utamaduni hasi, na ugomvi. Madondoo yanayodhihirisha matumizi ya mazungumzo kukabiliana na changamoto za ndoa yananukuliwa na kisha maelezo kutolewa kuhusu mbinu za usimulizi zinazotumiwa kuyawasilisha. Mazungumzo yametumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika katika ndoa ya Hasani na Muna kwenye riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. Mazungumzo kati ya wanandoa hawa yanasimuliwa ifuatavyo:

> Lakini unafanya kazi, unapata pesa nzuri zaidi yangu mimi.
> Hiyo sio sababu na wewe unajua sijakataa kukusaidia, lakini kila jambo lina mpaka. Au ndio maana ukanioa? (Uk.189).

Kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoasisiwa na Durkheim karne ya kumi na tisa ndoa inahitaji kuwa thabiti ili itekeleze majukumu yake ipasavyo. Mazungumzo yametumika kukabiliana na kutowajibika katika ndoa ya Muna na Hasani ambako kunaikosesha uthabiti.Hasani alikuwa ameacha kutoa pesa kugharamia mahitaji yao ya nyumba. Hasani alianza kupunguza pesa alizompatia Muna kwa matumizi ya nyumba na baadaye anaacha kumpatia kabisa. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolijia unaofafanua mbinu za usimulizi na wa tatu unaotaka uchambuzi wa usimulizi kufanywa kwa kuhusisha masuala yanayoshughulikiwa, njia hii imesimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Mazungumzo haya yanasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu. Wamitila(2003b) anaeleza kuwa usimulizi wa nafsi ya tatu unahusu usimuliaji wa matukio yanayohusu watu wengine. Tukio hili la mazungumzo linasimuliwa na msimulizi ambaye anasimulia mazungumzo yanayohusu Muna na Hasani na wala si yeye. Msimulizi anasimulia majibizano kati ya Muna na Hasani kuhusu kukataa kwa Hasani kutoa pesa kugharamia matumizi yao wote. Mtazamo unaodhihirika katika mazungumzo haya ni mtazamo wa nje. Genette (1980) anasema kwamba mtazamo wa nje huhusishwa na hadithi ambazo zinasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu.

Mazungumzo haya yamesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu na kudhihirisha mtazamo wa nje. Njia hii imesimuliwa msimulizi horomo kwa kuwa wahusika wameachwa kuzungumza bila msimulizi kuingilia au kutoa maamuzi kuihusu. Katika dondoo hili msimulizi anawaacha Hasani na Muna kujibizana. Muna anaanzisha mazungumzo haya kumtaka Hasani awajibike kwa kutoa pesa kuchangia matumizi yao wote. Kauli ya Hasani inaonyesha kuwa sababu ya kutowajibika inatokana na wivu kuwa Muna anamshinda kwa mshahara. Usemi wa Muna unadhihirisha hisia za maonevu alizo nazo kutokana na sababu anayotoa Hasani ya kutomsaidia. Anakiri kuwa hajakataa kumsaidia lakini kuachiwa mzigo wote ni kumuonea. Anahitimisha kauli yake kwa swali kuonyesha kuwa kuachiwa gharama zote za nyumba huenda ndio sababu fiche ya Hasani kumuoa. Madai ya Hasani kwamba Muna anapata mshahara mwingi kumliko na hafai kulalamika hayana msingi. Wanandoa wanafaa kuelewana kuhusu matumizi ya pato lao ili mmoja asione anaonewa. Mazungumzo haya yanasimuliwa na msimulizi wasifu kwa sababu yanasimuliwa na msimulizi ambaye hayashiriki.

Mazungumzo yanatumika kukabiliana na changamoto ya umaskini na kutowajibika katika ndoa ya Tabu na Ngoma. Mazungumzo haya yanasimuliwa hivi:

> Mama akimuuliza pesa zote anazopata anapeleka wapi, kila siku jibu lake ni kwamba anataka kuongeza gari nyingine. Alianza na mbili, zikawa tatu, sasa nne. Mama akiuliza faida ya gari zote hizo ni nini kama watoto hawana nguo, wanatembelea marapurapu, yeye kazi kumsuta mama kwamba hajui maendeleo. Eti alikuwa anamtishia mama kuwa ataoa mwanamke mwingine anayejua kutafuta pesa (Uk. 125).

Mazungumzo haya yananuiwa kumfanya Ngoma awajibike ili ndoa hii itekeleze ipasavyo jukumu la ndoa la kulea watoto kulingana na Talcot (1951). Ngoma alikuwa na tamaa ya mali, aliongeza idadi ya magari ya kubeba abiria huku mke na watoto wake wakiendelea kuishi kimaskini. Anafanya hivi ili kupata faida nyingi ambayo anaitumia kwa ulevi na uasherati badala ya kuikimu familia yake. Mazungumzo haya hayaafikii suluhu kwa changamoto hii kwa sababu badala ya kutoa suluhu Ngoma anamsuta mkewe na hata kumtisha kuwa ataoa mwanamke mwingine. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa naratolojia unaoeleza kuhusu mbinu za usimulizi na wa tatu kuhusu haja ya kuchambua hadithi kwa kuhusisha usimuliaji wake na

maswala yanayoshughulikiwa, mazungumzo haya yanawasilishwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Yanasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa sababu yanasimuliwa na msimulizi ambaye hayamhusu bali yanahusu wahusika wengine. Njia hii inasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa msimulizi yuko nje ulimwengu wa hadithi na anasimulia mazungumzo haya akiwa nje ya ulimwengu huu. Msimulizi anasimulia maelezo ya Juma kuhusu mazungumzo kati ya wazazi wake kuhusu kutowajibika. Juma anamweleza jirani yao Omolo. Kwa kurejelea mawazo ya Wamitila (2003b) kuhusu mtazamo wa nje msimulizi wa mazungumzo haya hayashiriki. Njia hii imesimuliwa na msimulizi horomo kwa sababu msimulizi amemruhusu Juma kuzungumza anaposimulia tukio hili la mazungumzo baina ya wazazi wake bila kuingilia na kutoa ushauri kuyahusu. Hatimaye njia hii inasimuliwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimulizi anasimulia matukio ambayo yeye hashiriki. Maelezo ya Tabu kwamba watoto wanatembelea marapurapu yanaibua taswira ya umaskini katika ndoa hii na kudhihirisha kushindwa kwake kutekeleza majukumu yake.

Suala la matumizi ya mazungumzo kukabiliana na changamoto za ndoa limejadiliwa na wataalamu wa fasihi katika tafiti zao kuhusu ndoa. Gicuku (2012) anaeleza umuhimu wa mazungumzo katika kusuluhisha changamoto za ndoa. Hufanya wanandoa kuelewana na kutafuta njia bora ya kusuluhisha matatizo yanayowakabili. Njia hii huleta utulivu na kuendleza mapenzi kati ya wanandoa. Kulingana na utafiti huu mazungumzo kati ya Tabu na Ngoma hayatatui shida ya umaskini katika ndoa yao. Hii ni kwa sababu Ngoma hayatilii maanani na badala yake anamsuta na kumtisha mkewe. Hii inaonyesha kuwa mazungungumzo yanaweza tu kutatua changamoto za ndoa ikiwa kila mwanandoa anayatilia maanani.

Nyaosi (2008) anajadili mawasiliano kama njia ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba wanawake walio katika ndoa. Karinge (2013) vile vile anajadili mawasiliano kama njia ya kukabiliana na ndoa bila kuegemea jinsia ya kike kama Nyaosi. Matokea ya utafiti huu yanabainisha matumizi ya njia ya mawasiliano au mazungumzo kukabiliana na changamoto za ndoa. Utafiti huu mbali na kujadili matumizi yake unachanganua mbinu za usimulizi ambazo zimetumika kuiwasilisha katika riwaya teule za Kiswahili. Katika riwaya zote mbili *Ua la Faraja* na *Mwisho wa Kosa* njia hii imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu. Katika *Mwisho wa Kosa* mazungumzo ya moja kwa

moja baina ya wahusika wanandoa yamesimuliwa. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* mazungumzo baina ya wanandoa yanasimuliwa baada ya kutokea.

### 4.4.2 Ushauri Nasaha na Jinsi ambavyo Unawasilishwa na Mbinu za Usimulizi

Njia hii imetumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika na ugomvi katika ndoa ya Muna na Hasani kwenye riwaya ya *Mwisho wa Kosa.* Unatolewa katika kikao cha Hasani na Salimu, babake Muna anayeitwa Said na kakake babake Muna. Ushauri nasaha anaopewa Hasani unasimuliwa hivi:

> Said alimwambia, Masharti yangu ni haya: Kuwa kwanza, lazima umwangalie mkeo kama sheria inavyosema, kwa nguo, chakula, matumizi na haja zake zote." Hasani aliitikia, na baba yake alikubali kuwa hayo ni lazima. Said aliendelea, "Tena, lazima umpe fursa ya kutoka, kuzungumza na kuonana na wenziwe. Pia awe na ruhusa ya kuja hapa kwangu, kwa wazee wake." Hayo pia Hasani aliyakubali. " La tatu , na ambalo kwangu mimi ni muhimu sana, ni kuwa mambo ya kumpiga Muna yasiwepo. Tena napenda ujue kuwa tumekubaliana hapa, sisi wazee wake kuwa ukifanya hayo tena basi tutakuwa na haki ya kukushitaki. Wala hatutomlazimisha Muna arejee tena kwako. Kwa hivyo hii ndiyo fursa yako ya mwisho, kwa upande wetu sisi." (Uk. 246).

Njia hii inatumika ili kuifanya ndoa ya Hasani na Muna kuwa thabiti na kutekeleza majukumu yake katika jamii kama yanavyojadiliwa na Talcot (1951). Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaoeleza kuhusu mbinu za usimulizi na wa tatu unaoeleza kuhusu kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa njia hii inasimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Ushauri nasaha huu unasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa sababu inasimuliwa na msimulizi ambaye hashiriki katika tukio hili la ushauri. Njia hii pia inasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa inasimuliwa na msimulizi ambaye hayashiriki kama mhusika kulingana na maoni ya Wamitila (2003b). Ushauri nasaha huu unasimuliwa na msimulizi horomo kwa sababu Said, babake Muna anazungumza moja kwa moja. Haingilii kati au kutoa maamuzi fulani ya kimsingi kuwahusu kama anavyosema Genette (1980). Said anatoa ushauri kwa hasani kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za ndoa yake na Muna. Said anamtaka Hasani amkimu Muna kwa mahitaji yake, ampatie uhuru wa kutoka na kutangamana, amruhusu

kutembelea wazazi wake na asimpige. Ushauri nasaha huu unaambatana na tahadhari, Hasani anaonywa kuwa akimpiga Muna anaweza kushitakiwa na Muna hangelazimishwa tena kuirudia ndoa yao. Ushauri huu unafuata hatua, Hasani anatakiwa kuhakikisha kukubaliana na kila sharti kabla ya Said kutoa masharti mengine. Said anaonyesha kwamba tabia ya Hasani inakera na haingevumilika tena, anamwambia kuwa anapewa fursa ya mwisho kujirudi. Hasani anakubaliana na masharti ya ushauri nasaha anaopewa katika kikao hiki na anakubaliwa kumchukua Muna na kumaliza utengano wa muda kati yao. Hatimaye njia hii inasimuliwa na msimulizi wasifu kwa kuwa inasimuliwa na msimulizi ambaye yeye hashiriki kama mhusika

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ushauri nasaha umetumiwa kukabiliana na changamoto ya uasherati katika ndoa ya Kasina na wakeze watatu. Kasina alikuwa na wapenzi wengi nje ya ndoa na wengi wao aliwapatia mimba. Kwanza anashauriwa na watu wanaomjua na baadaye nababake.

> Watu waliomjua wakawa wanamshauri aache hiyo tabia ya jogoo kwa sababu ina madhara makubwa, kwamba ulimwengu wanamoishi watu, mtu huvuna alichopanda, naye akaamua kuipuuza maana ya ndani ya methali hii na kupendezwa na ile ya juu (Uk. 239)

Kasina anapewa ushauri nasaha mwingine na babake anapomshuku mkewe kuwa na jicho la nje. Ushauri nasaha huu unasimuliwa ifuatavyo:

> Mzee Usina Sini akaendelea, "Usiwe mjinga kumwacha mkeo kwa sababu za kipumbavu. Ndoa zenu zinavunjika haraka kwa kufuatilia mambo yasiyofaa. Usijaribu ujanja kwa mwanamke, hutamweza! ( Uk. 244)

Mhimili wa kwanza wa naratolojia unafafanua mbinu za usimulizi na wa pili unaeleza haja ya kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa katika hadithi. Kwa kurejelea mihimili hii maelezo yafuatayo yanafafanua mbinu zilizotumika kuwasilisha njia hii. Katika madondoo haya mawili njia hii inasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa inasimuliwa na msimulizi ambaye si mhusika katika riwaya hii. Imesimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa msimulizi

yuko nje ya ulumwengu wa hadithi ya riwaya hii anaposimulia tukio hili jinsi anavyosema Wamitila (2003b) kuhusu mtazamo wa nje. Ushauri nasaha katika madondoo haya mawili umesimuliwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimuli anasimulia tukio linalohusu wahusika wengine. Msimulizi wasifu anaeleza namna watu wanaomjua Kasina walimshauri dhidi ya uasherati. Watu hawa wanatumia methali kumuonya lakini yeye anapuuza. Msimulizi huyu anasema alifurahishwa na maana ya juu kumaanisha alipuuza athari hasi za kitendo hiki na kushikilia ile anasa ya muda mfupi. Ndoa ya Kasina na wakeze inaendelea kudumu licha ya yeye kupuuza ushauri huu na kuendelea na kutokuwa mwaminifu. Anavuna matokeo ya matendo yake anapofika uwanjani siku moja kuwahutubia raia wa eneo lake kama mbuge wao. Watoto wengi aliopata nje ya ndoa wanamjia kumtaka awajibikie mahitaji yao ya makao, chakula na elimu. Jambo hili linamtia aibu mbele ya umati.

Katika dondoo la pili usimulizi unafanywa na msimulizi horomo kwa sababu mhusika ambaye ni Mzee Usina Sini anazungumza moja kwa moja anapotoa ushauri. Kauli yake haingiliwi na msimulizi kwa kutolewa maamuzi au tathmini kulingana na maelezo ya Genette (1980) kuhusu msimulizi horomo. Anaiita sababu ya Kasina kutaka kumuacha mkewe kuwa ya kipumbavu kumaanisha haina maana au msingi. Anaealeza kuwa ndoa za siku hizi huvunjika haraka kwa kufuatiliwa mambo yasiyo muhimu. Anaonya dhidi ya wanawake kufanyiwa ujanja na wanaume kwa kuchukuliwa kuwa hawawezi kukabiliana nao. Mzee Usina anaonya dhidi ya kuvunja ndoa kwa sababu ambazo si muhimu kama vile kushuku kwamba mwanandoa mmoja si mwaminifu. Kauli yake inadhihirisha kwamba katika mahusiano yoyote kwa mfano ndoa tofauti hazikosi kwa kuwa binadamu si mkamilifu. Ni wajibu wa wanandoa kujaribu kutatua tofauti hizi badala ya kukimbilia kuvunja ndoa zao.

Njia hii imetumika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa na ulevi katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Njia hii inasimuliwa ifuatavyo:

> Huko hospitalini alielezwa tatizo lake, "Una shida kubwa ya ini kwa hivyo nakushauri uache pombe!" aliambiwa. Wakati wote anamkodolea macho daktari kana kwamba anamtangazia hukumu ya kifo. Usimwache ajiue huku unaona, Dr. Homo akaniambia. (Uk. 53)

Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa tatu wa nadharia ya naratolojia kuhusu mbinu za usimulizi na kuhusisha usimuliaji na masuala yanayoshughulikiwa njia hii imewasilishwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Ushauri nasaha unaotolewa kwa mujibu wa dondoo hili unawasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza kwa sababu unasimuliwa na Kasekei ambaye ni mhusika katika riwaya hii. Unasimuliwa kwa mtazamo wa ndani kwa sababu msimulizi anashiriki tukio la ushauri nasaha unaotolewa jinsi anavyofafanua Wamitila ( 2003b) kuhusu aina hii ya mtazamo. Njia hii vile vile imesimuliwa na msimulizi tawasifu kwa sababu msimulizi ni mhusika katika hadithi ya riwaya hii na anashiriki katika tukio hili la kutoa ushauri nasaha. Msimulizi anatamka maneno halisi yaliyotamkwa na Dr. Homo wakati wa kumshauri mumewe. Maneno haya yana kihisishi mwisho kuonyesha hofu ya daktari kutokana na kiwango cha kuharibiwa kwa maini ya mumewe Kasekei. Ushauri nasaha huu unatolewa na mtaalamu wa masuala ya afya Dr. Homo. Lengo la ushauri huu ni kumtaka mlengwa kuacha kunywa pombe ili kuokoa afya yake. Afya yake ni muhimu katika kumwezesha kuendelea kutekeleza majukumu ya ndoa yake kwa mujibu wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu iliyoongoza utafiti huu. Pombe ilikuwa imeathiri maini ambayo ni kiungo mhuhimu katika mwili wake. Kukodoa macho kwa mume huyu kunaonyesha kushangazwa na ujumbe wa daktari, kwamba pombe imemdhuru na pia kwa kuambiwa awache jambo ambalo amelizoea na analoliona kuwa gumu.

Akirejelea riwaya hii, Karinge (2013) anajadili namna wahusika wanatumia ushauri nasaha kukabiliana na changamoto katika riwaya ya *Unaitwa Nani*?. Anaeleza namna njia hii imetumika kukabiliana na changamoto ya ugonjwa katika ndoa anapojadili mchango wa wanandoa katika kudumisha ndoa zao. Mumewe Kasekei sawa na Kasina katika riwaya hii anapuuza ushauri anaopewa na kuugua hadi kufa. Kasina anapuuza ushauri nasaha anaopewa kuhusu tabia yake ya uasherati. Ndoa yake inaendelea kukumbwa na shida hii na anaishia kupata watoto wengi nje ya ndoa. Wanandoa hawana budi kuzingatia ushauri nasaha wanaopewa ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili na kujenga ndoa imara.

Katika riwaya ya *Kiu* ushauri nasaha umetumika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa watoto katika ndoa ya Kidawa na Makame. Kidawa alikuwa ameishi na mumewe kwa miaka

mingi bila kupata mtoto na akakaribia kukata tamaa. Kidawa anapewa ushauri nasaha na Bahati ambaye ni shoga yake. Ushauri huu unasimuliwa hivi:

> Bahati akamwuliza, Je, hujapata mtoto bado?
> Akamjibu, Ah, mwaka wa tano huu hata alama. Hata hiyo baraka imeondoka. Mungu atakujalia upate mke na dume, uzae, ujukuu, wawe na kheri na wewe.
> Mungu hamsahau mja wake! (Uk. 69)

Kulingana na Talcot ( 1951) ndoa hutekeleza jukumu la kuzaa na kulea kizazi kipya. Ushauri huu unanuiwa kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa watoto inayotatiza utekelezaji wa jukumu hili. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa tatu wa nadharia ya naratolojia na kwa kuzingatia dondoo hili njia hii imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa sababu imesimuliwa na msimulizi ambaye si mmoja wa wahusika katika riwaya hii, imesimuliwa na msimulizi horomo kwa sababu Kidawa na Bahati katika dondoo hili wameachwa wazungumze wao wenyewe kwa wenyewe bila kuingiliwa. Bahati anamuuliza Kidawa ikiwa hajapata mtoto naye Kidawa anamjibu kuwa amekaa miaka mitano na hata amekosa matumaini. Bahati anampatia Kidawa matumaini kuwa Mungu angemwezesha kupata watoto wa kiume, wa kike na hata wajukuu. Bahati anahitimisha ushauri nasaha wake kwa kutumia methali kumaanisha Mungu bila shaka angemtatulia Kidawa shida hii. Ushauri huu unampatia Kidawa matumaini kuwa Mungu angemwezesha kupata watoto japo haumshauri namna ya kutatua tatizo hili. Huenda hii inatokana na imani kwamba kupata watoto ni majaaliwa na binadamu hana udhibiti kuhusu suala hili. Ushauri huu umewasilishwa na msimulizi wasifu kwa sababu msimulizi wa tukio hili la ushauri nasaha halishiriki.msimulizi wasifu na mtazamo wa nje. Imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi anasimulia mambo yanayowahusu Kidawa na Bahati na wala si yeye. Ushauri nasaha huu unasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa sababu msimulizi wake kwa kurejelea mawazo ya Wamitila (2003b) hashiriki katika tukio hili analosimulia.

Njia hii ya ushauri nasaha vile vile imetumika kukabiliana na ulevi katika ndoa kati ya Tatu na mumewe kwenye riwaya ya *Kiu*. Ushauri anaopewa Tatu na Bahati unasimuliwa hivi:

> “ Mungu atamhidi mumeo,” Bahati alimpa moyo. “Wangapi wakilewa halafu wakaacha. Pengine mumeo naye ata… (Uk. 71)

Ushauri huu unakusudiwa kuifanya ndoa ya Tatu na mumewe kuwa thabiti na kutekeleza majukumu yake kama inavyosisitizwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo-uamilifu. Mumewe Tatu alikuwa akilewa kupindukia na hata wakati mwingine aliwaalika marafiki zake katika nyumba na kunywa pombe nao. Jambo hili liliikosesha ndoa hii utulivu ambao ni muhimu katika kujenga ndoa thabiti. Kwa kuzingatia mawazo ya Genette (1980) kuhusu mbinu za usimulizi na kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa tatu wa nadharia ya naratolojia ushauri nasaha huu umewasilishwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Unasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi anaeleza tukio ambalo linahusu wahusika wengine na wala si yeye. Njia hii inasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa inasimuliwa na msimulizi anayelitazama na kulisimulia tukio hili akiwa nje ya ulimwengu wa hadithi ya riwaya hii. Ushauri nasaha huu unasimuliwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimulizi hashiriki katika tukio hili la kumshauri Tatu. Hatimaye usimulizi huu unasimuliwa na msimulizi horomo kwa kuwa msimuulizi amemuacha Bahati kuzungumza anapomshauri Tatu. Anamshauri kuwa Mungu atamwezesha mumewe kuacha pombe, anampatia matumaini kuwa mumewe anaweza kuacha pombe kwa sababu kuna wale ambao huacha baada ya kuwa waraibu wa pombe.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* ushauri nasaha umetolewa kwa Tabu na Grace ili kukabiliana na ugonjwa wa ukimwi katika ndoa yake na Ngoma. Ushauri huu unasimuliwa hivi:

> Pengine bado hujaambukizwa. Nenda kapime. Japokuwa mimi si mtaalamu wa mambo hayo, nakushauri kabisa uepuke kufanya kitendo na shemeji. Kama yeye ameambukizwa na hao malaya wake asizidi kukuambukiza wewe. Kama akisisitiza, mwambie kwanza akapime ili akuhakikishie usalama wake na wako. Usitegemee sana mipira kwa sababu anaweza kufanya ujanja mpira uchanike. (Uk. 61)

Ushauri nasaha mwingine unatolewa na Daktari Hans kwa Tabu kumwezesha kukabiliana na changamoto ya ugonjwa wa ukimwi. Ushauri nasaha anaotoa Daktari Hans unasimuliwa hivi:

> Ukipima ukajua mapema kwamba una virusi, utajitahidi kuutunza mwili wako ili uweze kuishi zaidi ingawa una virusi. Utatumia maelekezo yetu ya lishe, matibabu ya maradhi ya kawaida na pia kutumia dawa za kupunguza kasi ya kuongezeka kwa virusi. Ukitumia dawa hizo vizuri zitaongeza muda wako wa kuishi… (Uk. 186)

Ushauri nasaha unaotolewa na Tabu na Daktari Hans unalenga kukabiliana na changamoto ya ugonjwa ambao umeifanya ndoa hii kukosa uthabiti ambao unafaa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unafafanua mbinu za usimulizi na wa pili unasisitiza kuwa uchambuzi wa hadithi unafaa kuhusisha usimuliaji wake na masuala yanayoshughulikiwa. Kwa kuzingatia mihimili hii njia hii imewasilishwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Njia hii imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa sababu inasimuliwa na msimulizi anayeeleza tukio linalohusu wahusika wengine ambao ni Grace, Tabu na Daktari Hans. Msimulizi huyu anasimulia ushauri nasaha ambao Grace anampatia Tabu na pia ule ambao Daktari Hans anampatia Tabu. Ushauri nasaha wa Grace kwa Tabu unamtaka Tabu kupima kujua ikiwa ameambukizwa na kuwa mwangalifu ili asije akaambukizwa na mumewe ikiwa bado hajaambukizwa. Ushauri nasaha wa Daktari Hans unamfafanuliwa Tabu faida ya kupima ili kujua ikiwa ana ukimwi na namna ya kuongeza muda wa kuishi hata baada ya kupatikana na virusi vya ukimwi. Ushauri nasaha anaopewa Tabu unasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa msimuli anausimulia akiwa nje ya ulimwengu wa hadithi ya riwaya hii. Ushauri nasaha huu katika madondoo haya mawili unasimuliwa na msimulizi wasifu, msimulizi huyu anasimulia tukio hili lakini halishiriki. Hatimaye njia hii inawasilishwa na msimulizi horomo kwa kuwa wahusika Tabu na Daktari Hans wameachwa na msimulizi kuzungumza wanapotoa ushauri nasaha. Grace katika ushauri anaotoa kwa Grace anaonyesha huruma kwa Tabu na chuki kwa Ngoma, anamchukia kwa uasherati wake na malaya ambao umemweka dadake katika hatari ya kuambukizwa ukimwi. Anamtahadharisha dadake dhidi ya kushiriki naye mapenzi hata kama ni kwa kutumia mpira kabla hajapimwa. Anatumia tafsida kutoa tahadhari hii kwa kumwambia aepuke kufanya kitendo. Anaonyesha kutomwamini Ngoma hata kama watatumia mpira. Daktari Hans anamshauri Tabu kuhusu manufaa ya kupima mapema na kugunduliwa kuwa na virusi. Hii inawezesha mgonjwa kupata huduma za kimatibabu na kuishi kwa miaka mingi.

Matumizi ya ushauri nasaha kukabiliana na changamoto za ndoa yamejadiliwa na Gicuku (2012) na Karinge (2013) katika tafiti zao kuhusu ndoa. Gicuku (2012) anasema kuwa wanandoa wanafaa kushauriana na kuelewana badala ya kulaumiana na kunung'unika. Ndoa ya Hasani na Muna ambayo ilikosa uthabiti na kukaribia kuvunjika inakuwa imara tayari kutekeleza majukumu yake ya kijamii kulingana na nadharia ya umuundo- uamilifu inayoongoza utafiti huu. Karinge (2013) anajadili namna wahusika wanatumia ushauri nasaha kukabiliana na changamoto katika riwaya ya *Unaitwa Nani*?. Anaeleza namna njia hii imetumiwa na wahusika katika riwaya hii kukabiliana na changamoto za ndoa zao. Utafiti huu umechunguza njia ambazo zimetumika kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa ndani, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu, msimulizi tawasifu na msimulizi horomo. Katika riwaya hii imesimuliwa kwa mbinu nyingi za usimulizi kuliko katika riwaya nyingine. Katika riwaya ya *Kiu* njia hii imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* njia hii imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu. Usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo ndizo mbinu za usimulizi ambazo zimetumika kwa wingi katika riwaya teule kusimulia njia hii.

### 4.4.3 Msamaha na Jinsi ambavyo Umewasilishwa na Mbinu za Usimulizi

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* njia hii imetumiwa kukabiliana na changamoto ya uasherati na talaka katika ndoa kati ya Ngoma na Tabu. Matumizi yake katika kukabiliana na uasherati yanasimuliwa ifuatavyo:

> Huko nyuma alikwishajua kuwa Ngoma alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Queen. Alikwisha wafumania Kanga Moja Club. Wakagombana na Queen. Tabu akasusiana na mumewe kwa muda wa karibu juma zima. Wakawa hawaongei wala kusalimiana. Ngoma akamwomba mke wake msamaha, akasamehewa. Akaapa kwamba hatarudia tena uhusiano na mwanamke huyo. Kwa shingo upande, Tabu akamwamini. (Uk. 31)

Kulingana na nadharia ya umuundo- uamilifu uthabiti wa ndoa unahitajika ili kuifanya itekeleze majukumu yake ipasavyo. Ndoa ya Tabu na Ngoma ilikumbwa na uasherati na kutowajibika ambako kuliifanya ishindwe kulea watoto ipasavyo. Msamaha umetumiwa ili kukabiliana na changamoto hii. Msamaha unaondoa kimya kati ya wahusika hawa ambacho kilizuka baada ya Tabu kumfumania Ngoma akiwa na mpenzi wake Queen. Kwa kuejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia na mawazo ya Genette (1980) kuhusu mbinu za usimulizi na kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa njia hii imesimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Msamaha katika dondoo hili unasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi anaelezea matukio yanayowahusu wahusika wengine, Tabu na Ngoma. Msahaha huu unasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa sababu msimulizi yuko nje ya ulimwengu wa hadithi ya riwaya hii na anasimulia tukio hili akiwa nje. Njia hii inawasilishwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimulizi hashiriki tukio hili la kusameheana kwa Tabu na Ngoma. Msimulizi anaeleza kuwa Tabu alimwamini mumewe shingo upande kumaanisha alishuku kwamba mumewe hataachana na uasherati. Tabu anamsamehe mumewe ili kuondoa uhasama kati yao lakini Ngoma harekebishi makosa yake jinsi anavyoahidi. Anaendelea na tabia ya uasherati na hata kuishia kumwambukiza mkewe ugonjwa wa ukimwi. Ili msamaha uchangie kukabiliana na changamoto za ndoa anayesamehewa anafaa kuthamini msamaha anaopewa na kurekebisha makosa yake.

Gicuku (2012) anaeleza kuhusu matumizi ya msamaha kukabiliana na changamoto za ndoa. Anasisitiza haja ya mke au mume kuomba msamaha kosa linapotokea na kujirekebisha. Ni muhimu pia kusahau makosa baada ya kutoa msamaha na wala si kuyahifadhi. Anaeleza kuhusu manufaa ya msamaha kwa kusema kuwa unaweza kuleta utulivu katika ndoa ikiwa wanandoa wataomba msamaha kwa dhati na kurekebisha makosa yao. Kutokana na utafiti huu mhusika Ngoma anaomba mkewe msamaha anapogundua kwamba ni muasherati lakini baada ya kusamehewa anaendelea na tabia hii. Anaendelea hadi anaambukizwa ukimwi na kumuambukiza mkewe. Katika hali hii kuomba msamaha na kusamehe hakuleti utulivu katika ndoa.

Katika riwaya ii hii ya *Ua la Faraja* njia hii msamaha unatumiwa kukabiliana na changamoto ya talaka kati ya Tabu na Ngoma. Njia hii inawasilishwa hivi:

> Nisamehe mke wangu," alijikusuru kusema na machozi yakatoka tena. Mke wake akayafuta. Na Tabu machozi yakaanza kutoka, lakini hakujali kuyafuta. Ngoma akaendelea, " Nisamehe kwa yote niliyotenda. Waambie watoto wanisamehe. (Uk. 292)

Njia hii inatamatisha talaka ambayo ilikuwa imefanya wanandoa hawa kutengana kurudiana na kuendeleza jukumu la kulea watoto ambalo limebainishwa na Talcot (1951). Ngoma anaomba mkewe na watoto msamaha kwa kuwatelekeza na kushiriki uasherati ambao unafanya aambukizwe ukimwi na kumwambukiza mkewe. Kulingana na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia tukio hili la kuomba msamaha linasimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi kwa kurejelea maelezo ya Genette (1980) kuzihusu. Msamaha katika dondoo hili unasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi anaelezea matukio ambayo hayamhusu bali yanahusu wahusika wengine ambao ni Tabu na Ngoma. Msahaha huu unasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa sababu msimulizi anasimulia tukio hili akiwa nje ya ulimwengu wa hadithi ya riwaya hii. Njia hii inawasilishwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimulizi hashiriki tukio hila la kusameheana kwa Tabu na Ngoma. Njia hii imesimuliwa na msimulizi horomo kwa sababu msimulizi amemwacha Ngoma kuzungumza na kuomba msamaha bila kuingilia kwa kutoa maoni au tathmini. Anatiririkwa na machozi ishara ya kujutia makosa aliyoitendea familia yake. Ngoma anaomba msamaha wakati yu katika kitanda cha hospitali akiwa hali mahututi. Hatimaye anafuta talaka na kuaga dunia muda mfupi baadaye. Neno 'nisamehe' limerudiwa katika kauli ya Ngoma ili kusisitiza kuhusu msamaha anaoomba. Wanandoa wanafaa kuombana msamaha wanapokosea mapema katika ndoa yao. Ngoma anaomba msamaha wakati yu hali mahututi kutokana na kuugua ukimwi, baada ya familia yake kusambaratika na watoto wake kutatizika kimasomo.

Matokeo ya utafiti huu sawa na ya utafiti wa Gicuku (2012) yanabainisha msamaha kama njia ya kukabiliana na changamoto za ndoa. Hata hivyo matokeo ya utafiti huu yanaonyesha namna njia hii imewasilishwa na mbinu za usimulizi katika riwaya teule. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* njia hii imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Msamaha katika ndoa ya Tabu na Ngoma kwa mara ya kwanza unaleta tu utulivu wa muda kwa kuwa Ngoma harekebishi makosa yake. Msamaha wa mwisho anaoomba

Ngoma unakuja mwisho wakati yu hali mahututi. Hata hivyo unamwacha Tabu kama mke halali na mrithi wa mali ya Ngoma baada ya kifo.

### 4.4.4 Uvumilivu na Jinsi ambavyo Unawasilishwa na Mbinu za Usimulizi

Njia hii imetumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika, ugomvi na umaskini katika ndoa ya Kidawa na Makame katika riwaya ya *Kiu*. Njia hii inasimuliwa hivi:

> Nikwambie nini mambo ya Bwana huyo! Nikikueleza kutwa hayeshi. Na utoshe huo wivu aliokuwa nao; na litoshe hilo domo lake. Si wa nguo si wa kula, yeye mwambie wivu na hamaki tu- basi! Lakini navumilia.(Uk. 68).

Ndoa hii inakosa uthabiti ambao ni muhimu katika kuiwezesha ndoa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu na maoni ya Talcot (1951). Makame alikuwa na wivu na hakutekeleza ipasavyo jukumu la kuikimu ndoa yake kwa mahitaji ya kimsingi kama vile nguo na chakula. Isitoshe alikuwa mwingi wa hasira. Kidawa anaamua kuvumilia ili kudumisha ndoa yake. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia njia hii imesimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi kulingana na maelezo ya Genette ( 1980) kuzihusu. Njia hii inasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi wa tukio hili si mmoja wa wahusika katika riwaya hii. Njia hii inasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa msimulizi anasimulia tukio hili akiwa nje ya ulimwengu wa hadithi anayosimulia. Tukio hili linasimuliwa na msimulizi wasifu. Hii ni kwa sababu msimulizi anasimulia matukio ambayo hashiriki. Hatimaye njia hii inasimuliwa na msimulizi horomo kwa sababu msimulizi amemwacha mhusika Kidawa kuzungumzia changamoto za ndoa na uamuzi wake wa kuvumilia moja kwa moja bila kuingilia. Hisia zake za kukerwa zinadhihiriswa na kauli fupifupi anazotumia kuzieleza na matumizi ya alama hisi mwisho wa baadhi ya kauli hizi. Makame alikuwa hawajibiki kuikimu familia yake, alikuwa hamwamini mkewe na alipenda kuzua ugomvi. Kidawa anasisitiza kutowajibika kwa mumewe kwa kutumia mbinu ya tabaini katika usemi wake. Hii inadhihirishwa na matumizi ya ‘ si wa nguo si wa kula’. Matumizi ya kihisishi mwisho wa neno ‘basi’ yanaonyesha kauli hii inatolewa kwa hisia zinanoonyesha kukerwa sana na tabia ya Makame.

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* inatumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika na ugomvi. Njia hii inasimuliwa ifuatavyo:

> Hasani alizidi kuona kuwa kupiga ndio njia nyepesi ya kushinda katika mabishano yake na mkewe, kwa hivyo alichukua njia hiyo kila mara. Muna alistahamili hayo kwa muda na kujaribu kujihami kama alivyoweza, lakini wakati ulifika alipohisi hawezi tena. ( Uk. 224)

Ndoa hii ilikosa uthabiti umbao unahitajika kuifanya kutekeleza majukumu yake ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu. Muna anavumilia kupigwa na Hasani na pia kuachiwa gharama zote za nyumba yao ili kudumisha ndoa yao. Alifanya hivi kwa kutumai kuwa Hasani angebadilika na ndoa yao iwe thabiti. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia imewasilishwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi si mmoja wa wahusika katika riwaya hii kulingana na maelezo ya Wamitila (2003) kuhusu usimulizi wa aina hii. Imesimuliwa kwa mtazamo wa nje. Hii ni kwa sababu msimulizi anaisimulia akiwa nje ya ulimwengu wa hadithi ya riwaya hii. Kwenye dondoo hili njia hii imesimuliwa na msimulizi wasifu kwa sababu msimulizi anayesimulia hashiriki tukio linaloiibua. Katika riwaya hii haijawasilishwa na msimulizi horomo kama ilivyo katika riwaya ya *Kiu* kama ilivyo katika dondoo la hapo juu. Muna anaamua kuvumilia zaidi na kuamua kuondoka kwa muda na kurudiana tena na Hasani baada ya Hasani kupewa ushauri nasaha na babake Muna.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* njia hii imetumika kukabiliana na changamoto ya umaskini, ulevi, kutowajibika, ukosefu wa uaminifu na ugomvi katika ndoa ya Tabu na Ngoma. Njia hii inasimuliwa hivi:

> Ila alitoa kisingizio kwamba baba na mama yake na ndugu zake watamlaumu kwa kuvunja ndoa iwapo ataamua kuachana na Ngoma. Pia alioogopa kwamba jamii itamcheka kwa kuwaachia malaya wamchukue mume wake na kuacha watoto wao wapate shida kutokana na wazazi wao kufarakana. Aidha aliogopa Mungu atamlaani

> kwa kuvunja kiapo cha ndoa alichoapa pale walipofunga ndoa hii. Visingizio hivi ndivyo vilivyomfanya avumilie na kuubeba mzigo mkubwa wa ndoa ile. ( Uk. 113)

Njia hii inawezesha ndoa hii kudumu na kuendelea kutekeleza jukumu la kulea watoto lililobainishwa na Talcot (1951). Katika dondoo hili Tabu anaeleza sababu za kuvumilia na kuendelea kuhangaika kuwalea watoto wake. Aliogopa lawama kutoka kwa wazazi wake, jamii na Mungu. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia njia hii imewasilishwa kwa mbinu zifuatazo. Imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi wa tukio hili si mhusika katika ulimwengu wa riwaya hizi. Pia imesimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa sababu msimulizi anasimulia matukio haya akiwa nje ya hadithi za riwaya hii. Tukio hili linasimuliwa na msimulizi wasifu kwa sababu msimulizi anasimulia tukio ambalo hashiriki. Tofauti na uwasilishaji wa njia hii katika riwaya ya *Kiu*, hapa njia hii haiwasilishwi kwa msimulizi horomo. Wahusika hawajapewa nafasi ya kuzungumzia kuvumilia kwao moja kwa moja.

Keringe (2013) anajadili mchango wa wanandoa katika kuimarisha ndoa zao. Anaeleza namna wahusika wanandoa wanavumila shida zinazowakumba ili kudumisha ndoa zao badala ya kuzivunjilia mbali. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha namna mbinu hii inatumika kudumisha ndoa licha ya changamoto zinazozikabili. Kidawa katika *Kiu*, Tabu katika *Ua la Faraja* na Muna katika *Mwisho waKosa* wanazidumisha ndoa zao kwa kuvumilia. Utafiti huu mbali na kuonyesha ufaafu wa mbinu hii katika kudumisha ndoa unafafanua mbinu za usimulizi ambazo zimetumika katika riwaya teule kuziwasilisha. Katika riwaya ya *Kiu* uvumilivu umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* uvumilivu umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, msimulizi wasifu na kwa mtazamo wa nje. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje na msimulizi wasifu. Uvumilivu japo unafanya ndoa iendelee kudumu unamkosesha furaha mwanandoa ambaye anadhulumiwa. Kuvumilia kwa Tabu katika *Ua la Faraja*, Muna katika *Mwisho wa Kosa* na Kidawa katika *Kiu* kunafanya wakose furaha na kuendelea kuishi kwa masikitiko. Anayedhulumu anafaa kuikumbatia hatua ya mwenzake kuamua kuvumilia kujirudi na kujitahidi kusuluhisha shida za ndoa yao. Si haki kwa

anayedhulumu kuendelea kudhulumu huku mwenzake akijitahidi kuvumilia ili kudumisha ndoa yao.

### 4.4.5 Kuanzishwa kwa Mradi wa Kuleta Pato na Jinsi ambavyo Kumewasilishwa na Mbinu za Usimulizi

Kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato kumetumika kukabiliana na umaskini. Njia hii inasimuliwa ifuatavyo katika riwaya ya*Unaitwa Nani?* :

> Nikafungua banda dogo la kuuzia matunda, vinywaji na maua karibu na mtaa tunamoishi, karibu na lango la kuingia kwenye hospitali kuu jijini. Na kweli baada ya muda nikaanza kuona mabadiliko. Nikaweza kupata pesa za kufanyia mambo ya kimsingi. Na mwenyewe nikahisi huru kwa kiasi fulani. (Uk. 54)

Njia hii imetumika kukabiliana na umaskini uliokumba ndoa hii na kuifanya kukosa uthabiti na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kulea watoto kama yanavyobainishwa na Talcot (1951). Gicuku(2012) anasema kuwa ndoa ikikosa mahitaji ya kimsingi huwa ni vigumu kuiendesha. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza wa nadharia ya naratolojia unaeleza kuhusu mbinu za usimulizi na mhimili wa pili wa nadharia hii unaoeleza kuhusu kuhusisha usimulizi na masuala yanayoshughulikiwa njia hii inasimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Njia hii inawasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza kwa kuwa inasimuliwa na Kasekei ambaye anashiriki katika tukio hili la kuanzisha mradi. Kulingana na Genette(1980) usimulizi wa aina hii hufanywa na msimulizi anayesimulia mambo yanayomhusu. Kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato kunawasilishwa kwa mtazamo wa ndani. Hii ni kwa sababu tukio hili limesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza kulingana na maelezo ya Genette (1980) kuhusu mtazamo huu. Njia hii inasimuliwa na msimulizi tawasifu ambaye ni Kasekei. Kasekei anasimulia tukio hili la kuanzisha mradi ambalo anashiriki. Kasekei anaanzisha biashara ndogo baada ya mumewe Agusto kufilisika na kuzama katika ulevi na kufanya familia kukosa mahitaji muhimu kama chakula. Anakopa mtaji wa kuanzisha biashara hii kutoka kwa mjombake. Ugumu aliokuwa nao wa kuiendesha ndoa hii unapungua anapoanzisha biashara hii. Anaweza kugharamia mahitaji yake ya kimsingi kama chakula na kuhisi yuko huru kwa kuweza kujitegemea.

Kuanzisha kwa mradi wa kuleta pato kumetumika kukabiliana na changamoto ya umaskini na kutowajibika katika ndoa ya Tabu na Ngoma kwenye *Ua la Faraja*. Njia hii inasimuliwa hivi:

> Ndipo Juma akaanza, " Huko nyuma kote baba alikuwa hamjali mama wala kujali kumpa pesa za chakula na mahitaji ya nyumbani. Ikabidi mama aanze ule mradi wa genge, kuoka maandazi na chapati. Alhamdulilahi, Mungu akabariki biashara hizo. Mama akawa anaingiza faida ya kutosha kuilea familia.
> (Uk. 124)

Ndoa ya Tabu na Ngoma ilikumbwa na umaskini na kupata ugumu kutekeleza jukumu la kulea watoto ipasavyo kulingana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umuundo- uamilifu kuhusu majukumu ya ndoa. Umaskini huu unatokana na babake Juma kutumia pato lake kwa ulevi na uasherati na kuitelekeza familia. Pato analopata kutokana na biashara hii inamwezesha kukidhi mahitaji ya kimsingi ya familia hadi Ngoma anapobadilika na kuanza kuikidhi familia kwa mahitaji haya. Kwa kurejelea mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya naratolojia njia hii inasimuliwa kwa mbinu zifuatazo za usimulizi. Njia hii inasimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa msimulizi hashiriki hili tukio la kuanzishwa kwa mradi. Pia yeye si mhusika katika riwaya hii. Njia hii inasimuliwa kwa mtazamo wa nje kwa kuwa msimulizi wa tukio hili halishiriki. Aidha njia hii imesimuliwa na msimulizi horomo kwa kuwa msimuli wake amewaacha mhusika Juma kuzungumza bila kuingilia wala kutoa ushauri. Hatimaye njia hii inasimuliwa na msimulizi wasifu kwa kuwa msimulizi wake hashiriki katika hii shughuli ya kuanzisha mradi. Msimulizi anamwacha Juma kueleza namna mamake alianzisha biashara ndogo ili kukabiliana na imaskini.

Gicuku (2012) japo matokeo ya utafiti wake hayabainishi hii kama njia ya kukabiliana na changamoto ya ndoa, anasema kuwa kuafikiwa kwa uthabiti wa kifedha katika ndoa huchangia kuiimarisha. Utafiti huu unaibanisha na kufafanua njia za usimulizi ambazo zimetumika kuiwasilisha. Kuanzisha mradi wa kujipatia pato kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu kunazipatia ndoa zilizorejelewa afueni kidogo kutokana na umaskini. Kutokana na biashara ndogo ambazo Tabu na Kasekei wanaanzisha wanaweza kugharamia mahitaji ya kimsingi ya familia zao. Biashara hizi zinawapatia uhuru fulani kwa kuwa zinawaepusha na utegemezi.

Hata hivyo biashara hizi hazisuluhishi kikamilifu shida ya umaskini katika ndoa hizi. Hii ni kwa sababu ya faida ndogo inayopatikana kutokana nazo pengine kutokana na mtaji mdogo na uwezo wa chini kiuchumi wa wateja waliolengwa. Faida hii inamezwa na mahitaji mengi ya familia na kutoacha akiba ya kuzipanua ili kuongeza faida. Faida anayopata Tabu haimwezeshi kugharamia mahitaji yake na ya wanawe kikamilifu. Hii inafanya mwanawe Juma kuacha kuendelea na masomo na kuajiriwa ili amsaidie. Njia hii inaweza kufanikisha kukabiliana kikamilifu na umaskini ikiwa wanaoianzisha miradi watakuwa na mtaji wa kutosha kuanzisha miradi mikubwa ya kuleta faida nyingi. Mbali na mtaji wanahitaji ujuzi wa kuendesha miradi mikubwa inayoanzishwa na kufanya uamuzi wa busara kuhusu miradi ya kuanzishwa na wateja wanaolengwa. Bila haya kufanywa miradi inayoanzishwa inawezesha wanandoa kupata afueni ya muda  na umaskini kuendelea.

**4.5 Hitimisho**

Katika sura hii data imechanganuliwa na kuwasilishwa chini ya sehemu tatu. Katika sehemu ya kwanza changamoto za ndoa zimebainishwa na maelezo kutolewa kuhusu namna kila changamoto inasawiriwa na wahusika kupitia uhusika wao. Changamoto ambazo zinasawiriwa na wahusika kupitia uhisika wao kimatendo na kiusemi peke yake ni; talaka, kutowajibika, ukosefu wa watoto, ushikilizi wa utamaduni hasi na ugomvi. Changamoto  ya kifo imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo peke yake. Changamoto ya ulevi, umaskini na magonjwa imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo.

Katika sehemu ya pili athari za changamoto za ndoa zimebainishwa na maelezo kutolewa kuhusu namna zinadhihirishwa na wahusika kupitia uhusika. Athari ambazo zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi peke yake ni kutatizika kimasomo na matatizo ya kiafya. Athari ambazo zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wa kimatendo peke yake ni ajira ya watoto, chuki ya watoto kwa wazazi, huzuni na ukiwa, watoto kuachiwa jukumu la ulezi, ndoa za mapema, ukeketaji wa watoto, kubaguliwa kwa watoto kijinsia na kunajisiwa. Athari ambayo zimedhirishwa kupitia uhusika wa kimatendo, kimazingira na kiusemi ni ukosefu au upungufu wa mahitaji bora ya kimsingi.

Njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimebainishwa na mbinu za usimulizi zilizotumika kuziwasilisha kuelezwa. Njia ambazo zimebainishwa ni mazungumzo, ushauri nasaha, msamaha, uvumilivu na kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato. Mazungumzo, msamaha na uvumilivu umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo peke yake. Ushauri nasaha na kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa ndani, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu, msimulizi horomo na msimulizi tawasifu.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa nyingi ya changamoto zinazoikumba ndoa zimesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi. Muonekano wa nje umetumika kusawiri magonjwa na umaskini. Uhusika wa kimazingira umetumika kusawiri umaskini na pia ugonjwa. Athari nyingi za changamoto za ndoa zimesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo. Ni athari mbili tu, ya kutatizika kimasomo na ya matatizo ya kiafya ambazo zimesawiriwa kwa uhusika wa kimatendo na usemi pekee. Athari ambayo imesawiriwa kwa uhusika wa kimazingira, kimatendo na kiusemi ni moja tu ambayo ni ukosefu au upungufu wa mahitaji bora ya kimsingi. Njia ya kunzishwa kwa mradi wa kuleta pato na ushauri nasaha ndizo ambazo zimewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtazamo wa ndani na msimulizi tawasifu tofauti na nyingine.

# SURA YA TANO
# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ina sehemu mbalimbali kama vile muhtasari, mahitimisho na mapendekezo. Sehemu ya kwanza itatoa muhtasari wa matokeo kwa mujibu wa madhumuni yaliyobainishwa katika sura ya kwanza na kufuatwa na sehemu ya mahitimisho. Baada ya mahitimisho kuna sehemu ya mapendekezo kutokana na matokeo ya utafiti na pia kuhusu utafiti wa baadaye.

## 5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina sura tano, sura ya kwanza ni utangulizi. Kwenye sehemu hii usuli wa utafiti huu umejadiliwa. Swala la utafiti huu limefafanuliwa na lengo, maswali na madhumuni ya utafiti kuorodheshwa. Misingi ya utafiti huu imebainishwa na kufuatwa na maelezo kuhusu nadharia zilizoongoza utafiti huu. Sura ya pili inahusu uhakiki wa maandishi. Katika sura hii uhakiki wa maandishi ya awali kuhusu mada ya utafiti umefanywa na pengo la utafiti kubainishwa. Uhakiki umefanywa kuhusu changamoto za ndoa, athari zake na njia za kukabiliana nazo. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Maelezo yametolewa kuhusu muundo wa utafiti huu, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data na vifaa vya kukusanyia data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data na hatimaye maadili ya utafiti yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Sura ya nne inahusu uchanganuzi, uwasilishaji na mjadala wa matokeo. Sura hii imegawanywa kwa sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ina mjadala kuhusu changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimasawiriwa na wahusika kupitia usawiri wao. Sehemu ya pili ina mjadala kuhusu athari za changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Sehemu ya tatu ina mjadala kuhusu njia za kukabiliana na changamoto za ndoa na jinsi ambavyo zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Sura ya tano inahusumuhtasari, mahitimisho na mapendekezo.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuafikiwa kwa madhumuni yaliyobainishwa katika sura ya kwanza. Madhumuni ya kwanza yalilenga kueleza jinsi changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa na wahusika kupitia usawiri wao. Utafiti huu umegundua kuwa ndoa

katika riwaya teule za Kiswahili inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto za ndoa zilizobainishwa ni; ulevi, talaka,uasherati, umaskini, kutowajibika, ukosefu wa watoto, magonjwa, kifo, ushikilizi wa utamaduni hasi na ugomvi. Changamoto hizi zimesawiriwa na wahusika kupitia mbinu mbalimbali za kusawiri wahusika. Ulevi umejengwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Kiu* na *Ua la Faraja*. Umejengwa kwa kusawiri wahusika kwa kitendo cha kushiriki ulevi. Umejengwa kwa uhusika wa muonekano wa nje katika riwaya ya *Kiu* peke yake. Changamoto hii vile vile imejengwa kwa uhusika wa kimazingira katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Haya ni mazingira ya baa ambamo Ngoma anakunywa pombe.

Changamoto ya Talaka imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya ya *Kiu*. Hii imefanywa kwa kumsawiri Idi kuitia kitendo cha kumtaliki Bahati na usemi unaoambatana na kitendo hiki. Talaka imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Hii inatokana na kitendo cha kumsawiri Ngoma cha kumtaliki Tabu. Uasherati umesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Kiu*, *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?*. Kitendo ambacho kimetumika kuwasawiri wahusika na kuisawiri changamoto hii ni kuwa na mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa. Umaskini umesawiriwa kupitia uhusika wa Kiusemi, kimatendo na kimazingira katika riwaya ya *Kiu*. Cheusi katika riwaya hii anausawiri kupitia kusawiriwa kwa usemi wa kukiri yeye ni maskini, mazingira ya nyumba duni anamoishi na pia kitendo cha kuombaomba kinu. Umaskini pia umesawiriwa kwa uhusika wa kimazingira katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Katika riwaya hii umesawiriwa na mazingira ya nyumba ndogo inayovuja paa na kuta ambamo Mama Josii anaishi. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* umasikini umesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi wa Tabu. Anatoa kauli ya kuonyesha kuwa watoto wake walivaa nguo mpya kwa nadra. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani*? Umaskini umesawiriwa kupitia uhusika wa muonekano wa nje. Mamake Mwanamuka anaisawiri kwa kuvalia gauni ambalo lina mashimo na kuonyesha mabega yaliyoparara.

Kutowajibika kumesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo peke yake katika riwaya ya *Kiu*. Hii ni kutokana na kitendo ambacho kimetumika kumsawiri Jaku cha kuondoka nyumbani na kutomsaidia mkewe na mtoto. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* kutowajibika kumesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo wa Ngoma na uhusika wa kiusemi wa Tabu.

Ngoma anasawiri kutowajibika kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kuacha kumkimu mkewe na watoto naye Tabu anafanya hivi kupitia kauli yake kwamba Ngoma hamtunzi yeye na watoto.

Katika *Mwisho wa Kosa* kutowajibika kumesawiriwa kuitia uhusika wa kimatendo na kiusemi wa Hasani. Kitendo kinachomsawiri na kusawiri kutowajibika ni kukataa kumpatia Muna pesa za matumizi yao wawili. Usemi wake wa kudai hana pesa na kumtaka Muna agharamie mahitaji yao wawili peke yake unamsairi na kuchangia usawiri wa changamoto hii.

Changamoto ya ukosefu wa watoto imesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi na kimatendo wa wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* na ya *Kiu*. Changamoto hii imesawiriwa na wahusika katika riwaya hizi mbili kupitia kitendo cha kukaa muda mrefu bila kupata mtoto. Katika *Kiu* Kidawa anaisawiri kupitia usemi wa kuonyesha anatamani kupata mtoto lakini hajapata. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kitonga anaisawiri kupitia usemi wake kuelezea kukasirishwa kwake na kukaa muda mrefu bila kupata mtoto. Mwanamuka anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kauli anayotoa kuelezea kuhuzunika kwake kutokana na kitendo cha mumewe kumpa mimba msichana wao wa kazi kwa kuwa walikuwa wamekosa kupata mtoto. Magonjwa yamesawiriwa kupitia uhusika kimatendo, kiusemi, wa muonekano wa nje na wa kimazingira katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Tabu na Ngoma wanausawiri kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kuugua ugonjwa wa ukimwi. Wahusika hawa wawili wanasawiri magonjwa kupitia kusawiriwa kwao kwa mazingira ya wodi ya wagonjwa wa ukimwi ambamo wanalazwa. Tabu anaisawiri changamoto hii kupitia kusawiriwa kwake kwa kauli anayotoa kueleza kuwa ana virusi vya ukimwi. Ngoma anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa usemi anaotoa kuelezea maumivu yake kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Ngoma pia anasawiri magonjwa kupitia kusawiriwa kwake kwa muonekano wa nje. Muonekano huu ni mwili wake uliodhoofika mno. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Magonjwa yamesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo. Yamesawiriwa kuitia matendo ambayo yametumiwa kusawiri Purupesa na pia Maria. Purupesa anasawiriwa kwa kitendo cha kuugua tezi- shahawa naye Maria anasawiriwa kupitia kitendo cha kuugua ugonjwa wa kutodhibiti haja ndogo.

Changamoto ya kifo imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na *Ua la Faraja*. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* kifo kimesawiriwa kupitia kusawiriwa kwa Mzee Omar na mkewe Kibibi kwa kitendo cha kufa mmoja baada ya mwingine. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* kifo kimesawiriwa na Ngoma na Tabu kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kufa kutokana na ukimwi.

Changamoto ya kushikilia utamaduni hasi imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kamene anaisawiri changamoto hii kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kumbagua mtoto wake msichana anayezaliwa kwa kuwa alitarajia mtoto mvulana na baadaye kukatiza masomo yake na kumuoza huku akiacha wavulana kuendelea. Mamake Kaseli Nzeli anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kumshinikiza bintiye kushiriki ukeketaji na kauli za kumlaumu ngariba wanaposhindwa kumkeketa. Lusweti anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kukaa na kutaka kuhudumiwa na mkewe na pia kwa kitendo cha kutotaka mkewe kuuliza kuhusu kuadimika kwake nyumbani na kauli anayotoa kusisitiza jambo hili.

Changamoto ya ugomvi imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Tabu anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kumzaba Ngoma kofi. Tabu na Ngoma wanasawiri ugomvi kupitia kusawiriwa kwao kwa usemi, wanajibizana kuhusu matatizo ya ndoa yao. Katika *Mwisho wa Kosa* ugomvi umesawiriwa na Hasani na Muna kupitia uhusika wao kimatendo na kiusemi. Wanausawiri kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kupigana. Aidha wanausawiri kupitia kusawiriwa kwa usemi, wanajibizana kuhusu matatizo ya ndoa yao. Muna anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kuvunja vitu vya nyumba. Hasani anaisawiri changamoto hii kupitia kusawiriwa kwake kwa kauli anayotoa kwa sauti kupinga pendekezo la Muna kumtaka azoe kusoma. Katika *Maisha Kitendawili* ugomvi umesawiriwa kupitia uhusika wa kiusemi wa mke wa Marufuku. Mke huyu anaisawiri kupitia kusawiriwa kwake kwa kauli anazotoa kumtusi mume wake usiku.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu ni kutathmini namna athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili. Athari ambazo zimebainishwa ni kutatizika kwa masomo ya watoto wa wanandoa, ukosefu au upungufu wa

mahitaji bora ya kimsingi, ajira ya watoto, ukiwa, huzuni na chuki ya watoto kwa wazazi, watoto kuachiwa jukumu la ulezi, ndoa za mapema, matatizo ya kiafya, ukeketaji wa wasichana, kubaguliwa kijinsia kwa watoto na wazazi na kunajisiwa. Athari hizi zimedhihirishwa na wahusika kupitia mbinu mbalimbali ambazo zimetumika kuwasawiri. Kutatizika kimasomo kumedhihirishwa katika riwaya ya *Kiu* kupitia uhusika kimatendo wa Bahati. Bahati anadhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kupitia kitendo cha kufeli mtihani. Katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* athari hii imedhihrishwa kupitia usawiri wa Agne, Jane, Josii na ndugu zao tisa kwa kitendo cha kutoenda shuleni. Katika *Ua la Faraja* imedhihirishwa na Juma na Aisha kupitia usawiri wao kiusemi na kimatendo. Juma anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kulazimika kwenda sokoni kumnunulia mamake bidhaa za kuuza kabla ya kwenda shuleni na pia kukatiza masomo yake ili kumsaidia mamake. Aisha anaidhihirisha kwa kukatiza masomo yake anapofika darasa la saba. Juma vile vile anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwa usemi wa kueleza kuzorota kwake kimasomo.

Athari ya ukosefu au upungufu wa mahitaji ya kimsingi imesawiriwa kupitia usawiri wa Rose, Kasu, Farida, Agnes, Jane, Josii na ndugu zao tisa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Rose anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kwa kauli anayotoa kueleza namna yeye na ndugu zake walikosa chakula na viatu. Kasu katika riwaya hii anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kimazingira, mazingira haya ni mtaa duni anamoishi. Anaisawiri pia kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kuhamahama. Kasu na Farida wanaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kulalia malazi mabovu. Agnes, Jane na ndugu zao tisa wanadhihirisha athari hii kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kulalia karatasi. Bahati katika riwaya ya *Kiu* anaidhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kimazingira. Mazingira haya ni chumba chake duni.

Ajira ya watoto imedhihirishwa na Juma na Aisha katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Juma na Aisha wanaidhihirishwa kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kufanya kazi katika kiwanda wakiwa na umri mdogo. Wamae na ndugu zake wanadhihirisha ajira ya watoto kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kufanya kazi katika mashamba ya mkonge na mananasi wakiwa na umri mdogo.

Chuki ya watoto kwa wazazi, huzuni na ukiwa umedhihirishwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia usawiri wa Juma na Aisha. Juma anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kiusemi, anasema kuwa hampendi babake. Juma pia anadhihirisha chuki kwa wazazi kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kukataa kwenda kumuuguza babake anapolemewa na ukimwi. Huzuni umedhihirishwa na Juma kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kulia mfululizo kwa siku tatu baada ya mamake kufariki. Mhusika huyu anadhihirisha ukiwa kupitia uhusika wake kiusemi. Anafanya hivi kupitia kusawiriwa kwake kwa mawazo kuhusu kuachwa pweke na wazazi wake wote. Aisha anadhihirisha huzuni kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kulia usiku baada ya kusikia mamake akilia kwa kuambukizwa ukimwi na babake

Watoto kuachiwa jukumu la ulezi ni athari ambayo imedhihirishwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* kupitia usawiri wa Juma na Aisha. Juma na Aisha wanaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwao kwa kitendo cha kufanya kazi ili kupata pato na kulitumia kulea wadogo zao. Juma anafanya kazi ya kuendesha gari la kubeba abiria aliloacha babake naye Aisha anafanya kazi katika kiwanda.

Ndoa za mapema ni athari ambayo imesababishwa na ushikilizi wa utamaduni hasi. Imedhihirishwa kupitia usawiri wa wahusika kimatendo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Kamende na Mwanamuka katika riwaya hii wanadhihirisha ndoa za mapema kupitia usawiri wao kwa kitendo cha kuolewa wakiwa na umri mdogo. Kamende anaozwa na babake na kutekwa nyara hadi kwa mume naye Mwanamuka anaozwa na kuondoka kwenda kwa mumewe.

Matatizo ya kiafya yamedhihirishwa na mhusika mmoja katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Wamae anaidhihirisha athari hii kupitia usawiri wake kiusemi. Usemi wake unahusu kuvamiwa kwake na funza ambao wanaharibu mwendo wake. Wamae pia anaidhihirisha athari hii kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kutembea kwa shida kwa sababu ya funza walio katika miguu yake

Ukeketaji wa wasichana umedhihirishwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kupitia usawiri wa Kaseli Nzeli. Anadhihirisha athari hii kupitia uhusika wake kiusemi na kimatendo. Anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kushiriki ukeketaji na usemi wake

anaposimulia jinsi alivyojisalimisha na kushiriki kitendo hiki na juhudi za ngariba kumkeketa na hatimaye kushindwa.

Kubaguliwa kijinsia kwa watoto kumedhihirishwa na Kamene kupitia usawiri wake katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Anaidhihirisha kupitia kusawiriwa kwa kitendo cha kubaguliwa na babake na kutopewa jina na babake baada ya kuzaliwa kwa sababu yeye ni msichana na babake alitarajia kupata mvulana. Aidha anaidhihirisha athari hii kupitia kusawiriwa kwake kwa kitendo cha kukatiziwa masomo yake na babake na ndugu zake wa kiume kuachwa kuendelea na masomo. Babake alidai kuwa elimu ndogo ya shule ya msingi ilimtosha kwa kuwa yeye ni msichana.

Kunajisiwa kunajitokeza kama athari ya changamoto za ndoa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Athari hii imesawiriwa na Kasu kupitia kusawiriwa kwake kiusemi katika riwaya hii. Kunajisiwa kumedhihirishwa naye kupitia kusawiriwa kwa mawazo kuhusu jinsi alivyonajisiwa na mjombake jambo ambalo limemtia uchungu moyoni na ameliweka siri mpaka sasa.

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu ni kufafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Mbinu ambazo zimetumika kukabiliana na changamoto za ndoa ni mazungumzo, ushauri nasaha, msamaha, uvumilivu na kuanzisha mradi wa kuleta pato. Njia hizi zimewasilishwa kwa mbinu mbalimbali za usimulizi katika riwaya teule. Mbinu zilizozingatiwa ni aina za usimulizi, aina za wasimulizi na aina za mitazamo.

Mazungumzo yametumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. Njia hii vile vile imetumika kukabiliana na changamoto ya umaskini na kutowajibika katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Katika riwaya hizi mbili njia hii imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu.

Ushauri nasaha umetumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika na ugomvi katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. Imetumika pia katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kukabiliana na changamoto ya uasherati, magonjwa na ulevi. Katika riwaya ya *Kiu* imetumika kukabiliana na ukosefu wa

watoto na ulevi. Kwenye *Ua la Faraja* imetumika kukabiliana na changamoto ya magonjwa. Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* katika matumizi yake kukabiliana na uasherati imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo. Kwenye riwaya hii katika kukabiliana na changamoto ya magonjwa njia imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtazamo wa ndani na msimulizi tawasifu.

Msamaha umetumika katika riwaya ya *Ua la Faraja* kukabiliana na changamoto ya uasherati na talaka katika ndoa ya Ngoma na Tabu. Njia hii imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje na msimulizi wasifu. Msimulizi anasimulia jinsi Tabu aliamua kumsamehe Ngoma kwa uasherati na kisha jinsi Ngoma baadaye alimsamehe Tabu na kufuta talaka.

Uvumilivu umetumika kukabiliana na changamoto ya kutowajibika, ugomvi na umaskini katika riwaya ya *Kiu* na *Mwisho wa Kosa*. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imetumika kukabiliana na umaskini, ulevi, kutowajibika na ugomvi. Katika riwaya hizi zote njia hii imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje na msimulizi wasifu. Katika riwaya ya *Kiu* mbinu ya msimulizi horomo imetumika mbali na hizi mbinu ambazo zimetajwa.

Njia ya kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato imetumika katika riwaya ya *Ua la Faraja* na ya *Unaitwa Nani?* kukabiliana na umaskini. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imesimuliwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtazamo wa ndani na msimulizi tawasifu.

## 5.3 Hitimisho

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalihitaji kueleza jinsi changamoto za ndoa zimesawiriwa na wahusika kupitia usawiri wao. Changamoto za ndoa katika riwaya teule zimesawiriwa kupitia mbinu mbalimbali za kusawiri wahusika. Changamoto za ndoa zimebainishwa na maelezo kutolewa kuhusu namna kila changamoto imesawiriwa na wahusika kupitia uhusika. Changamoto ambazo zimesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi peke yake ni;

talaka, kutowajibika, ukosefu wa watoto, ushikilizi wa utamaduni hasi na ugomvi. Changamoto ya kifo na uasherati imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo peke yake. Ulevi umesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo, kiusemi, kimazingira na wamuonekano wa nje. Umaskini umesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo, kimazingira, kiusemi na wa muonekano wa nje. Magonjwa yamesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo, kimazingira, kiusemi na wa muonekano wa nje. Baadhi ya changamoto za ndoa zimesawiriwa kwa mbinu tofauti za kusawiri wahusika katika riwaya moja. Kwa mfano umaskini umesawiriwa katika riwaya ya *Kiu* kwa uhusika wa kimatendo, kiusemi na kimazingira. Magonjwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* yamesawiriwa kwa uhusika wa kimatendo, kiusemi, kimazingira na wa muonekano wa nje. Baadhi ya changamoto zimesawiriwa kwa mbinu tofauti za kuwasawiri wahusika katika riwaya teule. Kwa mfano talaka imesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi katika *Kiu* na kupitia uhusika wa kimatendo peke yake katika *Ua la Faraja*. Kuna changamoto ambazo zimesawiriwa kupitia uhusika wa aina moja katika riwaya zaidi ya riwaya moja. Kwa mfano uasherati umesawiriwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Kiu*, *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?*. Imebainika kuwa hata pale ambapo changamoto ya ndoa imesawiriwa kwa mbinu moja ya kusawiri wahusika, matumizi ya mbinu hii hutofautiana kutegemea riwaya. Kwa mfano ugomvi umesawiriwa kwa uhusika wa usemi katika riwaya ya Ua la Faraja, *Mwisho wa Kosa* na *Maisha Kitendawili*. Katika *Mwisho wa Kosa* na *Ua la Faraja* usemi unahusu majibizano kati ya wanandoa. Katika *Maisha Kitendawili* usemi unahusu kauli za Mke wa Marufuku kumtukana mumewe.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu ni kutathmini jinsi athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao. Changamoto za ndoa zinasababisha athari mbalimbali kwa watoto wa wanandoa. Athari hizi ni; kutatizika kwa masomo ya watoto wa wanandoa, ukosefu au upungufu wa mahitaji bora ya kimsingi, ajira ya watoto, ukiwa, huzuni na chuki ya watoto kwa wazazi, watoto kuachiwa jukumu la ulezi, ndoa za mapema, ugonjwa, ukeketaji wa wasichana, kubaguliwa kijinsia kwa watoto na wazazi na kunajisiwa. Athari hizi zimedhihirishwa na wahusika kupitia mbinu mbalimbali za kuwasawiri. Athari ambazo zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wao kimatendo peke yake ni ajira ya watoto, ndoa za maema, watoto kuachiwa jukumu la ulezi na kubaguliwa kijinsia kwa watoto. Athari ambazo zimedhihirishwa na wahusika kupitia uhusika wa kimatendo na kiusemi ni matatizo ya kiafya,

ukeketaji wa wasichana, chuki ya watoto kwa wazazi, huzuni na ukiwa, kutatizika kimasomo na kunajisiwa. Ukosefu au upungufu wa mahitaji ya kimsingi umedhihirishwa na wahusika kupitia kusawiriwa kwao kimatendo, kiusemi na kimazingira. Kuna athari ambazo zimedhihirishwa kupitia zaidi ya mbinu moja ya kuwasawiri wahusika katika riwaya moja. Kwa mfano athari ya kutatizika kimasomo imesawiriwa kwa uhusika wa kimatendo na kiusemi katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Kuna athari ambazo zimedhihirishwa kwa mbinu tofauti za kusawiri wahusika katika riwaya tofauti. Kwa mfano kutatizika kimasomo kumedhihirishwa kupitia uhusika wa kimatendo peke yake katika *Kiu* na uhusika wa kimatendo na kiusemi katika *Ua la Faraja*. Kuna athari ambazo zimedhihrishwa kupitia uhusika wa ina moja lakini kwa namna tofauti. Kwa mfano ajira ya watoto imedhihirishwa kupitia uhusika wa kimatendo katika riwaya ya *Ua la Faraja* na *Unaitwa Nani?* Tofauti ni kuwa katika *Faraja Ua la* imedhihirishwa na Juma kwa kusawiriwa kwa kitendo cha kufanya kazi katika kiwanda na katika *Unaitwa Nani?* Wamae na nduguze wanaidhihirisha athari hii kwa kusawiriwa kwa kitendo cha kufanya kazi katika mashamba ya mkonge na mananasi.

Madhumuni ya tatu ya utafiti huu ni kufafanua jinsi njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto za ndoa zimesawiriwa katika riwaya teule. Njia za kukabiliana na changamoto za ndoa ambazo zimejitokeza ni mazungumzo, msamaha, uvumilivu, ushauri nasaha na kuanzisha mradi wa kuleta pato. Njia hizi zimesimuliwa kwa mbinu mbalimbali za usimulizi. Baadhi ya njia hizi zimewasilishwa kwa mbinu sawa za usimulizi katika riwaya teule. Kwa mfano mazungumzo yamewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo katika riwaya ya *Ua la Faraja* na *Mwisho wa Kosa*. Njia ya kuanzishwa kwa mradi wa kuleta pato imewasilishwa kwa mbinu tofauti za usimulizi katika riwaya ya *Ua la Faraja* na ya *Unaitwa Nani?* Katika riwaya ya *Ua la Faraja* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi horomo na msimulizi wasifu. Katika *Unaitwa Nani?* imewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtazamo wa ndani na msimulizi tawasifu. Uvumilivu umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo katika riwaya ya *Ua la Faraja* na *Kiu*. Njia hii imewasilishwa kwa mbinu sawa na hizi katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* ijapokuwa mbinu ya msimulizi horomo. Ushauri nasaha umewasilishwa kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa

ndani, msimulizi wasifu na msimulizi horomo katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa, Ua la Faraja* na *Kiu*. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* njia hii imewasilishwa kwa mbinu sawa na hizi na nyingine kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, mtazamo wa ndani na msimulizi tawasifu. Msamaha umewasilishwa katika riwaya ya *Ua la Faraja* kwa usimulizi wa nafsi ya tatu, mtazamo wa nje, msimulizi wasifu na msimulizi horomo.

## 5.4 Mapendekezo ya Kijumla Kutokana na Matokeo ya Utafiti

Kutokana na matokeo haya utafiti huu unapendekeza yafuatayo:

1. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha matumizi ya uhusika katika kujenga masuala ya kijamii katika kazi za kifasihi likiwemo suala la changamoto za ndoa. Uhakiki wa kina wa masuala ya kijamii likiwemo suala la changamoto za ndoa unaweza kufanywa tu kwa kushirikisha vipengele zaidi vya fani kwa mfano matumizi ya lugha na mandhari. Hii ni kwa sababu maudhui katika kazi za kifasihi hujengwa kwa ushirikianao wa vipengele kadha vya fani na wala si uhusika peke yake.

2. Utafiti huu unaonyesha namna athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa na wahusika kupitia usawiri wao. Utafiti huu umebaini kuwa ndoa ina athari hasi na chanya na uhakiki wa kina kuhusu athari zake unafaa kuhusisha hizi athari zote kupitia uhusika na vipengele vingine vya fani na wala si kujikita katika udhihirishaji wa athari za changangamoto zake peke yake kupitia uhusika.

3. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa na mbinu za usimulizi. Ili kuhakiki kikamilifu usimulizi wa masuala  ya kijamii katika kazi za kifasihi vipengele vyote vya usimulizi vinafaa kuzingatiwa na wala si vichache tu jinsi ilivyo katika utafiti huu.

## 5.5 Mapendekezo Kuhusu Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye.

1. Utafiti huu umezingatia kipengele cha wahusika cha kuchunguzia hadithi kuhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa. Inapendekezwa kwamba utafiti wa baadaye uhakiki ubunilizi wa changamoto za ndoa kwa kuzingatia vipengele vingine vya fani kwa mfano matumizi ya

lugha na mandhari. Hii ni kwa sababu masuala ya kijamii katika kazi za kifasihi hujengwa kwa vipengele kadha vya fani na uhakiki wa kina kuhusu ujenzi wake unafaa kuhusisha vipengele kadha na wala si kimoja tu jinsi ilivyo katika utafiti huu.

2. Utafiti huu umechunguza athari za changamoto za ndoa jinsi zinavyodhihirishwa na wahusika ambao ni watoto wa wanandoa au wanaolelewa nao. Nadharia ya umuundo-uamilifu inaeleza kuwa asasi za kijamii kama vile ndoa zinafaa kuchanganuliwa kwa kuzingatia athari zake kwa watu binafsi, makundi ya kijamii au jamii kwa ujumla. Inapendekezwa kwamba utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu namna athari za changamoto za ndoa zinadhihirishwa kupitia usawiri wahusika ambao ni wanandoa, jamii au jamaa zao.

3. Utafiti huu umefafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zimewasilishwa kwa mbinu za usimulizi ambazo ni nafsi za usimulizi, aina za wasimulizi na aina za mitazamo. Uhakiki kikamilifu wa usimulizi wa masuala katika kazi za kifasihi unaweza kuafikiwa kwa kutumia vipengele zaidi vya usimulizi. Inapendekezwa utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa zinawasilishwa na mbinu zaidi za usimulizi kama vile aina za usimulizi, daraja za usimulizi na wakati.

## MAREJELEO


Akivaga, S. K& Odaga, A. B (1982). *Oral literature: A school certificate course*. Nairobi, Kenya: Heineman (K)

Ann, C. & Samuel, C. (2007). *Literature and its writers*: *A compact introduction to fiction, poetry and drama(4th ed)*. Boston, Newyork: University of Connecticut.

Burhani, Z. (1987). *Mwisho wa kosa.* Dar-es-salaam, Tanzania:Longhorn.

Charles, Z. (2008). *Introduction to* social *work and social welfare:Empowering people*. U. S. A:Thomson Brooks/Cole.

Chatman, S. (1978). *Story and discourse infiction&film*. Ithica, New York NY: Cornell University Press.

Creswell, J. W. (1998). *Qualitative inquiry & Research design: Choosing among five traditions*. London, England: Sage.

Durkheim, E. (1962). *Orality and technologizing of the world*. NY: Methuen Press.

Genette, G. (1980). *Narrative discourse.*Ithica, *New* York:Cornell University Press.

Gicuku, M. (2012). *Usawiri wa maudhui ya ndoa katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia.*(Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Gichinga, E. M. (2005).*Marriage counselling. A counselling guide*. Nairobi, Kenya: GEM Counselling Services.

Giddens, A. (2006). *Sociology* (5th ed.) U.S. A: Polity Press.

Gitau, E.N. (2011). *Unyanyasajidhidi ya wanaume katika fasihi andishi ya Kiswahili*. ( Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Glare, P. G. W ed (2000) *Oxford latin dictionary*. Bath:The Bath Press

Habwe, J. (2000). *Maisha kitendawili.*Nairobi, Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

Haralambos, M., Martin, H. & Robin H. (2004). *Sociology: Themes and perspectives (6thed.)* London, England: Collins Education.

Ilomo, L. F. (2015). *Mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao*. Mulika 34 (2015)

Katola, E. (2006). *Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia ya kiswahili*. ( Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Karinge, E. ( 2013). *Usawiri wa ndoa katika riwaya ya Unaitwa Nani ?* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Kinara,G. (2012). *Maudhui ya ukimwi katika Ua la Faraja na Kala Tufaha* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Kenan, R. S. (1983). *Narrative fiction: Contemporary poetics*. London, England: Routledge.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi, Kenya: Heineman.

Kinara, G. (2012). *Maudhui ya ukimwi katika Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*. (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Kombo, K. D. & Tromp A. L. D. (2006). *Proposal and thesis writing*: *An introduction.* Nairobi, Kenya: Paulines Publications Africa.

Macious, J. J. (2002). *Society: The basics* (6th *ed.*).Upper saddle River, New Jersey:Pearsons Education.Mberia, W. K. (1997 a). *Natala*. Nairobi, Kenya: Marimba.

Masua, J. M. (2016) *Demographic & spatial- temporal dimensions of marital instability and its effects on the family livelihood in Machakos County, Kenya*. (PhD thesis). Kenyatta University.

Merton, R. K. (1957). *Social theory & social structure*. New York: The free Press.

Mkufya, W. E. (2005). *Ua la Faraja*. Nairobi, Kenya :Longhorn.

Mohamed, S. M. (1972). *Kiu*. Nairobi, Kenya: Longhorn.

Mohochi, S. M. (2000). *Usimulizi wa riwaya ya nyongo Mkalia Ini*. Nordic Journal of African Studies 9 (2): 49- 50 (2000)

Monika, F. (2009). *An introduction to narratology*. London& New York: Routeledge Taylor& Francis Group.

Mugenda, M. O & Mugenda, G. A. (2003). *Research methods: Quantitative & qualitative approaches*. Nairobi, Kenya: Acts Press.

Mugenda, G. A. ( 2011) *Social science research methods*: *Theory and practice.*

Nairobi, Kenya: ARTS press.

Murungi, G. K. (2013). *Mtindo unavyoendeleza maudhui katika Natala*. ( Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Nakhumicha, W. M. ( 2013 ). *Narrative voice and focalization in the narration of generational conflicts in selected kiswahili noveles.*(PhD thesis) University of Bayreuth, Bayreuth.

*Njogu, K. & Chimera, R. (1999). Ufundishaji wa fasihi, nadharia na mbinu.* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Nyamete, F. *Ufafanuzi wa vichocheo vya migogoro ya kindoa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea na Ken Walibora, Kenya*. International Journal of Advaned Education and Research. 9(9): 19-27 (2000)

Nyaosi, N. K. (2008). *Taswira ya asasi ya ndoa katika riwaya mbili za Kiswahili, Kiu na Msimu wa Vipepeo.* ( Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Odhiambo, E. S. O. (2013). *Social dimensions of marital conflicts in Kenya*. Journal of power, politics & Governance 1(1) December 2013

Patton, M. Q. ( 1990 ) *Qualitative evaluation and research methods.* Beverlly Hills, C A : Sage publications.

Patton, M. Q. (2002). *Qualitative research methods* ( *6 th ed.*). London: Sage Publications.

Prop, V. (1968). *Morphology of the folktale*. Austin Texas: University of Texas.

Sounders M. Lewis P. & Thornhill A. ( 2011 ). *Research methods for business students* ( 5 th ed ). Pearson: New Delhi.

Schaefer, R.T. (2008). *Sociology* (11 th ed.*)*. New York, U. S. A:Mcgraw – Hill.

Scott, A. & Laura, D. E. (2007). *Sociology in the contemporary era.* California, U. S. A:Pine Forges Press.

Selfe, P. (1993). *Alevel sociology*: *Trends and patterns* (2 nd ed). London: Macmillan Press ltd.

Talcott, P. (1951). *The social system*. Glencoe, IL: Free Press.

Torodov, T. (1969). *French literary theory today*. New York: Combridge University Press.

Vidya, B. & Sachdeva, D. R. (2007). *An introduction to sociology*.22- A Sarojini Naidu Marg, India: Kitab Mahal.

Wamitila, W. K. (2002). *Uhakiki wa fasihi. Misingi na vipengele vyake*. Nairobi, Kenya:Phoenix.

Wamitila, W. K. (2003 a). *Kichocheo cha fasihi, simulizi na andishi*. Nairobi, Kenya: Focus.

Wamitila, W. K. (2003 b). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Nairobi, Kenya : Focus Publications Ltd.

Wamitila, W. K. (2008 a).*Unaitwa nani?* Nairobi, Kenya : Vide- Muwa.

Wamitila, W. K. (2008 b). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi, Kenya: Vide- Muwa.

## VIAMBATANISHO

### A. Orodha ya uchunzaji

| **Madhumuni ya utafiti** | **Sifa za nukuu za kukusanywa kutoka kwa riwaya teule za Kiswahili kama data za utafiti** |
|---|---|
| Kueleza jinsi changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimesawiriwa kupitia usawiri wa wahusika | Nukuu zinazoonyesha changamoto ya ndoa na zile zinazotaja matendo, matamshi, mawazo, muonekano wa nje na mazingira yanayosawiri wahusika wanaoibua changamoto iliyoonyeshwa. |
| Kutathmini namna athari za changamoto za ndoa zimedhihirishwa kupitia usawiri wa wahusika katika riwaya teule za Kiswahili. | Nukuu zinazoonyesha athari ya changamoto za ndoa na pia zile zinazotaja matendo, matamshi, mawazo, muonekano wa nje na mazingira yanayosawiri wahusika na kuidhihirisha athari iliyoonyeshwa. |
| Kufafanua namna njia za kukabiliana na changamoto za ndoa katika riwaya teule za Kiswahili zimewasilishwa kupitia mbinu za usimulizi. | Nukuu ambazo zinaonyesha njia za kukabiliana na changamoto za ndoa. Nukuu hizi zinaweza kuwa usimulizi wa msimulizi, mawazo ya wahusika, kauli za wahusika au matendo yao. |

**B. Mpangilio wa muda wa utafiti**

| **Kazi** | **Wakati** |
|---|---|
| Kuandika pendekezo la utafiti | Miezi 4 |
| Kukusanya data | Mwezi 1 |
| Kuchanganua data | Miezi 2 |
| Kuandika tasnifu na kuiwasilisha | Miezi 5 |

**C. Makadirio ya matumizi ya pesa**

| **Shughuli** | **Gharama** |
|---|---|
| 1. Vitabu | 8,500/= |
| 2. Kutoa nakala | 15,000/= |
| 3. Uchapishaji | 29,000/= |
| 4. Karatasi, Kalamu | 2,500/= |
| 5. Matumizi mengine | 15,000/= |
| **JUMLA** | **70,000/=** |